


SAUTI ISIYOJULIKANA

 Habari za asubuhi, marafiki. Nina furaha sana kurudi kanisani tena, asubuhi ya leo, baada ya juma la... la kumrudishia ibilisi mafua yangu, kila dakika chache, mnajua. Kila wakati anaponikabidhi, ninamrudishia. Nasi tungali tunapigana. Nimeyakinia tu yeye hana budi kubaki nayo. Mnaona? Kila anaponikabidhi, ninayasukuma tu na kumrudishia. Mnaona? Ananikabidhi, nami ninamrudishia. Kwa hiyo ye—yeye ni bingwa kwa kuirudisha, hata hivyo, mnajua. Bila shaka anajua jinsi ya kufanya hivyo. Lakini hatimaye tutamchosa, ama kuuchosha uvumilivu wake, kama nilivyosema hivi majuzi usiku.

² Jamaa alisema, wakati mmoja, aliombewa, naye akasema, “Vema,” kasema, “ibilisi aliniambia siku ponywa.” Ndipo kasema, “Niliangalia chini,” kasema, “dalili zangu zote zilikuwa pale, kama tu zilivyokuwa hapo mwanzo.” Naye akasema, “Vema, nikasema, ‘Shetani, hiyo—hiyo—hiyo ni kweli, sioni tofauti yoyote. Lakini wajua nini? Mpaka zitakaponiondokea, nitashuhudia tu kwa nguvu niwezavyo, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kwa hiyo sasa kama unataka kukaa huku, unisikilize, kaa tu huku.’”

³ Hiyo ni imani halisi. Shuhudia kwa utukufu wa Mungu, maana, “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” Mnaona? Huioni imani. Unaamini tu, imani.

⁴ Basi juma hili, nimekuwa na kazi nyingi sana nyumbani. Wamekuwako, hakika, siku ya kwanza, nafikiri, kulikuwa na yapata thelathini walioingia, kama nilivyotaka. Kisha, mahojiano yangu yote na kadhalika yakaja. Limekuwa ni juma lenye shughuli nyingi sana.

⁵ Nami nimejifunza mambo fulani juma hili. Nilishuka... Nami ninaye rafiki hapa mjini, ambaye ni jamaa mzuri sana. Yeye ni daktari wa tiba. Tulisoma pamoja, Daktari Sam Adair, naye ni jamaa mtanashati. Na basi sijamwona kwa yapata miaka minne. Nilikuwa na yapata saa tatu ama nne za mazungumzo pamoja naye, juma hili. Tulishuka ofisini na kujifungia tu, tukaingia na kuzungumza.

⁶ Nami nilikuwa nikimsimulia mambo fulani niliyokuwa nimepata, ya kiroho, kuhusu nguvu za uovu, na jinsi zinavyoingia. Naye alikuwa akiniambia ya tiba, ama u—ubaini wake katika istilahi za tiba. Ni la kushangaza, mtaona jinsi hayo yanavyoafikiana pamoja. Uh-hum.

⁷ Kwa hiyo, alikuwa akiniambia kuhusu kamasi fulani ambalo huingia ndani ya wanadamu, ambapo haimbidi mtu kushikwa

na kitu kama mafua, ama chochote. Akasema unaninii tu. . . Ni kamasi fulani tu linaloingia mle, kisha kijidudu kinaingia katika kamasi fulani hili, ama kamasi hili linasababisha kijidudu.

⁸ Nikasema, “Vema, kama hilo kamasi husababisha hicho kijidudu, basi ningetaka kujua ni wapi uhai wa hicho kijidudu unakotoka.” Mnaona?

⁹ “Vema, hakika, hilo,” akasema, “hatujui hilo.” Kasema, “Hatujui kabisa.”

¹⁰ Unashikwa na baridi, ama kitu fulani, nacho kijidudu hicho kinaumbika katika sura mbalimbali. Halafu kinayo njia ya kujizidisha chenyewe, kinaendelea tu kuzaa viini kutoka kwenye kamasi hili, nadhani. Daktari, mtu fulani akiwa hapa, ama mwuguzi, angeelewa zaidi juu yake.

¹¹ Lakini kilichonivutia kilikuwa, na mawazo yangu, yalikuwa, hicho kijidudu, chenyewe. Ule uhai ulio ndani ya hicho, ndani ya hicho kitu kama kifuniko kama—kama kidonge kidogo, kidogo sana jicho la mwanadamu haliwezi kukiona. Lakini ndani ya kitu hicho kidogo sana ambacho ni darubini yenye nguvu sana tu ingeweza kuona, ndani ya hicho kuna uhai. Kinachoufanya uhai huo kuchukua kiasi fulani cha kamasi hilo na kujifunganisha chenyewe mle, na kufanyiza kidonge hiki, mnaona, ama kijidudu, huyo ni ibilisi. Hizo ni nguvu za kiroho. Ambapo, kamwe hawataweza. . . Wamefikia mahali hata chini ya molekuli, ambapo wangeweza kuchukua maskini seli hii ya kijidudu, na kadhalika, na huo utando mdogo sana wa kamasi ambao ungeweza tu kuonekana kwa darubini yenye nguvu. Halafu basi, bali, kupita hapo, hawawezi kuona, maana hakuna. . . hakuna. . . hakuna kitu cha asili cha kushikilia. Sasa, kabla si—si. . .

¹² Watu wamesimama. Sasa, Charlie, ninachukia kuona. . . Wewe, na Daudi, na Rodney, nanyi nyote hapo, nyinyi ni wakarimu sana kwangu ninaposhuka kuja nyumbani kwenu, na kadhalika. Siwezi kuwapa kiti katika nyumba ya Mungu, lakini, nitawaambia nitakalofanya, endapo mtakuja papa hapa, hiki hapa changu. Njoni huku, na mjisikie kukaribishwa. Yeyote wenu anayetaka kuja papa hapa na kuchukua kiti hiki, njoo tu huku juu. Unaona? Mtakaribishwa hata na zaidi.

¹³ Na ni—ni kizuri. Kweli si changu. Ni cha Bw. Wilson, mkuu wa shule. Nimekuwa nacho tangu mwaka wa 1937, kwa hiyo ndicho cha zamani sana. Kwa hiyo mimi. . .

¹⁴ Alikuwa hapa siku moja, kasema, “Hei, ungali una viti vyangu?”

Nikasema, “Ninaketi juu yake kila usiku kabla sijahubiri.”

Naye akasema, “Vema, kiko kwenye mikono mizuri basi, na kiwe hivyo basi.”

¹⁵ Sasa mmekaribishwa. Kuna kiti kimoja hapa. Halafu basi kama mkitaka kuja hapa ambapo hawa jamaa wadogo wameketi. Sasa usi—usiache hilo likutahayarishe, kufikiria kwamba wewe ni jamaa mdogo, kwa kuwa sivyo ulivyo. Lakini, ukitaka kuwa, tena. Lakini, na hivi hapa viti vingine *hapa*, vimewekwa huku. Na—na kuna kimoja *hapa*. Na kwa hiyo huenda mkaweza, sana sana baadhi ya hao kina mama pale, ambao kwa namna fulani wamesimama namna hiyo. Asante. Nasi tungefurahi kama mngalikuja moja kwa moja hapa na kuketi chini. Ingekuwa ni sawa. Weka tu mkono wako huku, uiname, tunapozungumza.

¹⁶ Na—na, Charlie, nilidhani ulikuwa ukija huku. Ni—ninamtafia, wakati wote. Nikasema, “Njoo huku, kanisani.” Ninajaribu kumfanya, aje, kuniona. Halafu basi yeye... Nikasema, “Utakapokuja kanisani, nitasema, ‘Asubuhi ya leo, Dr. Charlie Cox atakuwa na ujumbe,’ na kuondoka.”

¹⁷ Akasema, “Nitazimia.” Kwa hiyo kabla sijamwita, akaingia kwenye chumba cha nyuma. Yeye... .

¹⁸ Kwa hiyo ningetaka ku-, kabla tu hatujaanza hili somo... . Niliwazia, juma lililopita, ya kwamba Bwana kweli alitubariki. Mliupenda ule—ule...? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Jamani! Umesambaa kila mahali. Hata Ujumbe huo umefika hata California. Walikuwa wakipiga simu jana usiku, kutoka California, kuuhusu. Na—na sasa wanataka kufanya mpango wawe na jambo lilo hilo huko California, katika mwezi mwingine ujao wa Januari. Mnaona?

¹⁹ Roho Mtakatifu alionekana tu kugusa, mara moja, mumo humo Shreveport. Na anaenda tu mahali mahali, namna hiyo, na ni—ni saa moja tu ya ufunuo.

²⁰ Na kwa hiyo tuna furaha sana, na kutumainia, na kuliona kundi le—letu wenyewe hapa, hapa maskanini, likifanikiwa sana kwa jambo hili, kuona dhihirisho la Mungu miongoni mwetu hapa. Tuna furaha sana kwa ajili yake, na kuamini kwamba tuko kwenye ile saa kuu ya kuitwa kwa Kanisa, na kuliweka katika utaratibu. Kwa hiyo wao... .

²¹ Nilikuwa nikipata kitu ambacho nilininii...wakati nikizungumza na rafiki yangu mwema, Dr. Adair, tukiketi ofisini mwake. Naye akasema, alikuwa akizungumza kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu eksi-rei, ndipo kasema juu ya mafua makali na viini mbalimbali. Na kunyosha mkono na kuchukua vitabu vyake, na kunionyesha kupitia kwavyo, yale wamepata kujua. Akasema, “Nitakwambia, Billy,” kasema. “Kama vile mafua makali, mengi yao,” kasema, “hatuna hata kitu kimoja kwa ajili ya mafua makali,” akasema.

²² Nikasema, “Vema, siku zote nilifikiri ya kwamba ukipata maumivu ya koo, kama ungegogomoa kitu fulani.” Nikasema, “Sasa nikiisha kumaliza kuhubiri,” nikasema, “huenda

nyumbani usiku, nimepwelewa na sauti kidogo hivyo.” Nikasema, “Ni—ninachukua Lavorisi, na—na kuigogomoa.” Nikasema, “Tumekuwa nayo nyumbani mwetu kwa miaka na miaka, kisukutua kinywa.”

²³ Akasema, “Maji baridi yangukuwa mazuri vivyo hivyo.” Akasema, “Maana, kamwe usiwazie ya kwamba chochote ungaliweza kugogomoa kamwe kinge—kingekusaidia kwa chochote. Kwa sababu, jambo pekee kingaliweza kufanya ni kuosha tu viini vilivyo kooni mwako, kabisa. Hakiwezi kuingia ndani ya mkondo wa damu. Kama kingeingia, kingeilipua koo yako nawe ungetokwa na damu. Unaona?” Kisha kasema, “Hakiwezi kufanya hivyo.”

²⁴ Kwa hiyo ule msemo wa kale unarudi tena, “Dawa zilifanywa zipate kuuzwa, sio kunywewa,” mwajua.

²⁵ Na hata hivyo, na kuona katika vitabu vya tiba ambavyo hata ninavyo nyumbani mwangu, kusoma, nina—ninavutiwa na tiba, hakika inanivutia, chochote kitakachowasaidia watu wa Mungu, kitakachowasadia binadamu. Kama ni amani, kuyasoma masharti ya amani, ninavutiwa na hayo. Ninavutiwa na jamii bo—bora zaidi ya kuishi ndani yake. Ninavutiwa na shule bora kwa ajili ya watoto wetu kuhudhuria. Ninavutiwa na chochote kilicho kizuri, kizima na cha kweli.

²⁶ Nayo tiba imefanya mambo makubwa. Ninaamini ya kwamba Mungu ameitumia, vitu vingi. Ninaamini, kama tungekuwa waaminifu zaidi na kujiweka wakfu kwa Mungu, tayari wangukuwa na vitu kwa ajili ya kansa na kila kitu kingine. Kama tukinini tu. . . Mungu anacho hicho kitu, kama tungemwomba tu Yeye kukihusu. Mnaona? Kwa hiyo, sasa, ninaamini sababu ya kupatikana kwa chanjo ya Salk, ni kwa sababu tu ya kuteseka kwa watoto wadogo jinsi ilivyo. Naye, Shetani, kitu hicho kiovu huko nje, kinachowalemaza watoto wadogo na kadhalika. Ndipo Mungu akaachilia hiyo igunduliwe, kwa ajili ya chanjo. Nayo imefanya jambo kubwa, na ambalo tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ajili yake. Nashukuru sana ya kwamba Mungu daima ametubariki!

²⁷ Na, ndugu, wapi. . . ? Yeye harudi nyumbani, sivyo, Dada Nash? Yeye—yeye. . . [Dada Nash anasema, “La, bwana. Yeye anaenda kuleta viti.”—Mh.] Loo, hilo ni zuri. Hilo ni jema. Uhuh. Vema.

²⁸ Sasa, katika kusoma, basi, nikiisha kuja nyumbani, niliketi chini hapo chumbani na kusoma kwa muda mrefu, “Haya yote ni ya nini?” Nitawapitishia jambo dogo, ambalo ninalisoma, mpate kusoma pamoja nami. Naye Bwana, tulipokuwa chumbani, ninalichukulia kuwa ni Yeye, maana nimekuwa na matukio makuu pamoja Naye.

²⁹ Lakini hivi mlifua, ya kwamba, baada ya daktari kuniambia jambo hilo, na kunionyesha katika vitabu vilivyo bora sana

na vya karibuni sana vya tiba, ambavyo ninajua ndio kwanza vigunduliwe. Yupo daktari aliyeketi hapa, kwa vyovyote vile, akinisikiliza. Sasa hili, vitu vya karibuni sana na vilivyo bora sana kwa ajili ya mafua makali, wao hawana dawa. Wanakemea kunywa asprini, na kadhalika; ambazo hupunguza tu maumivu, na kadhalika, ya mafua ama maumivu, bali hazisaidii mafua hata kidogo. Ila inasaidia kukutuliza. Basi jambo lililo zuri sana kwa mafua makali, ni kulala chini na kupata usingizi, usijisumbue. Lala tu kitandani, karibu ndilo jambo lifaalo zaidi unaloweza kufanya.

³⁰ Sasa, basi, nikaanza kusoma. Nikasema. “Daktari Sam, basi, hili ndilo hili. . . Mafua makali, jambo zuri kabisa ni kupumzika.”

Akasema, “Ndilo jambo zuri kuliko yote kwa chochote kile.”

³¹ “Vema,” nikasema, “asante, daktari, hilo ni zuri mno.” Ndipo tukazungumza muda kidogo zaidi, na kisha nikaenda nyumbani. Nami nikamwambia. . . Yeye anapenda sungura na kuchakulo, na kadhalika, hapati nafasi ya kutoka nje. Tulikuwa tukiwinda sana, pamoja, tulipokuwa wavulana, na kuwinda na kuvua samaki, ama kuvua samaki, hasa.

³² Kwa hiyo basi nilipoenda nyumbani, nilianza kuwazia. “Nini?” Mwajua, niliona. Mwangalie mnyama. Hebu mchukue mbwa, anapokuwa mgonjwa, ataenda anywe maji, kisha alale chini mahali fulani, anaenda kulala chini. Vema, ndipo wazo likanijia, kesho yake asubuhi. Nilikuwa nimelala kitandani, nikiwangojea jamaa hao. Wanaamka yapata saa kumi na mbili na nusu. Na kwa hiyo mimi huamka yapata saa kumi na nusu, ama saa kumi na moja. Nilikuwa nimelala pale. Nikiwazia, mara nyingi, Mungu hufunua mambo.

³³ Unajua, mimi sifundishi hili. Lakini hivi ulijua. . . Mwanadamu, hapo mwanzo, wakati Mungu alipomwumba, Yeye hakumwumba apate kutibiwa. Alikuwa na matibabu yake mwenyewe ndani yake. Alikuwa ameandali- . . . Alikuwa—alikuwa ni—mwenyewe alikuwa ni mfumo wa kivyake. Mnaona? Basi, uponyaji hauji kutokana na nguvu zozote za nje. Hauna budi kutoka ndani. Sasa tunaweza kuchukua usaidizi wa nje, kama vile kuua viini, ama chochote kilicho ndani yetu. Ama, tunaweza kuichukua mikono yetu na kukatana mmoja kwa mwingine, na kutoa ki—kipande kimoja, ama kitu fulani, kama kidole tumbo, ama jino baya ama kitu fulani, na kukitoa nje. Lakini uponyaji hauji kutoka kwa kitu chochote unachotumia. Uponyaji huja tu kwa ngu—nguvu zilizoko ndani yako, kujenga tena ti—tishu ambazo zimeraruliwa kutoka mahali ambapo imetolewa. Na, kwa hiyo, uponyaji uko ndani yako.

Sasa sikilizeni kwa makini, na mfikirie sana sasa kabla hamjatoa mawazo yenu juu ya hili.

³⁴ Mwanadamu, hapo mwanzo, wakati alipoubwa, mwanadamu ni mungu. Yeye kabisa ni mungu. Kwa kuwa aliumbwa katika sura ya Mungu, akiwa ni mwana wa Mungu, halafu yeye ni mrithi wa yote aliyo Mungu. Naye mwanadamu alipewa milki, nayo hiyo milki ilikuwa ni dunia. “Una mamlaka juu ya samaki, juu ya ndege wa angani, na juu ya kila kitu.” Angeweza tu kunena, na kila kitu kilimtii, kwa sababu yeye mwenyewe alikuwa ni mu—mungu; sio Mungu wa ulimwengu mzima, bali ninamaanisha . . . Mungu wa mbingu na nchi. Lakini alikuwa m—mtawala katika milki yake. Yeye alikuwa ni mfalme, mfalme—mtawala. Huyo alikuwa ni mwanadamu. Na hata sasa, katika hali yake ya kuanguka sasa, angali ana sura hiyo.

³⁵ Sasa, sio muda mrefu uliopita, walikuwa wakijaribu kuchanganya mbegu, na kadhalika, na kusema ya kwamba, “Mwanadamu alitokana na wanyama wa hadhi ya chini, na—na kupitia kwa mageuzi yanayoendelea akajipandisha juu.” Vema, mnaona, wameendelea kujipumbaza kwa sayansi hata wanatofautiana na nadharia yao wenyewe.

³⁶ Huwezi kuzalisha chochote kwa kuchanganya mbegu na kukifanya kipande juu zaidi. Kitashuka moja kwa moja. Hakiwezi. Mahindi chotara, ama chochote kile, hakiwezi kujizaa tena. Ama kama nilivyokuwa nikisema hivi majuzi, pu—pu—pu—punda na farasi jike wanaweza kuzalishana, itazaaa nyumbu, bali nyumbu huyo hawezi kumzaa nyumbu mwingine. Hana budi kurudi moja kwa moja, kuanza. Kwa sababu, Mungu alisema, “Kila mbegu izee kwa jinsi yake.”

³⁷ Sasa, wakati tulipoubwa—wakati tulipoubwa . . . Nao ndio kwanza wagundue, hivi majuzi, ya kwamba mwili wako umejaa nuru. Eksi-rei inathibitisha hilo. Eksi-rei haina nuru yake yenyewe. Hutumia nuru yako. Unazaliwa ukiwa na miale minne. Baada ya kitambo kidogo, tuseme ishirini, ishirini na mitano, mwale mmoja unatoweka; na thelathini na mitano, mwingine, ama arobaini, mwingine unatoweka; ndipo hatimaye, unapopita yapata umri wa miaka sitini na mitano, unaishi kwa mwale wako wa mwisho. Basi kila unapopigwa picha ya eksi-rei, unairarua hiyo miale. Hiyo ndiyo sababu hunayo tena, mnaichomelea miguu ya watoto hawa katika mitambo hiyo, kwa sababu ilikuwa ikiirarua tu hiyo miale moja kwa moja katika miili yao midogo. Na hiyo ni nurulimwengu iliyo ndani yako, ambayo umefanyizwa kwayo, iliyojaa seli za nuru. Sasa, hiyo ni nurulimwengu.

³⁸ Lakini Mungu ni Nuru tofauti, lakini hata hivyo Yeye ni Nuru. Sasa, ninafikiri ya kwamba hiyo picha hapo ni thibitisho kuu la yale ninayotaka kusema, kwamba Mungu ni Nuru. Ndipo wakati tulipokuwa tukitembea katika Nuru ya Mungu, kama wana wa Mungu; Mungu si nurulimwengu, bali Nuru ya Mungu ilifanya kazi kupitia kwa nurulimwengu ya miili yetu, seli zetu. Nasi tukafanyika . . . Sisi tulikuwa kabisa, wakati mmoja, wana

halisi, wa kweli wa Mungu. Lakini basi wakati kule kuanguka kulipokuja, halafu basi ambapo. . .

³⁹ Tunda la Roho siku hizi ni upendo, furaha, imani, uvumilivu, upole, unyenyekevu, saburi, yote ya kimbinguni. Ilifikia tu mahali ambapo mwili wote, polepole tu kabisa. . .

⁴⁰ Kama vile magugu ya baharini, ukiingia chini ya bahari. Mara nyingi, wapiga mbizi, nao wataingia chini ya magugu haya ya baharini. Na kabla hawajajua, wamefungwa hivi kwamba hawawezi kujitoa humo.

⁴¹ Vema, hivyo ndivyo dhambi imemfanya mwanadamu. Hivyo ndivyo baridi imelifanya kanisa. Hivyo ndivyo wakomunisti wamelifanya taifa. Ni danganyifu sana. Ndipo basi katika mwili wa mwanadamu, yametufunga, yanaisukuma nje Nuru hii ya Mungu; kwa madhehebu, na kuikana Imani, na kadhalika, yameisukuma nje miale yote ya Nguvu kuu za imani ya Mungu, mnaona, zilizo ndani yetu, zinazopaswa kuwamo. Yamesukuma na kutoa miale hiyo yote, kufikia mahali ambapo, mpaka tukafikia kwenye chama. Na—na ndipo sasa chini ya chama, kanisa liko hivyo, maana limesukuma tu, giza lote, nje, na hata kusema tu, “Hazitendeki.” Wakikana kwamba ingeweza kutendeka, mnaona, miujiza ya Mungu.

⁴² Na hata hivyo, mwanadamu, mahali fulani chini ndani yake, mahali fulani ndani yake, kama tu angeweza kuachilia hiyo ninii ndogo. . . Kama nilivyolielezea, kama kitufe. Mwanadamu anapookoka, kiasi hicho chake ni Mungu. Hiyo ndiyo ile Nuru ndogo inayoingia, kumfanya aache kufanya makosa. Sasa, kama unaweza kuondoa kijicho chote na wivu, na ugomvi na kutokuamini, nje, kitu hicho kidogo kama kitufe cha hiyo Nuru na Nguvu za Mungu kitaendelea kukua, zaidi, zaidi, zaidi, kikikuondosha kutokuamini. Wala hufanyi hivyo kwa ushawishi wa—wa mazoezi ya mwili. Unafanya hivyo kwa Maisha yaliyotakaswa, yaliyowekwa wakfu ambapo Roho Mtakatifu hufanya kazi kupitia kwako. Nilipata baadhi Yake mahali, ambapo, si muda mrefu uliopita.

⁴³ Ni wangapi wanaokumbuka wakati Elij' Perry alipofufuliwa katika wafu asubuhi ile, baadhi yenu huku? Mmeona kwenye gazeti hapa, mara nyingi. Ninamwona Dada Wilson, hao, wakiinua mkono wao. Nilikuwa nimesimama pale wakati mtu huyo alipokufa. Yeye anaishi papa hapa sasa, huja kanisani mara moja moja, akishuhudia basi.

⁴⁴ Alikuwa amekufa, saa kadhaa. Alikufa kwa kutokwa na damu ya mapafu, naye alikuwa amelowa damu kila mahali. Basi nikaondoka. Nilikuwa tu ni mhubiri kijana, siku hizo. Naye Dada Jackson alikuwa mshiriki wa kanisa hapa. Na—na mke wa mhuribi wa Kimethodisti, ninasahau jina la mtu huyo lilikuwa ni nani. Shafiner, Ndugu Shafiner na Dada Shafiner. Walikuwa na uhusiano fulani na Wisehearts. Nao pamoja naye walikuwa

wamesimama hapo kando ya kitanda. Nami nikaanza kuondoka. Naye alikuwa amelowa damu awezavyo kuwa, ambapo alikuwa amekufa. Nayo macho yake yalikuwa yamerudi nyuma, na koo yake ilikuwa imebenuka. Wakavuta shuka juu ya kichwa chake. Naye mke wake alikuwa huko nje, wanalia, na kujaribu kupata anwani, apate kuwaita wapendwa.

⁴⁵ Basi nikaanza kuondoka kitandani, ndipo nikahisi mtu Fulani akiweka mkono Wao juu yangu. Nilifikiri ilikuwa ni Dada Shafiner. Basi nilipogeuka, hapakuwapo na mtu yeyote karibu nami. Ndipo nikaanza . . . Ukaniacha, wakati nilipogeuka.

⁴⁶ Naye Ndugu Elij' alikuwa amelala pale, amekufa. Tulikuwa ni marafiki wazuri sana, tulivua samaki mtoni, mwajua, jinsi tulivyofanya mengi sana pamoja. Ndipo akajeruhiwa hapa nje, njia ya reli, akiendesha chombo kama buibui. Vema, kiliyaponda mapafu yake ndani. Alikuwa akitokwa na damu. Alitokwa na damu kisha akaambukizwa TB kutoka kwake, akafa.

⁴⁷ Nikaanza kuondoka *hivi*, ndipo nikauhisi Mkono huo tena. Nikageuka, Huo usingeniacha.

⁴⁸ Na kabla ya kujua nililokuwa nikifanya, nilikuwa nimelala juu ya mtu huyo, midomo yangu ikiwa juu ya midomo yake. Nilikuwa nimelowa damu kama alivyokuwa, huku nimelala pale juu ya mtu huyo, nikimlilia Mungu. Ndipo nikahisi kitu fulani kikipanda, kando ya sikio langu. Ilikuwa ni mkono wake.

⁴⁹ Mmemsikia akisimama papa hapa na kushuhudia juu yake. Mnaona? Jinsi yeye. . . Ndipo akafufuka. Na hiyo imekuwa yapata miaka ishirini na mitano iliyopita, ama labda thelathini. Yu hai, leo hii, papa hapa kwenye kizingo. Naye alikuja hapa si muda mrefu uliopita, alikuwa akilishuhudia kanisani.

⁵⁰ Sasa, hapo ndipo Canada ilipopiga simu na ilitaka kujua, wakati mmoja. Nilikuwa nimeshuhudia juu yake huko Canada wakati nilipoanza mikutano yangu mara ya kwanza. Walimpigia simu Bw. Coots, mtayarisha mazishi, na kuuliza kama kulikuwako na mtu aliyefufuka kutoka chumbani, aliyekuwa amekufa. Ningali nina makala niliyokata, bado.

Wao walisema, “Tumesikia juu ya miujiza mingi ikifanywa,” Bw. Coots akasema. Kasema, “Bw. Branham ni rafiki yangu binafsi, na kila namna ya mambo yametukia. Ila hatuna kumbukumbu ya mtu yeyote aliyefufuka katika wafu, hasa sana katika chumba hiki cha kuzikia.”

⁵¹ Wakanada walikuwa wamelielewa vibaya. Basi kesho yake. . . Jamani, gazeti lilikuwa limeyaandika. Akasema, “Mamia ya watu walipiga simu kutoka kila mahali.” Naye Ndugu Perry mle ndani, yeye mwenyewe, akishuhudia juu ya kufufuliwa kwa mwili wake kule, na kupinga ki—kile kitu alichokuwa amekiweka kwenye gazeti. Na kwa hiyo basi ilieleweka haikuwa ni kule. Lilitukia nyumbani kwake,

na kwa hiyo ndiko alikuwa amelala, amekufa. Hawakuwa wamempeleka kwenye chumba cha mazishi, bado.

⁵² Ndipo nikasoma hivi majuzi usiku, ambapo Ireneo, ninaamini alikuwa ndiye, ama Mtakatifu Martin, ambaye aliulaza mwili wake juu ya rafiki yake, akiisha kunyongwa. Sasa hiyo ni historia. Naye akamlalia kwa saa moja, ndipo huyo mtu akafufuka.

⁵³ Nami ninaona katika Biblia ambapo Eliya aliulaza mwili wake juu ya mwili wa mtoto aliyekufa naye akafufuka.

⁵⁴ Ninawazia juu ya maskini yule mvulana mdogo huko Finland, wakati alipokuwa amelala kule, amekufa, amelala kando ya barabara.

⁵⁵ Halafu, pia, yapata miezi miwili iliyopita, naamini ilikuwa hivyo, Gene, katika Newsweek; ambapo waliachilia, wale wanaowaita, “waponyaji wa Kiungu” ovyoovyo huko London. Na kuwaachilia waende, wakiwaombea wagonjwa. Na kulikuwako na yapata uponyaji asilimia themanini zaidi kuliko kwa dawa. Maombi hayo kwa ajili ya wagonjwa.

⁵⁶ *Reader's Digest* ikayaandika. Na hapa Marekani, wao, tumeyaandika hapa, na katika *Reader's Digest*, ambapo walikuwa wameuchunguza uponyaji wa Kiungu. Basi wakamchukua ndugu aliyekuwa akiwaombea wagonjwa, nao walikuwa na mgonjwa, nao wakamfanya amwombe huyo mgonjwa. Kisha wakaweka kipande cha jaribosi ya risasi. Mtu yeyote anajua, jaribosi ya risasi huiakisi nuru hiyo. Juu, kati ya huyo mtu, na yule mtu aliyekuwa akiomba, yule ndugu, mkono wake. Kisha wakaiweka chini namna *hii*, na kupiga picha ya eki-rei. Basi kutoka kwenye mkono wa huyo mtu, ilionyesha uakisizi unaoonekana wa mwale ukitoka mkononi mwake, ukimwendea huyo mtu mwingine.

⁵⁷ Mungu anajua alichomaanisha wakati Yeye aliposema, “Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.”

⁵⁸ Kuweka mikono, ya mtu huyu, juu ya mgonjwa, nayo eki-rei ya kimitambo (Ee Mungu!) ikionyesha Nuru ikija kutoka mkononi mwa huyo mtu. Watu wanawezaje kuwa wajinga hivyo, kusema hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu? Mbona, hata vyombo vya kimitambo, zile mashine ambazo—ambazo sayansi imeunda, ni—ni . . . (nini?) ni shutuma kwa mawazo yao wenyewe, ya makanisa haya yanayosema, “Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu na Nguvu za Mungu.”

⁵⁹ Vipi kuhusu yule mtu huko Chicago? Kuendelea tu zaidi na zaidi, nikisimulia, jinsi alivyoniweka mbele ya ile mita pale, nacho kitu hicho, jinsi ambavyo mkono huo ungeonyesha kama kigundua uongo, Chake. Mnaona?

⁶⁰ Naye mwanamke huyo amelala, akifa, wakaweka kipimo juu yake. Hicho hata kikauzungusha mkono huo, pamoja na Nguvu

za kutosha kutupa ujumbe wa redio kote ulimwenguni, mara arobaini, na kuuharibu huo mtambo. Mtakatifu huyo, akifa, akifanya maungamo yake. Wakakiweka juu ya mtu mwovu, naye yuafa; nao walipofanya hivyo, kiliutupa mkono, vinginevyo, upande huu mwingine, vya kutosha kuuharibu mtambo huo. Kafiri hu—huyo, kasema, “Endapo kuna Mungu, Naye ni wema wa moyo mwema, kwa sifa Zake, angeitumia mashine hiyo Nguvu za kutosha kuitupa huku na huku, kuna kitu Fulani katika mwanamke huyo, kinachozifanyiza Nguvu hizo. Na kama zikiwa juu ya mtu mwovu, zingeitupa upande huo mwingine,” kasema, “Mungu, unirehemu mimi, mwenye dhambi,” naye akautoa moyo wake kwa Kristo. Hiyo ni kweli. Mbona, sayansi inajua.

⁶¹ Basi siku moja utajua, Mungu yuko ndani yako. Unaona? Mungu, Mwenyewe, ndani ya mwanadamu. Mungu ndani yetu! Loo, jinsi ninavyomshukuru Mungu kwa ajili ya mambo hayo, ya ajabu sana!

⁶² Sasa, kabla ya kulikaribia Neno Lake, basi sasa hebu tuuchukue tu wakati wetu, kwa sababu asubuhi ya leo tutawaombea wagonjwa. Nami ni—ni—nililitangaza.

⁶³ Na sasa mtu fulani alikuwa akiuliza kama tutakuwa hapa Jumapili ijayo. Vema, jinsi . . . Sijui bado. Wao . . . Si—sijui kabisa isipokuwa Bwana alifunue. Iwapo Bwana ataliruhusu, labda Jumapili ijayo usiku. Ninachukua mahubiri haya yote ya asubuhi kutoka kwa ndugu yangu wa thamani hapa. [Ndugu Neville anasema, “Amina. Vema, ndugu.”—Mh.] Jumapili ijayo usiku, labda, kama nikiwa huku, Bwana akipenda, ambalo, kwa kawaida huwa niko, isipokuwa kama nina wito wa nje, ninataka kuzungumza juu ya: *Tumeiona Nyota Yake Mashariki Nasi Tumekuja Kumsujudia*. Mnaona, ujumbe tu, ujumbe wa Krismasi.

⁶⁴ Na sasa kabla hatujamkaribia Yeye, au Neno Lake, hebu tumwendee kwa maombi. Kama . . . Wote wanaoweza kusimama, hebu tusimame kwa muda mfupi.

⁶⁵ Baba yetu wa Mbinguni, sisi ndio watu walio na furaha kuliko wote, hata tunafurahi sana mpaka nafsi ze—zetu za kibinadamu haziwezi kulidhibiti. Inatubidi tu kupaza sauti, wakati mwingine, na kuiachilia furaha iliyo mioyoni mwetu, kupitia kwa Yesu Kristo; kujua ya kwamba katika saa tunayoishi sasa, ambapo kila kitu ki—kiko katika machafuko kilichomo, hata hivyo kuna Msingi ulio hakika.

⁶⁶ Na kuona watu wenye akili ambao wameinuka, katika siku zilizopita, nao wamejaribu hata kukanusha kwamba Mungu yupo, kupitia vyombo vyao wenyewe vya kimitambo, wamerudi moja kwa moja na kushuhudia juu ya utukufu wa Mungu. Hakika, ilimbidi Yuda kusema, yeye mwenyewe, ya kwamba alikuwa “ameisaliti Damu isiyu na hatia.” Yule akida wa

Kirumi alisema, “Hakika huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu.” Adui Zake Mwenyewe iliwabidi kushuhudia. Nasi tumeishi kuuona wakati wa kisayansi ukifikia mwisho wake. Hawawezi kwenda mbele zaidi. Wanaenda tu, dakika yoyote, kulipuana vipande-vipande. Na hata hivyo tunaona ya kwamba mitambo ile ile ya kisayansi waliovumbua, kujaribu kukukosoa Wewe, inageuka moja kwa moja na kuushuhudia utukufu Wako. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya hilo, Bwana! Tujalie, leo hii, kukumbuka ya kwamba Neno la Mungu halitashindwa kamwe.

⁶⁷ Tupe imani, Bwana. Kama lile tamshi dogo, fidhuli muda mfupi uliopita, nililotoa, kuhusu Nguvu za Mungu kuwa ndani yetu, na mishipa yetu yote kuwa Nuru ya Mungu, na giza na dhambi zimeviziba maskini vinyweleo ndani yetu, vya nafsi yetu. Mjalie Roho Mtakatifu, asubuhi ya leo, atandae katika utu wetu, akiingiza imani ndani ya utu wetu wa ndani kabisa, kusudi miili yetu yote na maisha yatajazwa kabisa na Nguvu za Mungu, hata watu wataona ya kwamba Yesu Kristo anaishi Kanisani Mwake. Lijalie, Baba.

⁶⁸ Tunalikabidhi lote Kwako sasa, na kuomba kwamba utayabariki maneno haya machache tunayoenda kusema sasa, kujaribu kutoa mawazo juu ya yale yaliyoandikwa tayari na mmoja wa mitume Wako, Mtakatifu Paulo aliye mashuhuri. Nami ninaomba, Baba, ya kwamba Roho Mtakatifu atalichukua Hili na kulifanya tu likue kupitia mioyo ya watu, na kutupa imani kwa ajili ya ibada ijayo ya uponyaji. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁶⁹ [Dada fulani anaanza kunena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu fulani anaanza kunena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mmoja anatoa tafsiri—Mh.] Bwana ashukuriwe. Amina. Mungu asifiwe. [Sehemu tupu kwenye kanda.]

⁷⁰ Mungu, tunakushukuru Wewe kwa wema Wako na rehema. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya dhihirisho Lako la upendo na Nguvu, kwa yote ambayo umetufanyia. Hatuzistahili baraka unazotupatia. Mimi kweli. . . Kwa sauti ya ujumbe, hapana shaka ulikuwa ni ujumbe ule ule uliotolewa, na inaonekana ulikuwa ukiwaita wenye dhambi, ku—kukutafuta Wewe, kwa kuwa saa ya maangamizi imekaribia. Na Baba Mungu, tunaomba ya kwamba kama kunaye mtu huyo hapa asubuhi ya leo, ama watu hao, ambao wangepahamu ya kwamba hatujui kitu juu ya mambo haya, ya kwamba kweli, ni Roho Mtakatifu akizungumza kupitia kwa midomo ya binadamu, kutoa tafsiri, kuwaita watu waliokusudiwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuwa wana na binti za Mungu, na labda wameliepuka hili kwa muda mrefu. Jalia waje leo hii, Bwana, kukujua Wewe, na kupata mahali hapo pa kujificha, kwa kuwa

saa imekaribia. Lijalie, Baba, tunapokungojea Wewe zaidi, kwenye Ujumbe. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁷¹ Sasa, kama kungekuwako na mtu fulani ambaye huenda asielewe kabisa jinsi ambavyo jumbe hutolewa namna hiyo, mbili za hizo, huenda ilikuwa ya kwamba mmoja alikosa kusema jambo fulani ambalo huyo mwingine alilichukua. Kwa kuwa, mliona jinsi huo mwingine ulivyo mdogo, huo mwingine ulivyokuwa mdogo, machache tu ambayo labda huyo mwingine aliacha. Ndipo wakati tafsiri ilipokuja, yote ilikuja kwenye mstari ule ule, mnaona, uliouleta huo ujumbe, wito kwa wenye dhambi.

⁷² I—ilitokea tu kwamba, watu hawa hawajui kile nilichokuwa nikitaka kuzungumzia. Hakuna mtu anayejua hilo, hakuna mtu ulimwenguni anayelijua mpaka sasa, lakini hilo ndilo jambo lenyewe ninalozungumzia. Mnaona? Naam. Sasa fungueni pamoja nami kwenye Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 14. Ni vema ku—ku—kuondoa tu kutokuamini kwote ndani yako, kusudi Roho Mtakatifu aweze kuingia na kuchukua tu njia Yake, mwajua, na kupitia moja kwa moja kwenye mishipa yenu, na—na kuyaongoza, na—na kuyaongoza maisha yenu.

⁷³ Sasa, ninyi ambao mnayaandika Maandiko, niliona, hivi majuzi, namna hiyo ya kuendelea kufundisha, ilisaidia sana, hata nina kurasa tatu ama nne hapa juu ya yale nitakayozungumzia, asubuhi ya leo, ya Maandiko na kadhalika, mpate kuyaandika na kutia alama sehemu hizo. Nami nimeyaandika hapa chini nisije nikayasahau.

⁷⁴ Sasa katika mlango wa 14 wa Wakorintho wa Kwanza, kifungu cha 1 hadi cha 8. Sikiliza kwa makini sasa.

Ufuateni upendo, na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu.

Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu bali husema na Mungu: maana hakuna aelewaye; lakini, roho yake, anena mambo ya siri katika roho yake.

Bali yeye ahutubuye asema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji, na kuwatia moyo.

Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake; bali ahutubuye hulijenga kanisa.

Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha, . . . lakini zaidi sana mpate kuhutubu: maana yeye ahutubuye ni mkuu kuliko yeye asemaye kwa lugha isiyojulikana, isipokuwa afasiri, ili kusudi kanisa lipate kujengwa.

Na sasa, ndugu, nikija kwenu na kunena kwa lugha, nitawafaidia nini isipokuwa . . . nasema nanyi kwa njia ya ufunuo, au kwa njia ya elimu, au kwa njia ya hotuba, au kwa njia ya fundisho?

Hata vitu visivyo hai vitoapo sauti, ikiwa ni filimbi, ikiwa ni kinubi, visipotoa sauti iliyo na tofauti, itatambulikanaje ni wimbo gani unaopigwa kwa filimbi au kwa kinubi?

Kwa sababu baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa vita?

⁷⁵ Sasa ninataka, mkienda nyumbani, mwendelee tu kusoma mlango huo wote hapo, kwa sababu kuna vifungu vingi Vyake, vifungu arobaini vya mlango huu. Nami ninawatakeni mu—muusome mtakapofika nyumbani. Unazielezea karama.

⁷⁶ Sasa kama ningeliita fungu asubuhi ya leo, juu ya ninii yangu. . . yale ninayotaka kusema, ni: *Sauti Isiyojulikana*.

⁷⁷ Sasa, Paulo hapa alikuwa akinena, juu ya—juu ya kunena kwa lugha. Kama hakuna mfasiri, ni nani angejua yale hao watu waliyosema muda mfupi uliopita? Wasingejua. Bali yeye ananena tu na Mungu. Hakika roho yake inatoa—inatoa Neno, na ni adhimu, linambariki tu. Yeye alisema, “Yeye anajijenga mwenyewe,” kwa kuwa ana faraja kwamba Mungu ananena kupitia kwake. Lakini akitokea mfasiri, pamoja na hilo, mnaona, mfasiri akitokea nyuma ya hilo; basi halimjengi tu yeye, linajenga kanisa zima, linampa kila mtu Ne—Neno la Bwana, kupitia hilo.

⁷⁸ Sasa, wao walisema, “Akiwepo nabii, basi, nabii akinena ili kwamba kanisa zima,” ambalo ni. . . Nabii, ni kitu gani? Mfunuzi wa Kiungu wa Neno la Kiungu, ambaye ana ufunuo wa Neno, kuwapa watu. Basi hilo linamjenga kila mtu. Mnaona?

⁷⁹ Sasa, mtu anayenena kwa lugha, angeweza kunena kwa lugha. Na imekatanzwa, pia, kwa mtu yeyote kunena kwa lugha kanisani, isipokuwa pawe na mfasiri hapo. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu tuseruhusiwa hapa kunena kwa lugha, kwa sababu tuna wafasiri watatu ama wanne mumu humu kanisani sasa, sasa hivi, papa hapa kwenye kanisa hili, wafasiri wa lugha isiyojulikana. Na kwa hiyo, kama kusingekuwako na mfasiri, basi tusingewaruhusu kunena kanisani. Hata hivyo, huko nyumbani na wakati wanapoomba, kwa sababu wanajijenga wenyewe, kwa sababu Roho yuko juu yao, hata wanajaribu. . . Hao watu kweli wanawazia ya kwamba wanasema mnayoweza kuelewa, bali hawajui wasemayo. Wao, kama tu vile kusimama na kuanza kusema jambo fulani, kamwe hawawezi kulikomesha. Linaendelea tu—linaendelea tu kutiririka. Nao wanafikiri wananena mnayoweza kuelewa. Ni—ni hali ya dhamira ya ndani.

⁸⁰ Ni kama tu wakati ukiwa jukwaani, kama vile leo, utaona wakati upambanuzi unapokuja. Wapo watu wengi hapa ndani, sijawahi kuwaona maishani mwangu. Angalieni Roho Mtakatifu wakati anaposhuka chini, ataanza kupitia kwenye wasikilizaji na kuwaambia hao watu kwamba wao ni nani, ama mahali wanakotoka, yale yaliyotukia, na ugonjwa walio nao, yote hayo.

Mnaona? Ni kitu gani? “Ni Neno la Mungu, kali kuliko upanga ukatao kuwili, likichoma hata kwenye mafuta ya mfupa, na hata huyatambua mawazo na makusudi ya moyo na nia.” Mnaona? Mnaona? Ni Neno la Mungu.

⁸¹ Sasa, Paulo alisema, “Kama ninyi nyote mkinena kwa lugha, bila mfasiri, mjinga akiingia, atasema, ‘Wana kichaa, wazimu.’” Neno *wazimu* linamaanisha “kichaa.” “Na sasa aseme, ‘Ni wendawazimu.’ Lakini kukiweko na mmoja anayeweza kutabiri na kuzifunua siri za mioyo, basi kila mtu ataanguka chini, aseme, ‘Mungu yuko miongoni mwao.’”

⁸² Sasa, “Kama kuna mfasiri.” Ufasiri, kwa lugha isiyojulikana, ni unabii. Mnaona, ni unabii, wenyewe, maana Roho Mtakatifu anazungumza Naye anatoa tafsiri. Anawaambia watu fulani, mambo fulani ya kufanya, na—na kila kitu. Na kila mmoja anajua wakati anapokugusa, unajua ni nani Yeye anazungumza naye.

⁸³ Na kwa hiyo ni—ni vema kuona ya kwamba sio tu... Si wanadamu, ni Mungu katika wanadamu ambaye—ambaye anafanya kazi Yake. Sana, hakika tunamshukuru Mungu kwa ajili yake.

⁸⁴ Nami nimeanza kuona ya kwamba zinaanza kuja mahali pengine, makanisa. Charles Fuller. Ni wangapi waliopata kusikia Ile Saa ya Uamsho wa Mtindo wa Kale? Mtu mashuhuri, yeye alisema, sio muda mrefu uliopita, alisema, “Tuna kule kunena kwa lugha, ufasiri, papa hapa.” Moja kwa moja kule Long Beach. Na hiyo ni kweli. Nimehubiri moja kwa moja huko pamoja naye, mara nyingi. Kwa hiyo wanao ufasiri, na humfanya kila mtu anyamaze.

⁸⁵ Mnaona, jambo ni kwamba, hatuziheshimu karama hizo. Halafu wakati mwingine kama karama ikikiuka utaratibu, basi inwabidi kuisahihisha. Sio—sio... Mnaona, ni—ni Shetani akijaribu kuwapotosha. Asipoweza kuwazuia msipate ukweli, yeye atauchukua ukweli uo huo na kuwapotosha nao. Mnaona? Hiyo ni kweli. Atafanya ulokole kutoka kwake. Mnaona?

⁸⁶ Sasa, tunajaribu kuzinyosha, hapa. Zi—zimeanza kupanda juu kanisani mwetu, tena, kwa mara ya kwanza kwa miaka kadhaa. Kwa hiyo tunalinyosha, wapate kujua hilo. Wakati, sasa, mara nyingi, kama vile sasa hivi, huenda kukawa na mtu fulani anayejisikia tu kunena kwa lugha, mnaona, sasa hivi, bali wanapaswa kutulia. Mnaona? Mimi... Ninalo Neno sasa. Mnaona? Mnaona? Mnaona? Ndipo baada ya haya yote kwisha, na wito wa madhabahuni ama chochote kile, haya yakiisha hapa, basi ujumbe unaweza kutolewa, mnaona. Mnenaji anaweza kunena kwa lugha, ama kabla ya wakati huu.

⁸⁷ Sasa kama ikiendelea kuongezeka, na karama zikiingia, basi tutakuwa na wakati maalum wapate kukutana. Nao watakutanika pamoja, saa kadhaa kabla kanisa halijapata

kuanza, na kuketi pamoja, na kutabiri, na kunena kwa lugha. Na kuandika jumbe hizo, na kuziweka papa hapa jukwaani.

⁸⁸ Wakati mchungaji anaposhuka, atatokea moja kwa moja, na kusema, “BWANA ASEMA HIVI. Itakuwa, kesho kutwa, ya kwamba Ndugu Jones, anayeishi huku karibu na njia ya reli, aondoke, kwa sababu kutakuwa na behewa litaanguka kwenye reli na kuiponda-ponda nyumba yake. BWANA ASEMA HIVI. Kutakuwa na mwanamke humu ndani asubuhi ya leo, jina lake *Fulani-wa-fulani*. Anatoka mahali fulani-fulani. Naye aliiba kitu fulani alipokuwa msichana. Ndugu Branham ama Ndugu Neville, yeyote yule, atamwekea mikonu, baada ya kukiri makosa yake na ataliweka sawa, ataponywa. Jina lake ni *Fulani-wa-fulani*.” Mnaona? Naye mchungaji, kabla halijatendeka, ibada, atasoma mambo haya. Hiyo ni kweli. Mnaona?

⁸⁹ Sasa liko kwenye uchanga wake, miongoni mwetu sasa. Mnaona? Liko kwenye uchanga. Ndipo, mnaona, hakuna kitu kinachoweza kuingia kisiri. Mnaona? Mnaona? Ibilisi anaingia na kulianzisha tu katika mwili, basi, yeye hufanya hivyo, atalirarua kanisa lote vipande-vipande namna hiyo, mnaona, liingie tu katika ulokole, na machafuko wakati wowote, mnaona. Lakini Kanisa liko katika utaratibu. Mnaona?

⁹⁰ Na sasa—na sasa kama—kama mtu aliye na karama, kisha asahihishwe na Maandiko, na—nao washikwe na hamaki juu yake, inaonyesha haikuwa karama ya Mungu. Kwa sababu, karama yoyote ya Mungu, italiheshimu Neno. Huh? Uh-huh.

⁹¹ Hiyo ndiyo sababu uponyaji wa Kiungu uko jinsi ulivyo. Mnaona? Ni Roho Mtakatifu akiliheshimu Neno, Roho Mtakatifu, ubatizo katika Jina la Yesu Kristo. Roho Mtakatifu ndani yako ataliheshimu Neno hili, kwa maana Yeye aliliandika, Mwenyewe, mnaona, Naye yuko ndani yako. Hiyo ni ile Nuru ya Mungu iliyoko ndani yako, ambayo italiheshimu Neno haidhuru limeandikwa wapi Hapa. Roho wa manabii (ni wenye kutabiri, karama) hutii nabii, mnaona, ambaye ndiye mfunuzi wa Kiungu wa Neno. Sasa, na hivi hatuna furaha kuyaona mambo haya katika siku zetu?

Sasa, hii ni siku ya kutokuwa na hakika.

⁹² Lilisema hapa, “Baragumu ikitoa sauti isiyotambulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa ajili ya vita?” Paulo akinena hapa, hakika, alikuwa akizungumza na hawa Wakorintho. Nao wengi wao walikuwa askari, katika siku hizo, katika jeshi lao wenyewe. “Sasa, sasa parapanda ikitoa sauti isiyotambulikana, ni nani atakayejifanya tayari?” Huna budi kuwa na uhakika wa chochote. Inatupasa kujua kama ni kweli ama si kweli.

⁹³ Na sasa tunaishi katika siku ya mashaka mengi. Sote tunajua hilo; siku ya kutokuwa na hakika, na wakati wa kutokuwa na hakika. Siamini kuliwahi kuwa na wakati. . . Tangu wakati ulipoanza huko nyuma katika bustani ya Edeni, wakati dhambi

ilipoingia na kuuvunja Umilele katika wakati, siamini kamwe kumewahi kuwa na kipindi cha wakati kilicho na mashaka sana kama ilivyo leo hii. Kwa sababu, hakuna hata tumaini moja lililosalia katika ulimwengu wa kawaida leo hii.

⁹⁴ Sasa, mnasema, “Vema, nimeona nyakati, na kusoma katika historia, ambapo vita viliufunika ulimwengu.” Hiyo ni kweli.

⁹⁵ Bali kamwe hapana wakati ambapo dunia nzima ingelipuliwa vipande-vipande, katika sekunde moja tu. Mnaona? Na maangamizi kama hayo, yangechukua majuma na saa, na kadhalika, sasa yanachukua dakika moja, labda si hiyo. Kubonyezwa tu kwa kitufe, nayo imekwisha. Ni mbaya sana. Nao hawana. . . Cuba inaweza kufanya hivyo, yenyewe. Sio lazima iwe, ndogo tu. . . Haiti ingeweza kufanya hivyo. Taifa lolote dogo tu linalotaka kufanya hivyo, linaweza kuutia ulimwengu moto kabisa, na kuulipua utoke kwenye mzingo wake, wakati wowote watakao. Mnaona? Inahitaji tu mpindukia mpaka mmoja, ambapo pana makumi ya mabilioni ya hao kote ulimwenguni, kufanya hivyo.

⁹⁶ Angalieni kisa cha kujiua kifike tu kule juu, na kuwa miongoni mwao, naye amepagawa kabisa na ibilisi, mahali tu hivi vibanda vikubwa vya ndege vilipo, kubonyeza tu kitufe hicho kimoja, nayo haya hapa yanaenda. Na mara hayo yakienda juu, yako kwenye skrini za rada za wengine; wao wanabonyeza zao, na haya basi. Mnaona? Hivyo tu. Maana, wananinii tu. . . Kila jamaa ametoa skrini yake, anaangalia, huko nje baharini, nyambizi, huko nje visiwani, kila mahali. Wamekaa kule, huko kwenye Ncha ya Kaskazini, chini katika Ncha ya Kusini, kila mahali, pamoja na skrini hizi kubwa. Acheni tu mtu fulani abonyeze kitufe, hivyo tu ndivyo wanavyotaka. Ndipo hapa kitufe chao kimebonyezwa, nao hao wengine wabonyeze, na kubonyeza na kubonyeza. Basi ni nini kitakachofanyika? Lakini, loo, ninii. . . Wazia, ya kwamba hiyo ingeweza kutukia kabla hatujatoka ibadani asubuhi ya leo.

⁹⁷ Lakini, kumbukeni, kabla hilo halijatukia, Mungu ameahidi kulijia Kanisa Lake, aliahidi kuja, kwa hiyo hatujui ni wakati gani hasa Yeye atakapokuja. Ni jambo adhimu jinsi gani! “Kwa wale wote wapendao kuonekana Kwake, Yeye ataonekana.” Msininii. . . Hivi msingependa kumwona Yeye asubuhi ya leo? Na huku tukiimba ule wimbo mdogo, “Ninataka kumwona, kuuangalia uso Wake. Hapo kuimba milele juu ya neema Yake iokoayo.” Wakati maisha yote yamekwisha, na shida na huzuni zimepeperushwa kwa mara ya mwisho, nasi tutamwona. Nasi hao hapo tumesimama, vijana, wasiopatikana na mauti, daima katika Uwepo Wake. Ambako kamwe hakutakuwako na dhambi, maradhi, huzuni, majonzi, wakati muda wote utafifia na kuingia katika Umilele. Mbona, ni wakati mtukufu jinsi gani!

⁹⁸ Na ndipo hilo linakufanya ufanye nini? Unataka kufanya

kazi sasa, kumweka kila mmoja kwenye mahali hapo, uwezapo, kwa ajili ya huo Unyakuo. Nataka . . .

⁹⁹ Nimejiweka wakfu upya, pia nime—nimemwahidi Mungu ya kwamba ningejaribu kufanya sehemu maradufu. Ni—nimefanya kila kitu nijuacho kufanya. Na laiti tu ningalikuwa—ningalikuwa jamaa mdogo tena, umri wa miaka kumi na minane, ishirini, na kujua yale nijuayo, jinsi ambavyo labda ningeweza kusimama muda mrefu zaidi kidogo, niwatembelee wengi zaidi, kitu kama hicho, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

¹⁰⁰ Enyi vijana asubuhi ya leo, mlio vijana, mna ujana mwingi ndani yenu bado, wala hamjajifunga na familia na kadhalika, Mungu na awawezeshe kuona hili ono, kuona—kuona ni wakati gani tunaishi.

¹⁰¹ Kule kutokuwa na hakika. Hebu tuangalie tu mambo machache yasiyo na hakika sasa, katika wakati huu wenye mashaka. Kuna mashaka juu ya . . . Kwa kuwa tulinena juu ya vita, kuna mashaka katika sauti ya jemadari wa vita. “Hatuwezi kuelewa.” Hawajui. Mnaenda, nao watakuwa na mikutano mikubwa, na kadhalika, wala kamwe hawawezi kukutana pamoja. Kuna mashaka. Hawajui. Hawajui yatakayotukia. Wenye mikakati mashuhuri wote, na kadhalika, wanaochunguza vita, na uwezekano na jinsi hii itakavyotokea, hawana jibu asubuhi ya leo. Hakuna mtu aliye nalo. Kamwe hawawezi kukwambia.

¹⁰² Vema, sayansi, baada ya mambo yote makuu ambayo wangeyawazia, mikakati yote mikuu ambayo wangeweza kupitia, mbinu zote za kisayansi na swichi ambazo wangeweza kuvuta, za mitambo yao ya kisayansi, na—na waanzilishi wao wakuu, na wataalamu wanaowashauri wataalamu; na walipoweka yote pamoja katika saa hii, walisema jambo moja, “Ni dakika tatu kabla ya usiku wa manane.” Hilo ndilo jibu lao.

¹⁰³ Ama, “Je, tunaweza kuponea hayo? Tungeweza kuchimba chini na kwenda juu, kuingia chini kilindi cha kutosha, tusije tukafikiwa na hayo mabomu, na kuponea kama taifa?” Bila shaka hungeweza. Ingelipua kufikia kilindi cha ma—maili moja ardhini. Vipi kama ulikuwa kwenye kilindi cha maili kumi? Kama ungeweza, ungekuwa kwenye lava. Lakini vipi kama . . . Kama ungeweza kufikia umbali huo, mtikisiko ungeweza tu kuuvunja kila mfupa mwilini mwako. Hakuna njia, chini.

¹⁰⁴ Njia ni juu. Loo, nina furaha sana kuwa na Jibu! Nanyi je? Sauti ambayo ni ya hakika.

¹⁰⁵ Hiyo baragumu, ya kuchimba chini na kuingia katika mapango. . . Sasa nasikia ya kwamba wanaihamisha serikali yote na kadhalika huko nje, karibu na Fort Knox, na huko chini karibu na Pango la Mammoth, nao wana mahali huko chini ambapo wanatengeneza. Ili kwamba ninii. . . Kama kukitokea kitu kama ugomvi mdogo wa vita ama chochote kile,

wataipeleka serikali ndani ya mapango haya. Hivi Biblia haisemi dhahiri wangejificha katika mapango na kadhalika ya ardhi? Kweli kabisa. Mnaona? Hawana jibu. Kwa hiyo, mfumo wetu mkuu wa nguvu za kijeshi hauna jibu.

¹⁰⁶ Sasa, tulikuwa, sayansi yetu ingesema, “Tunaweza kutengeneza mtambo mkubwa. Tuna bunduki bora kuliko Ujerumani ingaliweza kuunda. Tuna wa—wa—watu walio na ujasiri mwingi na nguvu, na maskini Yankee mwenye kulisimua, na kucheza ngo—ngoma, na—na baragumu ndogo, na kupiga, na zile bendera kupeperushwa, na maskini huree, na kila kitu namna hiyo. Jamani, tunaweza kwenda kule, nasi tunao ujasiri wa kale nyuma yetu, kulifanya.” Haiwabidi kwenda kule. Huu ndio wakati mmoja tutavipata nyumbani. Mnaona?

¹⁰⁷ Inambidi jamaa mmoja tu kubonyeza kitufe, hilo tu ndilo linalopaswa kutukia. Mtu mmoja. Haiwabidi kuwa na askari elfu moja waliofunzwa. Pawe tu na mtu mmoja asiye na akili, amepagawa tu na ibilisi, kubonyeza tu kitufe hicho, na hilo latosha. Mnaona?

¹⁰⁸ Kwa hiyo hawana jawabu, kwa hiyo hatimaye walikuja kusema nini? “Vema, ni dakika tatu ifike usiku wa manane.”

¹⁰⁹ Ninayo—ninayo sinema ya hilo. Imekopeshwa daktari rafiki yangu sasa, *Dakika Tatu Ifike Usiku Wa Manane*. Sasa, sinema hiyo ilitengenezwa yapata miaka mitano iliyopita, wakati Wayahudi walipoanza kurudi Palestina mara ya kwanza. Na sinema pale inawaonyesha wakiwaleta wazee viwete mgongoni mwao, wakitembea. Nao wanaenda kote, wakiwahoji. Na kwa hiyo walipowauliza, kasema, “Kwani mnarudi kwenye nchi ya uenyeji, m—mpate kufia katika nchi ya uenyeji?”

¹¹⁰ Kasema, “Tumerudi kumwona Masihi.” Uh—huh. Naye nabii aliahidi nini?

¹¹¹ Wengi wenu mlisoma gazeti la *Look, Life*, na hayo mengine. Walikuwa na picha ya hizo ndege zikiwaleta huko, kutoka huko chini mahali mbalimbali, chini, Irani na mahali walipokuwa. Na, wakati, walikataa kuingia kwenye ndege hiyo. Kamwe hawajaona... Wangali wanalima kwa plau za kale za miti, kama walivyofanya yapata miaka elfu mbili mia tano iliyopita, wakati Himaya ya Kirumi ilipowatawanya. Nao—wao walikataa kuingia hizo ndege. Lakini maskini... .

¹¹² Maskini kuhani wao akaenda pale, mmoja wa marabi wa kale, walimu, akaenda huko na kusema, “Hivi Mungu hakutwambia ya kwamba siku moja tungerudi kwenye nchi ya uenyeji wetu, ‘Juu ya mabawa ya tai?’” Wakazilaza plau zao chini, wakaingia kwenye ndege na kuruka wakarudi nyumbani, juu ya hayo mabawa. Isaya aliiona, bali hakujua ilikuwa ni nini. Ilionekana tu kama ndege wa angani akiruka. Aliwaona Israeli wakirudi, wakipunga mikono yao huku na huku. Nanyi mliruka

kwa ndege, mnajua ni kitu gani. Ni wimbi, huku na huku, kama tu ndege wa angani akiruka, wakirudi nyumbani.

¹¹³ Wakatoka humo, wakasema, “Vema, Masihi yuko wapi?” Walitaka kumwona. Nami nawaambia, mnapowaona Wayahudi wakirudi namna hiyo, hicho ni kipimo cha Mungu cha wakati. Tuko kwenye mwisho.

¹¹⁴ Sasa hivi karibuni tu lilifanyika taifa, wakawa yote waliyo, na kupata pesa zao wenyewe, na jeshi lao wenyewe, na kila kitu, kila kitu chao. Wao ni taifa tena. Mnaona? Loo, ni wazo zuri jinsi gani! Nina Maandiko juu ya hilo, chini kidogo humu, naam, juu ya hilo.

¹¹⁵ Sasa mashaka ya...ya vita. Hatujui ni wakati gani. Sikilizeni kwenye redio. Mnawasikia wakisema kwenye redio, “Weka kiasi fulani cha vitu kwenye chumba chako cha chini. Weka akiba maji ya kutosha, kwa ajili ya mnururisho. Weka redio yako mle ndani, na ustarehe.” Ninaona kwenye magazeti, wanatangaza mijengo midogo ya kuingia, kuketi kwenye chumba chako cha chini ama katika uwanja wako, ama kitu fulani. Mabomu yakianza kuja, unusurike, mnururisho utakupata, kwa vyovyote vile, kwa hiyo haikubidi kuhofu. Wangeweza kuangusha bomu huko chini New Orleans, nao mnururisho ungekupata hapa. Kwa hiyo haijalishi, ungekufa kwa vyovyote vile. “Kwa hiyo kaa ndani, na ukae hai muda kidogo zaidi,” ama kitu kama hicho. Loo, jamani! Hata siliamini. Ninaamini ni upuuzi hata kujaribu hilo. Hiyo ni kweli.

¹¹⁶ Ila Kanisa halipaswi kuhofu. Hamtakuwa hapa wakati huo, kwa vyovyote vile. Mnaona? Hilo ni jambo moja la hakika. Mnaona? Hamtakuwako, maana uhakika wa Neno la Mungu unaahidi hivyo.

¹¹⁷ Sasa hebu tuchukue tu kitu kingine ambacho hakina uhakika, kuna mambo mengi sana. Kazi hazina uhakika. Hujui ni wakati gani. Unafanya kazi leo, na kesho hujui. Hakuna uhakika. Utakuwa na kazi nzuri, unafikiri. Ndipo kesho yake, bosu anakuja huko, anamchukua mtu mwingine, na kukufukuza, anamweka mtu mwingine humo. Kwa hiyo, ni kutokuwa na uhakika wa kazi.

¹¹⁸ Hebu tuchukue, pia, maisha ya nyumbani hayana uhakika. Nawaambia, sijui nini kilichoupata uadilifu wa wanawake wetu. Talaka zinaongezeka. Mimi...Ni la kuchukiza sana. Na mnaona ambavyo mahakama za talaka zimejaa watu. Ambako wasichana na wavulana watafunga ndoa na kuishi pamoja, na kupata watoto wawili ama watatu, ama kitu kingine namna hiyo. Nao watatengana, na kuondoka na kuoa mwingine, na kuoa mwingine, na kuoa mwingine, na kuoa mwingine, na kuoa mwingine. Na makazi yao je?

¹¹⁹ Nilikuwa katika nyumba maskini, nyumba maskini sana, hivi majuzi usiku. Huyu mwanamume akasema, “Nakwambia,

kamwe si—sijui.” Kasema, “Sijui kabisa jinsi nitakavyomudu maisha.”

¹²⁰ Nikaangalia huku na huku. Yeye alifanya kazi. Alikuwa na maskini mke pale, mkweli na mwaminifu awezavyo kuwa, na maskini watoto wanne ama watano wadogo wenye nyuso chafu hapo sakafuni. Nikasema, “Jamani, wewe ni milionea.”

¹²¹ Naye akasema, “Huh! Vema, Ndugu Branham, nisingelipinga neno lako.” Akasema, “Ndugu, sina hata hela.”

¹²² Nikasema, “Lakini una kitu fulani ambacho pesa haziwezi kununua.” Nikasema, “Unaye maskini mke hapa ambaye labda hana nguo mbili zake mwenyewe.” Na—na kama alikuwa nazo, ni zile mtu fulani alizompa, maana mtu huyo hupata tu kibarua cha kutwa, mara kwa mara. Nami nikasema, “Angalia hapa, bali huyo mke ni mwaminifu tu awezavyo kuwa.”

Nikasema, “Kuna watu wengi walio na mamilioni, usiku wa leo, angetoa kila hela aliyokuwa nayo, apate kujia nyumbani kwa mke kama huyo. Kweli.” Nikasema, “Mke wake yuko huko nje na kundi la wanaume mahali fulani, kwenye baa mahali fulani, akilaani, kuimba, kuvuta sigara, akitangatanga usiku, na vitu kama hivyo. Na hata hivyo anampenda, lakini angalia kile alichu nacho. Maisha yake yote yamezamishwa katika mwanamke huyo, na hebu angalia jinsi mwanamke huyo afanyavyo.”

¹²³ Na vinginevyo, mwanamke kwa mwanamume. Mnaona? Ninii. . . Hakuna tofauti. Imefikia wakati ambapo wote, kila kitu, ni lu—lundo moja tu la dhambi. Maskini mwanamke nyumbani, akijaribu kuwahudumia watoto wake, naye mumewe huko nje mahali fulani, akinywa pombe na kupiga makelele, anatembea na wanawake wengine. Angetoa nini, iwapo alikuwa na mamilioni ya dola, apate kumwona mume huyo amekuwa mwanamume halisi? Ipo njia moja tu kwa hilo kutukia, Yesu Kristo ndiye jibu! Hakuna chochote kinachoweza kusaidia. Ni wakati wa mwisho. Ni Kristo, na Yeye pekee.

¹²⁴ Sasa, basi, nikasema, “Ni maskini baba wangapi wanaoenda huku na huku siku hizi, wakiwa na mamilioni ya dola, wangetoa kila kitu walichokuwa nacho, kama maskini mtoto huyo mwenye kifafa aliye naye angekuwa na afya tu kama wako hapa usiku wa leo? Mnaona?” Akaanza kuniangalia.

¹²⁵ Nikasema, “Angalia. Ulisema ulikuwa na soseji na maharagwe, na mkate; ya kwamba ulitoa pesa zako alasiri ya leo, ukanunua mkate na maharagwe, kwa ajili ya watoto wako usiku wa leo.” Nikasema, “Kila mmoja wao akiwa na tumbo zuri, na angeweza kula. Nawe ulikula, pia.” Ni wangapi wenye ma- . . .

¹²⁶ “John D. Rockefeller alisema nini? Yeye angetoa dola milioni moja, kama angeweza kula mlo mmoja wa kabeji.” Nikasema, “Ulisema uliketi karibu na dirisha asubuhi ya leo, upepo baridi ukipenya ndani. Yeye, akiketi katika ikulu, mnaona, mahali

fulani. Lakini, hata hivyo, kama ingekubidi kuketi pale na kula mlo wa kabeji, penye upepo huo baridi unaopenya ndani, ukachomeka kipande cha karatasi mle.” Nikasema, “John D. Rockefeller angetoa dola milioni moja, apate kula mara moja kama vile unavyoweza kula, wakati wowote.”

¹²⁷ “Ni vipofu wangapi, wakiwa na fimbo mkononi mwake, akitembea akigongagonga mtaani, angetoa kila hela aliyo nayo, kwa ajili ya macho yako?” Mnaona? Kamwe huwezi kutathmini vitu ambavyo kweli ni tajiri, kwa vitu tunavyoviita tajiri.

¹²⁸ Sasa samahani, washiriki wa kanisa. Hiyo ndiyo sababu tunajaribu kusema, asubuhi ya leo, huwezi kulitathmini kanisa lenu kubwa, minara yenu mikubwa, na kadhalika, kwa upendo wa Mungu ulio moyoni mwetu, kwa yale Roho Mtakatifu anayokupa. Havina kifani. Mambo haya ni ya kimbinguni. Huenda ukafikiri ya kwamba sisi ni wa kipekee, kwa sababu unawasikia wakina kwa lugha na kufasiri, na watu wanalia, na kupiga makelele na kupiga mayowe. Afadhali niwe nayo kuliko yote. Afadhali niwe mchungaji wa jengo bovu kama hili, ambamo nguvu za Mungu hukutana na watu, ambako Kanisa hukutanika pamoja na vitu hivyo namna hiyo; kuliko kuwa na kanisa kubwa zaidi lililopo katika ulimwengu mzima, kuhubiria, pamoja na kundi vuguvugu, baridi, la wenye kukiri, wanaodhaniwa ni Wakristo, ulazimike kuchunga kila neno usemalo, wala huwezi kuhubiri kwa uvuvio. Inakubidi kuwa nalo *hivi-hivi*, na kumwangukia kila hakimu na kila daktari, na kila kitu humo ndani, usije ukasema kitu cha kuudhi hisia zao, kwa kuwa hao ndio wanaolichangia sana hilo kanisa. Nitashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Amina. Huwezi kulitathmini. Hakuna njia ya kufanya hivyo.

¹²⁹ Kwa hiyo basi, leo hii, mtu ambaye ni tajiri ni mtu ambaye yuko ndani ya Kristo. Sasa, tuseme ulikuwa na macho mazuri, afya nzuri, pesa nyingi na kila kitu kingine, lakini, hata hivyo, bila—bila Kristo, umepotea. Wewe ni mwenye mashaka, mnyonge, maskini, kipofu, uchi, wala hujui. Unaona? Hivyo ndivyo Wakati wa Kanisa la Laodikia ulivyokuwa. Huenda ukawa mfuasi wa kanisa lililo kubwa sana nchini. Huenda ukawa mfuasi wa dhehebu lililo kubwa kuliko yote, bali iwe ungali umepotea iwezekanavyo. Mnaona? Kwa hiyo, tajiri ni mtu ambaye yuko ndani ya Kristo. Hiyo ni kweli.

¹³⁰ Sasa, mashaka ya maisha nyumbani, mashaka ya kazi, mashaka ya vita, mashaka ya makanisa.

¹³¹ Kwa kuwa tumelifikia hilo, hebu tuzungumzie tu hilo kwa dakika chache, mashaka ya maisha ya kanisa. Hayo, wewe—wewe unaninii tu... Hu—huwezi kamwe kuyatathmini, ni vigumu, kwa sababu hakuna njia ya kutathmini kile ujuzi katika Roho Mtakatifu ulicho, kwa uanachama wa kanisa. Mnaona? Hakuna njia. Hakuna—hakuna njia ungaliveza kumnunua huyu

Roho Mtakatifu. Yeye huja kama zawadi ya bure kutoka kwa Mungu. Humjia yeyote atakaye . . .

Unasema, “Ataenda tu kwa Pentekoste?”

¹³² Pentekoste siyo dhehebu. Walijaribu kufanya hivyo, bali huwezi kumuundia Mungu dhehebu. Pentekoste ni tukio ambalo mwaminio yeyote anaweza kupata. Mnaona? Ni kwa Wabaptisti, kwa Katoliki, kwa Wayahudi; kwa weusi, kwa wazungu, kwa wa hudhurungi, kwa wa manjano, kwa wekundu; kwa rangi yoyote, kanuni ya imani, ama chochote; kama wewe ni maskini, tajiri, huna chochote, una vingi; kama uko katikati, ama yeyote uliye. Wewe, ni kwa ajili yako.

¹³³ Na ni upendo na rehema ya Mungu uliyopimiwa wewe, kuuchukua. Haikugarimu hata kitu kimoja. Kitu tu inachokugarimu, ni kujitolea maisha yako Kwake, na kuipokea. Ni rahisi jinsi gani! Pata tu yote. . . Sahau tu yote uliyowahi kujua, na ujitolee tu Kwake. Na hivyo ndivyo inavyokuja, ni kumpokea tu, kumpokea hivyo.

¹³⁴ Madhehebu, kamwe isingewezekana. Madhehebu hutoa sauti isiyotambulikana. Sasa hebu mimi ni—ni—niwaonyeshe tu kwamba ni—ni sauti isiyotambulikana. Ukienda kwa dhehebu *hili*, wao wanasema, “Tunalo. Hao wengine hawana.” Vema. Ukienda kwenye dhehebu lile. Uende kwenye hilo lingine, “Tunalo. *Hao* hawana.” Mnaona, kila dhehebu. Kuna madhehebu mia tisa mbalimbali ya makanisa. Mia tisa na sitini na tisa, nafikiri, hasa, kulingana na takwimu. Madhehebu mia tisa na sitini na tisa mbalimbali ya makanisa, na kila moja hudai “hilo lingine limekosea,” nao “wamelipata.” Kwa hiyo hiyo hasa ndiyo kiwango cha sauti isiyotambulikana. Uh-huh. Mia tisa na . . .

¹³⁵ Lakini Hili linasikikaje, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele?” Hakuna mashaka juu ya Hilo, sivyo? Hiyo ndiyo njia ya kutathmini. Hapo ndipo pa kupata mahali Kweli ilipo. Mnaona?

¹³⁶ Mnasema, “Sisi Wamethodisti tunayo. Sisi Wabaptisti tunayo. Sisi Wakatoliki tunayo. Sisi Wapresbiteri tunayo.”

¹³⁷ Vema, Yesu Ndiye aliye Nayo, kwa kuwa Yeye alisema, “Mimi ndimi Nuru, Kweli, Njia.” Kwa hiyo, ni Kristo ndani yako.

¹³⁸ Kwa hiyo haya madhehebu mbalimbali makuu bila shaka ni tofauti, nayo yanatoa sa—sauti isiyoweza kutegemewa kabisa. Na chochote kisicho na hakika kama hayo, hakiwezi kutegemewa, pia. Chochote chenye mashaka hakitumainiki. Huwezi kutegemea kujiunga tu na kanisa, na kusema hilo Ndilo. Kwa sababu, kila moja linatoa sauti tofauti, nawe unaelekea wapi? Unachanganyikiwa. Kama kulikuwako na mahali. . . Nimetoa tamshi hili mara nyingi. Ninalisema tena asubuhi ya leo. Mahali pabaya zaidi panapohitaji wamishenari, nipajuapo, ni Marekani. Kafiri ni nani? *Kafiri* ni “asiyeamini.”

139 Vema, sasa, tuna, katika Afrika, na—na huko chini Tailandi, na sehemu mbalimbali nchini, tuna ka—kafiri mwenyeji anayeabudu sanamu. Nasi tunamwita kafiri kwa sababu anaabudu sanamu; hajui mkono wa kulia na wa kushoto, hajui ABC zake. Yeye, jambo pekee ajualo, ni, hiyo ni mungu ambaye mchawi alimwambia habari zake, “Na hapo ndipo Mungu alipo, ni katika hiyo.” Na jambo pekee ajualo sasa ni, kupata chakula, na—na kula, vyovyote awezavyo kukipata. Sasa huyo ndiye tunayemwita kafiri. Lakini, sasa, mtu huyo si mgumu sana kumshughulikia kama ukimletea Ukweli.

140 Lakini mtu aliye mgumu sana kushughulikia ni kafiri huyu mwenye elimu, mnaona, kafiri huyu hapa Marekani, aliye na digrii nne za chuoni, anayesimama nyuma ya mimbara, asiyeamini.

141 Useme, “Vema, tulikuwa na ibada hivi majuzi asubuhi, naye Bwana akamponya ma—mama fulani huko chini.”

142 “Huh! Huh!” Huyo ni kafiri. Yeye ni kafiri tu mwenye elimu. *Kafiri* ni “asiyeamini.”

143 Juzi, wakiketi chini mahali pale, kuna kundi la watu, baadhi yao wako hapa sasa, maskini mama mmoja alikaribia kwa gari, hapo mbele. Kulikuwa na watu watano ama sita ndani. Kulikuwako na mama mmoja aliyekuja kwa gari, hapo mbele, kwa trela. Mtu akaja mlangoni, na kusema, “Ndugu Branham, ninachukia kupita ishara ile pale. Lakini,” kasema, “tunapita tu, nasi tunataka kusema . . .”

Nikasema, “Karibu.” Mnaona? Nami nikasema . . .

144 “La,” kasema, “mke wangu anataka tu kushuhudia, kukwambia jambo fulani lilitukia.” Vema, alitokea kuwa ni rafiki msiri wa Dada Mercier; Ndugu Leo hapa, mmoja wa ndugu zetu hapa kanisani, mmoja wa wanaume wa kanda, mama yake.

145 Basi yapata miaka minane ama kumi iliyopita, nilikuwa mahali fulani Mashariki hapa, ndipo mwanamke akaja jukwaani apate kuombewa. Roho Mtakatifu akasema, “Wewe ni Bibi *Fulani-wa-fulani*, nawe umetoka mahali fulani. Unaugua *hiki-na-hiki*.”

“Naam. Hayo yote yalikuwa ni kweli.”

146 Hapo akasema, “Sasa, unaye rafiki anayeishi California, ambaye ni rafiki msiri wako sana. Naye mwanamke huyu yuafa, kwa kansa ya figo.”

Kasema, “Hiyo ni kweli kabisa, Ndugu Branham.”

147 Huyo ni Roho Mtakatifu akizifunua siri za moyo, mnaona. Inapaswa kuwafanya Wamarekani waanguke kifudufudi na kusema, “Mungu!” Mnaona? Linapaswa kufanya hivyo.

¹⁴⁸ Lakini, loo, hao ni makafiri wenye elimu. Hao ndio walio wagumu kushughulikia. Mnaona, yeye ni mwerevu sana, “anjua mengi kuliko Mungu ajuavyo,” kwa hiyo hiyo ndiyo sababu anachotarisha mahindi yake, anachotarisha mifugo wake, na kila kitu. Mnaona mahali amejifikisha? Anarudi moja kwa moja, akifanya tu kwa urahisi, vema, uzao potovu wa nafsi yake, hiyo ni kweli, kwa kufanya hivyo. Katika uzalishaji wote wa nia zao, wa roho, yeye kwa urahisi anaenda kombo, kwake.

¹⁴⁹ Sasa tunaona ya kwamba mwanamke huyu alisema, “Naam. Hiyo ni kweli. Kweli ninaye rafiki aliye California, anayekufa kwa kansa ya figo.” Nikasema, “Wewe mwandikie umwambie, ‘BWANA ASEMA HIVI. Hatakufa, bali ataishi.’”

Na huyo alikuwa ndiye mama aliyekuwa hapo nje. Naye akasema, “Hiyo imekuwa labda yapata miaka kumi, kumi na miwili iliyopita.” Kisha kasema, “Nilipona, niko mzima na mwenye afya. Hakuna dosari katika figo hilo,” ambalo aliponya. Kasema, “Yapata miaka mitano baada ya hapo, nilipata kivimbe, nacho hicho kivimbe kikakua kupita kiasi, hata kikawa,” ninaamini alisema, “ama inchi kumi na saba au ishirini na saba kuingama.” Naye alikuwa ni mkubwa sana, hata asingeweza kusimama, akiwa na hiki kivimbe. Alipojaribu kusimama, asingeweza kusimama wima.

¹⁵⁰ Ndipo wakamleta kwenye kanisa hili, na kumketisha chini papo hapo. Nao wakamleta usiku tukiisha kumaliza ibada ya uponyaji asubuhi hiyo. Ndipo ndugu hapa, wakamwambia kwamba hatutawaombea wagonjwa usiku huo. Kwa sababu tulikuwa tukitaka... Nilikuwa nimewaombea wagonjwa asubuhi hiyo. Nao hawakutaka kuweka mzigo mkubwa sana juu yangu wakati mmoja. Na kwa hiyo baada ya ibada kumalizika, lakini baada ya ibada kumalizika, mimi nikisimama, nikizungumza na watu fulani. Ndipo wanaume fulani wakamshika mwanamke huyu na kumbeba karibu na nyumba, na kumketisha kwenye kile kipandio pale wakati wakitoka. Naye alikuwa ameketi pale; hao wanaume wakimbeba.

¹⁵¹ Naye Ndugu Taylor, mmoja wa ndugu zetu wa thamani hapa, wa hili kanisa, alikuwa pale pale ambapo, wakati lilipotukia, nami nafikiri, alimsaidia huyo mwanamke hapo. Uko hapa Ndugu Taylor? Uko wapi? [Ndugu Taylor anasema, “Amina.”—Mh.] Nyuma, naam, nyuma *hapa* ndani. Alikuwa amesimama pale, akiwepo, na kumsaidia hapa huko nyuma.

¹⁵² Nao huo uvimbe, umetokeza *hivi*. Na kwa hiyo—na kwa hiyo basi kasema... Nilipotokea kwenye mlango wa nyuma, niliangalia chini tu na kumkazia macho, kasema, “Mwanamke, Bwana Yesu aliyekuponya ule ugonjwa wa kansa ya figo, miaka mingi iliyopita, atakuponya uvimbe huo pia. BWANA ASEMA

HIVI.” Kamwe sikumgusa wala chochote kile; nilitoka tu nje nikaingia kwenye gari, nikaondoka. Nami nikaenda. Mnaona?

Akasema, “Utakuja kumwanguka?”

Nikasema, “Naam. Hakika. Mwambie, aingie ndani.”

Kasema, “La. Hatuna wakati. Inatubidi tu kuondoka.”

¹⁵³ Akaenda huko nje. Ndipo maskini mwanamke, akaruka nje ya gari, mwembamba tu kama nilivyo mimi. A—alikuwa na wakati mzuri sana, huko nje barabarani, akikimbia huku na huko barabarani. Akinena kwa lugha, na kupiga mayowe, kwa sauti yake yote, mbele ya nyumba ya mchungaji wa Kipresbiteri, akiwa tu na wakati mzuri sana.

¹⁵⁴ Sasa, baadhi ya majirani huenda walianguka nje, wakawazia, “Vema, huyo hapana shaka ni baadhi ya wanaotoka kwenye hospitali ya wendawazimu, wanaokuja kuombewa na Ndugu Branham.” Mwanamke huyo hakuwa ametoka kwenye hospitali ya wendawazimu. Nafsi yake ilikuwa imerudi tu kutoka Utukufuni, mnaona, akiwa na wa—wakati wa ajabu sana.

¹⁵⁵ Akasema, “Angalia hapa, Ndugu Branham.” Akafungua koti lake; mwembamba tu anavyoweza kuwa. Akasema, “Sasa, kwa miezi ya kwanza miwili ama mitatu, baada ya wewe kuniambia hilo,” kasema, “Nilikuwa mahututi sana.” Kisha kasema, “Daktari alisema ha—hatajaribu kitu kingine chochote, kama nisingemruhusu kujaribu kukitoa kivimbe hicho humo.” Kasema, “Kingekuwa na uzito wa zaidi ya . . .”

¹⁵⁶ Alisema ni ngapi, “Yapata ratili thelathini,” ndugu, Ndugu Taylor? [Ndugu Taylor anasema, “Naam.”—Mh.] Yapata ratili thelathini, walikadiria ndio uliokuwa uzito wa hicho kivimbe.

¹⁵⁷ Kisha kasema, “Mara, ikaanza, ‘Shoo, shoo, shoo, shoo!’” Loo, Yeye hulitimiza Neno Lake. Hiyo ni kweli.

¹⁵⁸ Sasa kama ukitaka kumwandikia mwanamke huyo, tunayo anwani yake na kila kitu. Alimwachia Leo, kumsalimia mama yake kwa niaba yake, na kadhalika.

¹⁵⁹ Basi ilitokea kwamba ndugu yake alimwoa ra—rafiki yangu hapa juu Utica. Huyo msichana alikuwa mle ndani. Jina lake ni Clyde Raine. Ametekeleza yote, mengi, na ninii nyingi za . . . Chisel, ndivyo tunavyomwita. Nilicheza pamoja naye alipokuwa mvulana. Anaishi hapa juu Utica Pike, namna fulani ya afisa wa jimbo kule sasa.

¹⁶⁰ Naye dada yake alikuwa ameketi kwenye gari. Nao ni, nafikiri, huhudhuria kanisa la Wakampbeli. Nashangaa tu hilo lilileta dhana gani juu yake? Akasema, “Billy, ni ajabu sana.” Loo, nilikuwa namjua msichana huyo, mimi mwenyewe. Nimetoka pamoja naye, mara kadhaa, kama jamaa wadogo, tulipoishi hapa juu barabarani. Na—na ni msichana mzuri sana, mzuri tu awezavyo kuwa. Yeye ni karibu umri wangu sasa. Na

kwa hiyo, yeye, ameketi tu pale, akiusikiliza ushuhuda huo. Basi huyu alikuwa ni dada ya mumewe aliyekuwa ameponywa.

¹⁶¹ Loo, nakwambia, ndugu, hakuna mashaka kuhusu hilo. Hiyo ni Kweli. Hilo ni Neno la Mungu. Hilo linalifanya kweli. Kwa hiyo ninii . . .

¹⁶² Chochote kilicho na mashaka hakiaminiki. Na kwa hiyo wakati siku za wakati huu, wakati hawana uhakika kama Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, achana na kitu hicho.

¹⁶³ Wewe unaweza kuwa na hakika. Unaweza kujua ndivyo ilivyo. Kwamba ninii Yake . . . Kama kamwe hatafanya mwujiza mwingine wowote juu yako ila ule mwujiza mkuu, kuzisamehe dhambi zako! Huo ndio mwujiza mkuu kuliko wote ambao Mungu alipata kufanya, ulikuwa ni kumsamehe mwanadamu dhambi yake.

¹⁶⁴ Kumchukua mtu na kumwongoa kutokana na hayo mambo, angalia, ambaye ameubadilisha utu wake wa ndani kutokana na hayo mambo. Kwamba wakati mmoja alikunywa pombe na kucheza karata, na kufanya maovu na mambo kama hayo, na, mara, anamgeuza moja kwa moja, kupenda. Kisha anaenda nyumbani kwa mkewe, na kusema, “Kipenzi, ninasikitika nilikufanyia hayo.” Akawachukua maskini watoto wake wadogo, anawashika kwa mkono wake, “Baba alitumia pesa zake zote kwa viski, na baba amefanya *hivi*. Na—naye mama amekuwa nje usiku kucha, na kuwaacha nyinyi watoto. Kamwe sitafanya hivyo tena.” “Mungu, nisamehe.” Na jinsi ambavyo, ushuhuda huo, hilo ndilo moja ya mambo makubwa sana yaliyopo. Na Shirika lote la kusaidia Walevi Sugu, na yote namna hiyo, hawawezi kubadilika hivyo. Kamwe hawawezi kuyafanya kwa huyo mtu.

¹⁶⁵ Mwangalie maskini Rosella Griffith hapo, ameketi hapo, wakati Shirika lote la kusaidia Walevi Sugu huko Chicago, hospitali nne miongoni mwa zilizo kubwa, madaktari wake walikuwa wamemkatia tamaa. Katika muda wa dakika moja, jukwaani, akambadilisha maskini huyo mwenye macho ya kichaa. Akasimama hapo, huku koti lake limekatwa namna *hii*, amevaa koti la manyoya, ambalo mama yake alimnunulia. Alikuwa ni msichana mwerevu. Naye alibeba chupa zake za viski kwenye koti hilo pale, huku akihofia ataanguka mtaani, na kuganda hata kufa kabla mtu yeyote hajampata. Hapo, amesimama pale, wakati wote, Shirika la kusaidia Walevi na wote walikuwa wamemkatia tamaa. Yeye anaandika kitabu kuhusu hilo sasa.

¹⁶⁶ Huyo hapo akaja jukwaani. Roho Mtakatifu akamwambia, “Jina lako ni Rosella Griffith.” Hakuna shaka hapo. “Wewe ni mlevi sugu. Umekuwa kwenye Shirika la kusaidia Walevi Sugu na kila kitu. Lakini, BWANA ASEMA HIVI, imekwisha sasa.”

167 “Naye mama huyo anayeketi pale juu kwenye roshani, yeye ni mcheza dansi wa Fred Astaire, mwenzake.” Akaruka juu. “Hiyo ni kweli. Yeye pia ni mlevi sugu, na mwathiriwa wa dawa za kulevya. Sheria inamtafuta sasa.”

Ndipo baba yake akasimama, kasema, “Nachukia hilo.”

Kasema, “Ngoja kidogo, baba. Mtu huyo anasema kweli.”

168 Hakuna mashaka kuhusu hayo. “BWANA ASEMA HIVI, umeponywa. Jisalishe.” Sasa yuko hudumani, pamoja na mumewe, wakiihubiri Injili. Loo, jamani!

169 Ni kitu gani? Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Katika siku ambazo madhehebu hayana uhakika wake, kwa nini tulisikilize kanisa la kimadhehebu, wakati Kristo anabaki yeye yule? Hakuna mashaka kulihusu Hilo. Sikuzote ni ya hakika. Sasa, Bi- . . . Tunajua ya kwamba Biblia inasema hapa, kama . . .

170 Kitu chochote kilichokufa hutoa sauti. Kitu kilichokufa, makanisa yaliyokufa, ama chochote kile, kinaweza kutoa sauti; lakini isipokuwa hiyo sauti iwe dhahiri, isipokuwa kuna njia ambayo tunaweza kuwa na uhakika. Sasa, tunajua.

171 Hapa, ninayo Maandiko yaliyoandikwa hapa chini kuhusu askari. Naam. Askari wanaweza, katika siku za mafunzo yao, wamefunzwa kwa hizo baragumu ndogo. Na jinsi zinavyotoa sauti ya kurudi nyuma, ama wanayopaswa kufanya, na kila kitu. Wanafunzwa kwa sauti. Basi endapo—endapo hawakuijua sauti hiyo, wangejua je kujifanya tayari wenyewe? Hiyo ni kweli. Lakini wanafunzwa sauti hiyo. Nao wanajua, sauti hiyo inapotolewa, inamaanisha jambo fulani.

172 Jinsi, wakati Tito alipozingira kuta za Yerusalemu kwa jeshi lake, askari hao wote waliofunzwa; hao wanafunzi, jinsi wanahistoria wanavyoandika.

173 Yesu, akiketi juu ya ule mlima siku hiyo, alisema, “Mtakapouona Yerusalemu umezingirwa na majeshi; aliye shambani, asirudi nyumbani mwake, kuchukua koti lake. Aliye nyumbani asipande kwenye paa la nyumba ama kushuka.” Kasema, “Bali wakimbilie milima yao, kwa kuwa kutakuwako wakati wa shida.”

174 Sasa angalieni yale madhehebu yote makuu ya makanisa yaliyosema, walipomwona Tito akipanda juu kiaskari. “Sasa tutakwenda nyumbani mwa Bwana, kuomba dua.” Walikuwa wamechelewa kupita kiasi. Hiyo ilikuwa ni sauti isiyotambulikana, ya kuhani. Hiyo ilikuwa ni sauti isiyotambulikana ya kanisa.

175 Ila kwa wale ambao walikuwa wamezoezwa Sauti ya Yesu, walikimbilia mlimani kwa nguvu walivyoweza kwenda, nao ndio tu walionusurika. Sauti isiyotambulikana . . . “Utorokeni mji,” sasa, Yesu, kama hakuwa amewaambia hivyo na kuwapa hayo mafunzo, sauti hiyo ya mafunzo, wangejua je kukimbia?

¹⁷⁶ Sasa, Josephus, yule mwanahistoria mkuu, alisema, “Kitu pekee kilichonusurika kilikuwa ni hao wanafunzi wa—wa Kristo, ambao walikuwa wala watu.” Mmoja wa wanahistoria alisema walikuwa ni wala watu. Kasema, “Walimchukua mtu jina lake Yesu wa Nazareti, ambaye Pilato alimsulubisha, nao wakauiba mwili wake kutoka kaburini, kisha wakatoka wakaukatakata na kuula.”

¹⁷⁷ Walichokuwa wakifanya ni kula ushirika, “mwili wa Bwana,” mwajua, kama tunavyofanya hapa. Mnaona?

¹⁷⁸ Kisha kasema, “Hao ndio tu walionusurika, kwa sababu walitoka nje ya mji.” Walijua hiyo Sauti.

¹⁷⁹ Loo, ndugu, Roho Mtakatifu na aingie mioyoni mwetu asubuhi ya leo, atupe sauti ya hilo pigo la moyo wa Roho Mtakatifu na Nguvu Zake. Hiyo tu ndiyo itakayoweza kunusurika: sauti hiyo ya Parapanda ya Mungu, na mioyo yetu iliyofanywa tayari kwa ajili ya saa hii, kujua la kufanya.

¹⁸⁰ “Sisi tulio hai tuliosalia hatutawazuia ama kuwakawilisha wale waliolala mauti, kwa kuwa Parapanda italia.” Askari hao wote walio ng’ambo, wamelala usingizi, kote katika nyakati; bali Parapanda itakapolia, ingawa wamekufa katika usingizi, haitawazuia, kwa maana Parapanda italia na kuwaamsha. Wako tayari.

¹⁸¹ Hao wasio tayari, hawajui hiyo Sauti. Wakati hiyo—wakati hiyo Sauti, ya Kuja kwa Bwana, itakapolia, itaitikisa Mbingu na kuzimu, itakapolia. Lakini wale walio katika kuzimu, wale waliopotea, hawajui hiyo Sauti. Hawajui la kufanya.

¹⁸² Lakini wale, ingawa wamelala katika Kristo, wanajua Sauti hiyo ya uhakika.

Loo, Parapanda yake Bwana italia, na hapatakuwapo na wakati baada ya hayo,
Na asubuhi itapambazuka Milele, angavu na nzuri;

Wakati waliookolewa wa duniani watakapokusanyika nyumbani mwao ng’ambo ya anga,

Na wakati majina yaitwapo huko ng’ambo nitakuwako, nataka kuwa Huko.

¹⁸³ Weka jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwanakondoo, leo hii, kwa Damu ya Bwana Yesu, na haitakuwa ni sauti isiyotambulikana.

¹⁸⁴ Sasa tunasikia sauti ya maafa yakija, mabomu ya atomiki yakining’inia kila mahali, dhiki kati ya mataifa, na mshangao wa wakati. Kwa nini tuhofu kuhusu kazi? Kwa nini tuhofu kuhusu makazi? Kwa nini tuhofu kuhusu chochote?

¹⁸⁵ Yesu kamwe hakutwambia tuhofu, bali alisema, “Mtakapoyaona mambo haya yakianza kutukia, inueni kichwa

chenu, mkashangilie, kwa maana ukombozi wenu unakaribia.” Huo ndio uhakika wa sauti ya Injili.

¹⁸⁶ Tunapomwona Roho Mtakatifu akiingia kanisani, na kuanza kuyatambua mawazo ya moyo, akifanya ishara hizi kuu, kurudi kwa Roho katika wakati wa jioni wakati Nuru zinamulika, tunamwona akija na kufanya jambo lile lile alilofanya huko Sodoma, kabla haijateketezwa. Kumwona Malaika huku ameugeza mgongo Wake, akisema, “Mbona Sara amecheka?” nyuma Yake. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Ni kitu gani? Ni kule kutolewa kwa sauti ya Kuja kwa Bwana Yesu.

¹⁸⁷ “Tazama, nitawapelekea Eliya nabii kabla ya ile siku iliyo kuu na ya kuogofya itakayoungamiza ulimwengu. Atairudisha mioyo ya watoto iirudie Imani asilia, iirudie Injili, izirudie Nguvu za Mungu, imrudie Roho Mtakatifu halisi, imrudie Kristo tena, kabla haijaja ile Siku iliyo kuu.”

¹⁸⁸ Tunaisikia Parapanda ikilia. Loo, jamani! Ni kitu gani? “Amkeni, enyi watakatifu wa Bwana, kwa nini kusinzia wakati mwisho unapokaribia, na tujiweke tayari kwa ajili ya wito huo wa mwisho.” Kama ikitoa sauti isiyotambulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa vita, kama haitambulikani? Bali haina mashaka.

¹⁸⁹ Watu wanasema, “Ni kitu gani hiki wanachozungumzia, Roho Mtakatifu kuzisoma nia zenyewe za watu, na mambo anayofanya?” Huo ndio uhakika wa sauti ya Injili. Kristo alisema itakuwa hivyo.

¹⁹⁰ “Vema, haya makanisa yote makubwa yangeweza kuwa?” Kristo alisema ingekuwa hivyo. Haina mashaka. Ni uhakika wake. Ndio kwanza tumalize mkutano wa siku nane juu ya hilo, kujua ya kwamba Biblia inasema dhahiri ya kwamba kitu hiki kitakuwa hivyo. Madhehebu makuu yatainuka, yote yataungana kuwa muungano wa makanisa. Tunayo, yakifanya alama ya mnyama, ukasisi wa Katoliki. Sisi tutafanya sanamu ya mnyama. Hapo tunao, muungano, kila dhehebu ndani yake. Si sauti isiyotambulikana. Inatoa sauti halisi ya kweli. Ni sauti ya hakika.

¹⁹¹ “Tuna imani kuu katika UN, Umoja wa Mataifa.” Vema, ina kilindi tu kadiri Shirikisho la Mataifa lilivyokuwa nacho, kitu kile kile tu. Tulikuwa na Shirikisho la Mataifa, baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Walikuwa waulinde ulimwengu mzima. Haikufanikiwa. Mazungumzo halisi ya UN sasa hayana uhakika. Hawajui la kufanya. Wako mle ndani wakati Khrushchev alipovua kiatu chake na kulipiga dawati. Basi hilo lina faida gani? Na hayo yote mbalimbali. Ni kutokuwa na uhakika kwa UN. UN ni sawa, tuseme, bali imechelewa kupita kiasi. Imechelewa kupita kiasi kwa chochote kama hicho.

¹⁹² Kuna Sauti moja tu ya hakika. Hiyo ni Injili. Iweni tayari kwa vita. Vita vipi? Kule Kuja kwa Bwana. Jiwekeni tayari sasa kwa ajili ya vita dhidi ya uovu, wakati uovu unapowazinga watu kila upande. Kila kitu kikiharibika, na maisha ya nyumbani yakiharibika, na UN ikianguka, na mataifa yakivunjika, na mabomu ya atomiki pande zote, na nyumba zikigawanyika, na umama nao ukishuka, na utovu wa uadilifu miongoni mwa watu, na—na kutoaminiana mmoja kwa mwingine, madhehebu yote yakizozana na kugombana, mnataka kufanya nini? Iweni na hakika. Jiweke tayari kwa ajili ya vita.

¹⁹³ Wakati televisheni inaoza, na redio, na gazeti. Milango yote ya matangazo, kitu hicho daima ni sigara, tumbaku, na viski, na kunywa pombe, na wanawake waliovalia kizinifu. Mizaha michafu na wachekeshaji kwenye vipindi vya televisheni, huku Marekani ikivutiwa nayo. Kama vile ninii kubwa. . . Imeletwa kama nyumba ya Mfalme Nebukadneza ya—ya upumbavu usiku huo, wakati mkurupuko wa kiwazimu ulipopitia mle. Walikuwa na ka—karamu kubwa ya divai na dansi kule, na televisheni, kama ingalikuwaku siku hizo, wachekeshaji wao wakataka huko nje. Ndipo yakatokea maandishi ya Mkonu ukutani.

¹⁹⁴ Na, leo hii, wakati tulipowazia tuko salama kabisa, tuna wanasayansi walio bora kuliko wote ulimwenguni. Tunao walio bora kuliko wote ulimwenguni. Tumekuja kutambua, tuko nyuma kabisa, katika mbio za makombora. Uh-huh. Na basi ni kitu gani kilichotukia kwa Marekani? Sio tu maandiko kwenye ukuta, bali kuna kule—kule kurushwa kwa makombora kunakoandikwa angani, kwamba tuko nyuma kabisa, miaka kadhaa nyuma. Kuna nini? Yale maandiko ya mkono yako ukutani.

¹⁹⁵ Katika siku hiyo, yaliandikwa katika lugha isiyojulikana, maandiko ya mkono ukutani. Hapakuwapo ila mtu mmoja, katika ufalme wote, angaliweza kuyafasiri. Lakini alikuwa na karama ya ufasiri. Naye aliifasiri, na kusema, “Umepimwa kwenye mizani nawe umeonekana kuwa umepungukiwa. Mungu alilituma taifa la watu humu ndani miongoni mwenu, mnaowaita ‘watakatifu wanaojibingirisha.’ Mlishuka mkaenda kule na kuwatahayarisha, na kuwaua, na kuwakaba roho. Kisha mkawachukua miungu wenu na sanamu na kadhalika, na mmeabudu kwa hiyo, na kuishi kwa anasa. Na sasa mlienda na kuchukua vyombo vyenyewe kutoka hekaluni mwa Mungu wao, na kuja huku na kufanya mizaha navyo, mkifanyia utani wa, ‘mtakatifu anayejibingirisha, mhubiri mwenye upara,’ na yote namna hiyo. Naye Mungu ametosheka nayo. Nayo saa ya maangamizi yenu imekaribia.” Taifa lenyewe ambalo lingewachukua, lilikuwa linangojea langoni wakati uo huo. Kidogo tu baada ya hayo, waliangamizwa. Wanawake wao walikatiliwa mbali. Walinzi wao, jeshi lao, kila kitu, kilichukuliwa. “Umepimwa katika mizani, ukaonekana

umepungukiwa.”

¹⁹⁶ Nasi tumeingia kichaa cha redio na televisheni, na mizaha, na uchafu, na kinyaa, na upotovu, na ukaidi, na kila kitu, mpaka Mungu amechoshwa nayo. Wakati Injili, Injili ya kweli ya Kanisa la Roho Mtakatifu, iko huku na huku katika taifa, ikionyesha uhakika wa Yesu Kristo na Kuja Kwake, mpaka wakati umewadia hapa ambapo Mungu anaandika kote kwenye anga zetu, “Umepimwa katika mizani, ukaonekana umepungukiwa.” Amina. Tuko katika hali mbaya sana. Sikilizeni Sauti ya hakika, si UN yenye mashaka. Naam, bwana!

¹⁹⁷ Hata hivi majuzi, tulipokuwa na uchaguzi...Walisema hapa, siku moja, ya kwamba walipozihasabu kura za ulimwengu wa kisiasa, nao wangesema wakati huo, wanasema, “Tumeninii...Ninao mtambo sasa, ambao wote hawana budi kuwa waaminifu, kwa maana unavuta tu maskini nyenzo ndogo nayo inampigia kura mtu wako. Unaiivuta chini, kubofya kudogo, na kumpigia kura mtu wako.” Huh! Walikuta kwamba hilo halikuwa na uhakika.

¹⁹⁸ Bw. Edgar Hoover alikifichua kitu hicho, akakianika Chama cha Demokrasia hivi majuzi. Wakati walipofanya njama ya mtambo, hivi kwamba, kila walipompigia Bw. Nixon kura, iliwalazimu kumpigia Kennedy vivyo hivyo. Basi kwa nini hawafanyi lolote juu yake, basi, kama wakikuta kwamba iko hivyo? Kwa nini? Vema, hakuna uhakika kwake. Mna jua kile kingetukia, Bw. Hoover. Mnaona? Vema. Mnaona, kila kitu hakina uhakika. Huwezi kusema ni nani aliyechaguliwa, kama ni Kennedy ama kama... Kennedy aliitwa “mteule,” bali sijui kama amechaguliwa ama la. Sasa, mimi si mwanasiasa. Sijui lolote kuihusu. Bali ninajua kilicho kweli na kilicho uongo. Nina akili ya kutosha kujua hilo. Wakati likiwa moja kwa moja mbele zetu, ya kwamba mtu huyo amethibitisha, kwa FBI, ya kwamba walifanya njama na hiyo mitambo ipate kufanya hivyo. Haikuwa chama hicho kingine, kilichofanya hivyo. Ilikuwa ni cha—chama cha Kennedy kilicholifanya. Mbona? Haina budi kuwa hivyo.

¹⁹⁹ Hakuna kitu katika ulimwengu huu kinachoweza kusimama, nje ya Ufalme wa Mungu. Kwa kuwa kila ufalme “umepimwa katika mizani, ukaonekana umepungukiwa,” taifa letu. Ni kwa nini?

²⁰⁰ Hapa miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa na mti mkubwa hapa juu, nilikuwa nikiuendea na kuketi chini. Nami nikawazia, “Mti huo. Nitakapokuwa mzee, kama nikiishi, nitakuja na kuketi chini ya mti huo.” Ni kisiki tu sasa. Mahali nilipokuwa nikiishi, ningemwona baba yangu akija huko nje, na maskini mikono yake mifupi. Alikuwa, loo, Mkentakiki huko chini, naye alikata miti na kadhalika; jamaa mdogo, yapata pauni mia moja na arobaini na tano ama hamsini, ila ni mnene. Loo, jamani! Bw. Coots, hapa

juu, aliniambia alimwona akipakia gogo la majivu lenye uzito wa pauni mia tisa, peke yake, mtu tu mwenye nguvu kwe—kweli. Nilikuwa nikimwona akikunja mikono yake ya shati, apate kunawa huko nje, karibu na kipande cha kioo kilichobandikwa juu ya mtofaa.

²⁰¹ Na baadhi yenu watu wa Indiana huenda msijue jinsi ilivyotubidi kuishi zamani za kale mle ndani, pamoja na maskini karai ya kuogea huko nje karibu na gudulia, pampu. Naye mama alikuwa na maskini gunia chakavu pale, gunia la unga, akafanyiza taulo kwake, kidogo limepambwa; akatoa baadhi ya nyuzi na kufanya mapambo madogo nchani. Maskini ninii kubwa chakavu. . . Angenisugua sana kisha anipanguse kwa taulo hiyo, karibu ngozi itoke, kwa hilo gunia chakavu, la unga. Alikuwa akinisugua na kunipangusa kwa taulo hiyo chakavu.

²⁰² Sasa, ningemwona baba amesimama pale, anaingia, mwajua, na kuikunja maskini mikono midogo ya shati, naye angekuwa akinawa. Loo, jamani, kuiona hiyo misuli! Nikasema, “Unajua, ataishi kuwa miaka mia tano, ana nguvu sana.” Lakini mwajua nini? Alikufa alipokuwa na miaka hamsini na miwili. Kwa nini? “Hapa hatuna mji udumuo.”

²⁰³ Nilisimama huko Rumi, ambako—ambako wale Makaisari walisimama, waliotembea mitaani, wakiwa na umati wao mkubwa, na—na madoido na utukufu, na yote waliyokuwa nayo. Nanyi mwajua mahali pa kuupata ufalme wao? Ni futi ishirini chini ya ardhi. Miaka elfu mbili imeuzamisha.

²⁰⁴ Nilisimama huko Cairo, Misri, ambako yu—yule Farao mkuu alisimama, siku moja, aliyewatesa watu wa Mungu, aliyewafukuza na kuwafanya watumwa. Futi ishirini ama thelathini chini ya hapo, ndiko kuna magofu ya mahali pao.

²⁰⁵ Nilisimama huko London, Uingereza, ambako utawala wo—wote msonge mkuu na kadhalika umesimama, na yote hayo. Nami nikakuta, umezama chini ya ardhi. Ni kitu gani? “Hapa hatuna mji udumuo, bali tunautafuta Ule ujao.”

²⁰⁶ Kwa nini falme hizi? Ni kuwaambia tu, kuzungumza juu ya Ule ambao ni wa Milele. Ni kwa nini mti ni mzuri? Unangojea. Unangojea madhihirisho kamili ya wana wa Mungu, ambapo mti huo utaishi milele. Kuna Ufalme utakaokuja. Nayo—nayo Biblia ilisema, “Hapa hatuna mji udumuo, bali tunautazamia Mmoja ujao.” Na hapo Mungu ametupa Ufalme usioweza kutikisika.

²⁰⁷ Kila kitu duniani kinaweza kutikiswa na kinaweza kutetemeshwa, kinaanguka. Kila kitu kinaoza. Tunaishi katika ulimwengu unaokufa. Kila kitu kinakufa. Miti inakufa. Nyasi zinakufa. Maua yanakufa. Miji inakufa. Ulimwengu unakufa. Wewe unakufa. Kila kitu kinakufa. Mimi ninakufa. Kila kitu kinakufa. Miale fu—fulani ya asidi na kadhalika hewani, ambayo, kemikali hewani.

208 Hata kama ukichukua hili daraja kubwa hapa chini, nilipoliona likijengwa, miaka ishirini na miwili kabla halijajengwa huko chini, niliona baadhi ya watu wakipoteza maisha yao juu yake, wakati walipolijenga hilo daraja kuvuka pale, na kunena habari zake. Mama yangu alitaka kunipeleka kwa daktari, alifikiri nilikuwa nimeshikwa na kipindi cha wasiwasi. Nami nikamwambia. Nikasema, “Niliona daraja likivuka, nami nikawahesabu hao watu.” Miaka ishirini na miwili baada ya hayo, hilo daraja likavuka, na idadi iyo hiyo ya watu ikapoteza maisha yao. Nafikiri walikuwa kumi na sita. Kweli kabisa.

209 Sasa, nikawazia, wakati walipoweka hizo boriti kubwa huko juu, daraja hilo litadumu milele. Loo, wamelipaka rangi mara tatu ama nne, nalo linaingia kutu sasa hivi. Ni kitu gani? Miale hewani, inalianguza.

210 Tunaona msichana mrembo, wa miaka kumi na sita, ameketi kanisani, akizibua chingamu, akikata na kufanya vituko, akitoka nje na kuvuta nguo zake kufikia mahali fulani ambapo anaonekana wa kuvutia sana kijinsia, kujinyonganyonga kabisa. Na kabla ya kutua mara chache kwa jua, amezeeka na kuingia makunyanzi, na nyama zikianguka kutoka kwake. Nao maskini mwili huo mdogo aliounganyonga, na kuiacha roho fulani iishi mle, imtawale, iliyoukupilia mbali uadilifu wake kama takataka, naye awajibike, kwenye Siku ya Hukumu, kwa kufanya uzinzi. “Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye.” Pasipo kutambua ya kwamba yeye si kitu ila mavumbi, na anarudi mavumbini, kwa maana, “U mavumbi wewe, na mavumbini utarudi.” Ni kitu gani? Laiti angalitambua, na kukoma. Hiyo ni sauti isiyotambulikana.

211 “Vema, sasa, *fulani-wa-fulani* kwenye televisheni, *fulani-wa-fulani* shuleni,” akijaribu kuwaiga maskini watu fulani shuleni. Kamwe usiruhusu huyo awe ndiye kielelezo chako. Mtazamie Mungu.

212 Loo, sauti zisizotambulikana! Uchaguzi! Jinsi ambavyo wakati umewadia sasa, mashaka!

213 Laiti tungalikuwa na wakati, hebu tu tulifungue. Ninawaona akina dada, wote wakiyaandika hayo Maandiko, vema. Sasa katika Timotheo wa Pili 2, hebu tusome kwa dakika chache tu. Timotheo wa Pili, mlango wa pili, na kuanzia kwenye ninii wa 3. . . Timotheo wa Pili, mlango wa 3, hebu tusome tu. Sikilizeni hapa. “Jueni hili pia. . .” Sasa, huyu ni Roho.

Jueni hili pia, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari.

214 Sasa, huyu ni Roho Mtakatifu unayemsikia kanisani asubuhi ya leo, akinena huko nyuma kabisa, miaka elfu mbili iliyopita, A.D. 66, juu ya siku hizi.

Maana watu watakuwa wenye kujipenda, . . . wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi,

215 Angalieni siku hiyo, leo hii. Ungezungumza juu ya takatifu, wakuite “mtakatifu anayejibingirisha.” Waangalieni watoto, jinsi wafanyavyo. “Uhalifu wa vijana,” wanauzungumzia. Sasa nitatofautiana nawe, mzazi. Sio uhalifu wa vijana; ni uhalifu wa mzazi. Mnaona? Hivyo ndivyo ulivyo.

216 Baadhi yenu mnawaita hawa akina mama wa Kentucky hapa juu, jinsi Kentucky ilivyo “wajinga.” Hao akina mama wazee kule juu, wamevaa maskini kofia ya jua namna hiyo, na kuzungumza kuhusu yeye kuwa mjinga sana wala hajui ABC zake. Huenda asiwe wa tabaka la juu, bali, nawaambia, hebu mmoja wa binti zake aingie kama baadhi ya wenu usiku mmoja; nguo zimepindapinda kutoka kwake, na rangi ya midomo imejaa usoni mwake, na nywele zake zimeharibiwa jinsi hiyo. Hatasema, “Hivi ulikuwa na wakati mzuri, kipenzi?” Angenyakua kiboko kutoka kwenye kitu fulani, naye angeninii— angejua wakati wa mwisho aliotoka nje. Kisha mnauita, “ujinga.” Naam. Jambo ndilo hilo.

. . . wasio na shukrani, wasio na utakatifu,

Wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizua, wakali, na wasiopenda mema, wanawachukia watu wanaojaribu kuishi vema. (Mnaona?)

Wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu;

217 Jamani, watatumia mamilioni ya dola kwenda kwenye mchezo wa mpira, ama kitu kama hicho, ama mahali bingwa fulani wa sinema anaenda kufanya jambo fulani, ama lolote kama hilo, kama tu vile maskini zile sarakasi za Kirumi miaka mingi iliyopita. Lakini inapofikia kuvuka barabara kuhudhuria mkutano wa Roho Mtakatifu, wataketi na kucheka barazani mwao, kuucheka.

218 Vema, mnasema, “Vema, Ndugu Branham, hao ni wakomunisti.” Vema, hebu tuone kile kifungu cha 5 kisemacho.

Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake: . . .

219 Wakikana Nguvu za nini? Nguvu za Mungu. “Wenye mfano wa Mungu, bali wakikana Nguvu za Mungu.” Wakienda kanisani na kuwa wafuasi wa dhehebu, bali wakikana kuwepo kwenyewe kwa Roho Mtakatifu aliye Kanisani, akilifanya litende na kuridhika na vitu vile vile walivyofanya hapo mwanzo. Loo, jamani! Mnaona vile laana hiyo ya kimadhehebu ilivyo? Uh! natumaini hamtanikasirikia. Ila natumaini mnalipata katika nuru ninayojaribu kulisema kwake. Mnaona? Sasa angalieni hili.

*Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguzu zake:
hao nao . . .*

Yeye anasema nini kwa Kanisa? “Mjiejushe nao.” Jiejusheni nalo. Ondokeni kwake. Hiyo ni kweli.

²²⁰ Kwa kuwa, sikilizeni, hebu tusome kifungu kingine, ama viwili. Sikilizeni tu, kwa kuwa hebu tuone jinsi ambavyo watu wa namna hiyo walivyo na hakika. Tuone kama lina mashaka.

Kwa maana katika hao wamo wale wajingizao katika nyumba za watu, na kuchukua mateka wanawake wajinga wenye mizigo ya dhambi, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi,

wakijifunza siku zote, ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli.

²²¹ Kweli ni nini? Yesu Kristo ndiye Kweli. Yeye alisema, “Mimi ndimi Kweli.”

Pilato alisema, “Kweli ni nini?”

“Mimi ndimi Njia, Kweli, Uzima.”

²²² Wanawake wenye kila namna ya ma—ma—mashirika ya kina mama, na kutengeneza mablanketi, huku wakienda pamoja, na kufanya mizaha, na kuwa na chakula cha jioni na supu ya jioni wapate kumlipa mchungaji, na kadhalika namna hiyo, “Wala wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kujua Yesu Kristo yu hai leo hii katika Nguvu za kufufuka Kwake, katika Roho Mtakatifu.” Mnaona, “Kabisa!”

²²³ “Wanawake wajinga.” Sasa, yeye hakuwa akizungumza nanyi kina dada. Alisema, “Wanawake wajinga,” vema, “waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi.” Mnajua vizuri kuliko hivyo. Kwa hiyo nina furaha kwa ajili yako, dada yangu.

²²⁴ “Wasioweza.” Sauti hiyo ina mashaka jinsi gani, basi, dhehebu la kawaida. Sauti ya kanisa ni ya mashaka jinsi gani siku hizi. Ni nani ajuaye la kufanya? Hebu niwaonyeshe kanisa siku hizi. Kuna wingu la vita linaloning’inia kila mahali, matatizo kila mahali, nao watu wakiyakimbilia makanisa yao wala hawawezi kupata jibu. Nitahubiri juu ya hilo, usiku wa Krismasi, *Hakuna Jibu Kwa Ajili Ya Nyota Huko Mashariki*. Sasa angalieni. Loo, jamani! Ile pale imenging’inia, wala hawana jibu. Hawajui waseme nini. Mbona? Jambo pekee wanaloweza kurejea, “Tulijifunza hili chuoni.”

²²⁵ Kanisa halitegemei yale waliyofanya chuoni. Lakini ni Roho Mtakatifu aliye hai Kanisani, akiliongoza na kulielekeza, na kulionyesha kimbele mambo yajayo, kama alivyofanya katika siku za Tito; akiwaonya juu ya mambo yajayo, kuikimbia ghadhabu ijayo. Loo, jamani! “Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.”

226 Sasa kuna jambo lolote, basi? Ningeuliza. Sitaki kuwaweka muda mrefu kupita kiasi asubuhi ya leo. Lakini kuna kitu chochote kilicho cha hakika? Kama nimewaambia mambo mengi sana yasiyo na hakika, kuna kitu chochote kilicho hakika? Kuna uhakika wowote kuhusu chochote kamwe? Mbona, hakika, nina shukurani sana kwamba kipo. Kuna chochote kilicho cha hakika?

227 Nitawaambia kilicho hakika, hicho ni, Injili ya Yesu Kristo. Sasa, kama ukitaka kuliandika. Hatutalifungua, lakini unaweza ukitaka. Mathayo 24:35, Yesu akinena juu ya siku hizi na yale yatakayotukia. Mathayo 24:35, Yeye alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Hilo ni la hakika. Sivyo? Hilo ni jambo moja lililo hakika, ni Neno Lake. Sasa, kuna jambo moja. Tunaona hatuwezi kujenga juu ya kanisa letu. Hatuwezi kujenga juu ya taifa letu. Sisi. . . Lina mashaka mno. Lakini kuna kitu kimoja kilicho hakika, hicho ni, Neno la Mungu ni hakika. Bila shaka itakubidi kufanya hivyo.

228 Mmoja wao alisema, “Kitu kimoja cha hakika kilikuwa—kilikuwa ni kodi.” Loo, la. Kodi hazina uhakika sana. Bwana huenda akaja. Wanaweza kuitoza wakati huo. Imekwisha wakati huo.

229 Walisema, “Mauti ni ya hakika.” La, bwana. Mauti hayana uhakika. La, hashu. Huenda kukawa na Unyakuo, ndipo hakuna mauti. Mauti hayana uhakika sana. La, la, si katika siku hii. Yalikuwa, miaka mingi iliyopita, bali si sasa. Mauti hayana uhakika sana.

230 Na kwa vyovyote vile, ninamjua mtu siku moja, aliyetembea pamoja na Mungu, apate kuonyesha mfano. Ndipo siku moja akachoka kutembea, kwa hiyo akawa tu mwepesi sana akaanza kutembea juu, akapaa juu Nyumbani pamoja na Mungu. Kuna mtu anayejua huyo alikuwa ni nani? [Kusanyiko linasema, “Henoko.”—Mh.] Henoko. Naye alikuwa ni nini? Mfano wa Kanisa siku hizi.

231 Naye Nuhu, ambaye ni mfano, nasi tulikuwa na hilo juma lililopita katika somo letu. Nuhu, mfano wa Israeli waliovushwa, watakaokuwa kule juu ya Mlima wa Kugeuki Sura, hu—huko Uropa, huko chini Palestina, wakiangalia. Basi wakati wao. . . Wakati Nuhu alipoona Henoko ametoweka, aliwazia, “Henoko alipatwa na nini? Henoko alipatwa na nini? Yuko wapi?” Ambalo, alikuwa ni mjukuu. Nuhu alikuwa ni mjukuu wa Henoko. Naye akasema, “Yuko wapi? Ilikuwa kwake? Hatuwezi kumpata tena.” Nuhu akaanza kujenga safina hiyo. Alijua ya kwamba wakati ulikuwa umekaribia, papo hapo.

232 Na sasa wakati Kanisa limetwaliwa juu, nao watu waseme, “Vema, ni—ni—nimewaita polisi. Ni—nilipiga simu. Yeye alikuwa ameketi papo hapo mezani, kisha akatoweka.” Naam. “Ka—kamwe sijui alipatwa na nini.” Vema, si hayo tu. Vema, polisi

waseme, “Tuna—tumepokea simu mia tano juu ya hilo, asubuhi ya leo.” Ilikuwa je? Imekwisha basi, kwenu ninyi Mataifa. Hiyo ni kweli. Kukesha.

²³³ Neno la Mungu ni hakika. “Mbingu na nchi zitapita,” Mathayo 24:35, “lakini ahadi za Mungu haziwezi kushindwa.” Yesu alisema, “Mbingu zote na nchi zitapita.”

Mnasema, “Mbingu?” Naam. Ma- . . .

²³⁴ Ufunuo 21, Yohana alisema, “Niliona Mbingu mpya na nchi mpya, kwa kuwa mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza zimepita; wala hapakuwapo na bahari tena. Nami Yohana nikauona ule Mji Mtakatifu, Yerusalemu Mpya, ukishuka kutoka Mbinguni, kama Bibi-arusi (hivyo ndivyo ulivyokuwa) aliyepambwa kwa ajili ya mume wake.” Loo, hapo ndipo ninapotaka kuwa. Mungu anisaidie kuwa Kule siku hiyo. Vema. Ahadi za Mungu ni hakika. Tunatambua hilo.

²³⁵ Sasa hebu tuchukue tu Maandiko ma—madogo, ama ziara ndogo, na kurudi nyuma tupate mtu aliyeamini katika siku zilizopita, jinsi walivyotoka, kwa kutumainia kama Neno la Mungu lilikuwa ni sauti ya hakika. Sasa hebu turejee huko mwanzoni mwa Biblia, kwa ajili tu ya watu wawili ama watatu. Nasi tutakuwa tayari kwa mstari wa maombi, dakika kumi na tano zijazo, ama kitu fulani.

²³⁶ Sasa hebu turejee kwenye wa kwanza, na tumchukue Ndugu Nuhu, hapo mwanzoni. Nuhu, katika Mwanzo. Tunaona ya kwamba kulikuwako na sauti mbili ama tatu zilizotolewa katika siku za Nuhu. Moja ya hizo, Nuhu alisikia Sauti ya Mungu, kasema, “Itanyesha.” Sasa, Mungu. . .

²³⁷ Sikilizeni. Mungu kwa kawaida hukwambia kitu fulani ambacho ni cha kipumbavu kabisa, kwa mambo ya ulimwengu, hata inanini tu. . . Yeye hufanya hivyo kuushangaza ulimwengu. Mnaona? Wanashangaa tu niani mwao. Wanasema, “Sasa, kundi la watakatifu wanaojibingirisha, loo, masalale! Usiniambie hilo, kwamba Mungu, Mungu mtakatifu, ataishi na kundi kama hilo?”

²³⁸ Hilo ni jambo lile lile alilosema Balaki, na alilosema Balaamu, alipoangalia chini na kuwaona Israeli. Kasema, “Vema, wamefanya kila kitu ovyo kilichopata kuwapo, mstarini, wanafanya.” Ila alishindwa kuona ule Mwamba uliopigwa na yule Nyoka wa Shaba, na kuziona hizo ishara na maajabu, ya uponyaji na kadhalika, kambini. Kimsingi, walikuwa sawa tu. Lakini Mungu hufanya kitu cha kimapinduzi kabisa. Mungu ni wa kimapinduzi. Sasa hilo linasikika la kigeni, bali ndivyo Yeye alivyo. Sasa, hebu tutafute tu kujua, kwa watu wachache.

²³⁹ Hebu mwangalieni Nuhu. Sasa, Biblia inasema kwamba, katika siku za Nuhu, kamwe mvua haikuwa imewahi kunyesha kutoka mbinguni. Mungu aliitia nchi maji, huko juu kote ardhini. Haikuwa imenyeshwa. Basi huyu hapa “mlokole” huko nje, akijenga maskini mtumbwi mkubwa, yapata urefu wa

majengo mawili ya mji. Mtumbwi upate kuelea, wakati hapakuwapo na kitu chochote kwake kuelea! Hapakuwapo na maji. Hata hapakuwapo na yoyote. Kitu pekee ardhini, kitu kilichokuwa kikubwa kuliko vyote, kilikuwa ni chemchemi. “Sasa yeye anajenga kitu hicho kwa nini, akikitia lami ndani na nje, na vitu kama hivyo? Kwa nini,” wakasema “maji hayo yatatoka wapi, Nuhu?”

“Uh, kutoka *kule* juu.”

²⁴⁰ “Vema, mimi ni mwanasayansi. Nami ni—ni—ninaweza kuthibitisha, kwa hewa hii, ya kwamba—ya kwamba hakuna—hakuna maji yoyote huko juu. Kama yangekuwako, yangeshuka moja kwa moja sasa. Hakuna yoyote huko juu. Ninaweza kukuthibitishia kisayansi ya kwamba hakuna yoyote huko juu.”

²⁴¹ “Vema, lakini,” Nuhu alisema, “unajua, Mungu anaweza kuyaweka kule juu.” Jambo ndilo hilo. “Mungu alisema yangekuwa huko juu, nayo yatakuwa huko juu.”

“Vema, unafanya nini, Nuhu?”

“Ni—ninajiandaa kwa ajili yake. Mnaona? Ninajiweka tayari.”

²⁴² Vema, sasa, sayansi ilikuwa ikitoa sauti. Sayansi ilisema, “Kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha kule kwenye kile kilima kweli ni wendawazimu. Mbona, ha—hawajitambui. Vema, wana—wana—wanachonga maskini mtumbwi mkubwa huko nje. Vema, hivi kwa vyovyote watafanya nini nao? Vema, kama tungalichukua kila chemichemi ulimwenguni, na kuuweka ndani ya hayo maji, hayatatosha hata kulowesha chombo hicho kikiwa tupu. Nao hapa wanasema, ‘Utaelea. Na kwamba maji hayo yanashuka chini kutoka *huko* juu.’”

²⁴³ Lakini, Nuhu, haidhuru sayansi ilisema ilikuwa ni upumbavu jinsi gani, yeye alikuwa akiisikiliza Sauti ya hakika. Mungu alisema, “Nitauangamiza ulimwengu kwa maji.” Hakuna mashaka kulihusu. Lilisikika lisilo na uhakika wakati huo, bali lilikuwa ni Neno la Mungu, haidhuru lilisikika la kijinga namna gani.

²⁴⁴ Mungu alisema, “Mimi ni Bwana nikuponyaye.” Hakuna mashaka kuhusu hilo. Liamini hilo.

²⁴⁵ Mungu alisema, “Nitampa, kila atakaye, Roho Mtakatifu.” Yeye huja. Hakuna mashaka juu ya hilo.

Wasema, “Mimi ni mlevi. Mimi ni kahaba. Mimi. . .”

²⁴⁶ Sijali wewe u nani. “Kila atakaye, na aje.” Hakuna mashaka.

²⁴⁷ Ningependa Yeye angalisema hivyo, kuliko kusema, “Kama William Branham atakuja, katika mwaka wa 1960, nitampa chemchemi za Maji ya Uzima.” Sasa, hilo lingalikuwa ni zuri sana, inaonekana kana kwamba ilikuwa ni mimi. Lakini

huenda ikawa kuna William Branham wawili. Nisingejua ni yupi aliyekuwa mimi.

²⁴⁸ Lakini hapo aliposema “yeyote,” ninajua ya kwamba huyo alikuwa ni mimi, haidhuru, kwa hiyo mimi nilikuwa—mimi nilikuwa ndiye niliyetaka kuja. Mnaona?

Kwa hiyo, mnaona, Neno la Mungu ni la hakika.

²⁴⁹ Sasa kwa ulimwengu wa nje, ulimwengu wa kisayansi, linasikika lisilo na uhakika sana. Mnaona? Kwa sababu, kasema, “Sasa ni nani angaliweza kuwazia kamwe. . . Sasa angalieni. Ule kule mwezi usiku. Zile kule nyota. Ile kule angahewa.” Nao walikuwa ni werevu zaidi siku hiyo, mwajua, kuliko walivyo sasa.

²⁵⁰ Walijenga masfiniksi katika siku hiyo. Tungeweza kujenga leo hii? Wayo mmoja, nao unahitaji mabehewa kumi na sita, kuuweka kule juu, nayo imewekwa juu nusu jengo la mji, hewani. Tungeweza kujenga?

²⁵¹ Walijenga piramidi katika siku hizo. Wakati, hayo majabali mle ndani, yalikuwa na uzito wa maelfu ya tani. Vema, hatuna chochote ulimwenguni kingaliweza kujenga. Hatuna nguvu zozote. Petroli wala kitu kingine chochote kingaliweza kuyanyanyua kule juu. Usingeweza kuwa na mtambo mkubwa vya kutosha. Ni vipi. . . Nayo ni kamilifu sana hata. . . Hakuna saruji ndani yake. Lakini walilikata hapa sakafuni, kisha wakalinyanyua huko juu, kwa namna fulani, wala huwezi kuchukua wembe na kuendelea kukata kuikingama namna *hiyo*, yameshikana kikamilifu. Werevu kuliko tulivyo sisi sasa. Na yuyo huyo mwerevu. . .

²⁵² Walikuwa na rangi huko nyuma. Wangeweza kufanya maiti isioze katika siku hiyo. Hatuwezi kufanya moja siku hizi. Tusingeweza kuufanya mwili wa mwanadamu usioze, hatujui kile walichoweka ndani yao, kuifanya ionekane ya kawaida. Walikuwa na—walikuwa na rangi, waliyoiweka nguo katika siku hizo, tusiyo nayo sasa. Tusingeweza kufanya kitu kama hicho. Kuna mambo mengi tu waliyokuwa nayo wakati huo, ambayo hatukuwa nayo.

²⁵³ Hapa wakati fulani uliopita, walichimbua mfumo wa—wa kisasa wa ugavi wa maji, papa hapa Meksiko, ambao ulikuwa umechimbwa wakati uliotangulia ile gharika. Mfumo wa kisasa wa ugavi wa maji, ulio bora sana kuliko tulio nao siku hizi! Mnaona?

²⁵⁴ “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu,” watu werevu kama wanaofanya hivyo, “ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu,” kizazi kingine cherevu.

²⁵⁵ Jinsi hao watu walivyokuwa werevu, labda sayansi kuu zaidi, ambayo ingeweza kupima ni umbali gani kila nyota iliachana na nyingine. Walikuwa ni werevu sana mpaka, kijeografia,

waliijenga ile piramidi kubwa, kubwa vizuri, na kuiweka katikati ya dunia, hata, haijalishi jua liko wapi, kamwe hakuna ki—kivuli pande zote. Asubuhi, jioni, alasiri, popote, hakuna kivuli pande zote. Mnaona? Nimekuwa kule.

²⁵⁶ Sasa angalieni mambo haya yote waliyofanya, na nguvu walizokuwa nazo. Nawe ungeweza kuwazia, kamwe haikunyeshwa, wala hakuna kitu angani kuifanya inyeshe. Aliwezaje kamwe mtu huyo ku—kuufikisha huo ujumbe huko? Hakuweza. Hivyo tu.

²⁵⁷ Lakini kama vile Nuhu alivyosimama mlangoni pa hiyo safina, na kuwaonya watu juu ya maangamizi yajayo, ndivyo na mhubiri wa Injili aliyezaliwa mara ya pili, leo hii, amesimama Mlangoni, Kristo Yesu, amefunikwa kote na Roho Mtakatifu, akiwaonya watu juu ya maangamizi yajayo. Hakika. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, sisi hapa tumesimama katika siku hii.

²⁵⁸ Sasa, sayansi ingewezaje kusema, “Ati mvua ije kutoka *kule?*” Lakini, mnaona, Mungu alijua jinsi ya kuleta mvua kutoka kule. Ama alisababisha tetemeko la nchi, au mtu fulani alikuwa na nguvu za atomiki, ambacho walikitupa na kupasua sehemu fulani ya nchi. Ndipo ikairusha dunia nyuma, ikaitupa nje ya mzingo wake, na sasa imegemea nyuma. Basi walipofanya hivyo, joto la dunia na baridi ya duniani, kutoka kwenye jua na mbali na jua, lilisababisha wingu kuja huku. Yeye ni Yehova-yire. Yeye anaweza kujitolea Mwenyewe chochote ambacho Neno Lake lilisema.

²⁵⁹ Sasa Yeye anaweza kujipatia Mwenyewe Kanisa. Haimbidi kuwa na mimi. Haimbidi kuwa na wewe. La. Haimbidi. Haimbidi kuwa nayo. Anaweza kujipatia, mtu mwingine anaweza kuchukua mahali pako. “Kuwa mwangalifu wengine wasiichukue taji yako.” Haimbidi ku—kuwa nasi, bali inatubidi kuwa Naye. Kama ulipata kuishi, huna budi kuwa Naye, kwa sababu Yeye Ndiye pekee, kama Petro alivyosema. Wakati. . .

²⁶⁰ Yeye alisema, “Ninyi nyote mtaondoka vivyo hivyo?”

Alipofikia kuwaambia Ukweli. Yeye alikuwa ni Mtu mashuhuri wakati alipokuwa akiwaponya wagonjwa wao wote. Loo, wakati alipokuwa na ishara na maajabu zikimfuata, Yeye alikuwa ni Mtu mashuhuri. Lakini hapo alipoanza kuwaambia Ukweli, basi kulifanyika nini? Ndipo, “Akawa mlakole.” Wakamwacha.

Akawageukia wanafunzi. Kumbukeni, Yeye alikuwa huru sana, maana Yeye alikuwa ni Mungu. Akageuka, kasema, “Mnataka kuondoka, pia?”

²⁶¹ Petro akasema, “Bwana, twende kwa nani? Twende wapi? Kwa kuwa Wewe Ndiwe uliye na Maneno ya Uzima wa Milele, nasi tuna hakika na jambo hili.” Mnaona? Hakuna mashaka juu ya Hilo. “Tuna hakika ya kwamba Wewe Ndiwe uliye Nao.

Hatutupwi huku na huku na kila upepo wa fundisho. Tunajua ya kwamba Wewe una Maneno ya Uzima wa Milele, maana hakuna mtu awezaye kufanya mambo ufanyayo Wewe Mungu asipokuwa pamoja naye, hiyo ni kweli, kuwa pamoja naye.” Nikodemo alitoa tamshi lile lile.

²⁶² Sasa hebu tuseme, basi, Nuhu. Hivi ile sauti ilikuwa isiyotambulikana, ile Nuhu aliyokuwa akisikiliza? La, bwana. Ilikuwa ni ya kweli. Tulikuwa na maangamizi yaliyotangulia ile gharika, yaliyouangamiza ulimwengu wote, naye Mungu akayatuma maji jinsi tu alivyosema. Kwa nini? Ndivyo Neno la Mungu lilivyosema. Sayansi ikazama na kuangamia.

²⁶³ Angalieni, kitu kile kile kilichomwoko Nuhu, kiliwaua wakosoaji wake. Mlijua hilo? Maji yale yale. Kama kusingalikuwa na maji, Nuhu asingaliokolewa. Safina ilikuwa ndiyo iliyoelea. Kwa hiyo kitu kile kile kilichoifanya safina kuelea, kilimzamisha mkosoaji.

²⁶⁴ Naye Roho Mtakatifu yule yule leo hii, ambaye watu wanamdhihaki, Yeye ataliokoa Kanisa na kumhukumu mkosoaji. Kitu kile kile, mnaona, kitu kile kile. Kile kiokoacho, huwaua. . . Kimwokoacho mwaminio, humhukumu asiyeamini. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, mnaona, liaminini Neno la Mungu. Hilo ndilo unaloweza kusimama juu yake, na kujua kwamba ni la hakika. Kile Mungu asemacho ni cha hakika. Kiamini tu.

²⁶⁵ Sasa hebu tumchukue jamaa mwingine, katika siku za Musa. Sasa, Musa alikuwa amejaribu kupitia mpango wa elimu, alikuwa amejaribu kupitia mipango ya kijeshi, kuwaokoa Israeli, kwa sababu alijua yeye alizaliwa kufanya hivyo. Na wakati ulikuwa umewadia kwake kufanya hivyo. Lakini alijaribu kwa njia yake mwenyewe, elimu yake, na kuunda shirika lake kubwa, ama chochote kile, kufanya mapendekezo ya kijeshi kutoka kwake. Kwa maadili yake mwenyewe, alishindwa. Sasa sikilizeni kwa makini.

²⁶⁶ Lakini siku moja, Mungu alimshika, karibu na kichaka kilichowaka moto. Basi angalia jinsi—jinsi Mungu alivyomfanyia mtu huyo mambo yasiyo na busara. Sasa, Mungu alimvuta kwenye kichaka kilichowaka moto na akanena naye. Sasa, Mungu kamwe hakuwa amesema naye awali, yeye alijifunza tu kutoka kwenye kitabu. Kwa hiyo, Mungu akasema naye.

²⁶⁷ Hiyo ndiyo sababu Nuhu alijua yale aliyokuwa akizungumzia. Mungu alisema naye. Hivyo ndivyo alivyojua. Alilisia kutoka kwa Mungu. Mnaona? Ndipo sasa siku moja wakati hapakuwepo. . .

²⁶⁸ Musa, aliyefunzwa, ameadibishwa, loo, jamani, alikuwa mwanachuoni kwelikweli! Jamani! Naye alikuwa mwanajeshi kwelikweli! Basi akawazia, “Pamoja na usomi wangu wote. . . Nina Ph.D., D.D.D., L. maradufu D., na DD zote zinazoweza

kuwaziwa. Lakini, sasa, hakika nitajua jinsi ya kufanya jambo hili, kwa sababu mimi—mimi ndiye bingwa wa Misri.”

269 Sijali wewe ni bingwa wa nini, haifai kitu, inapofikia mambo ya Mungu. Ni upumbavu. Akili zako ni upumbavu, kwa Mungu. Unaona? “Kwa sababu, njia Zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo Yangu yako juu kuliko mawazo yenu, asema Mungu.” Mnaona? Kwa hiyo, akili zako zilizo bora sana . . .

270 Kama Paulo alivyosema, “Siji kwenu, nikiwahubiria maneno kwa maneno ya ufasaha, kama vile hekima ifanyavyo. Kwa sababu, kama ningalifanya hivyo, matumaini yenu yangejengwa . . .” Sasa, Paulo angeweza kufanya hivyo, maana alikuwa ni mtu mwerevu. Alisema, “Ningeweza kufanya hivyo. Lakini, jambo ni kwamba, mngetegemea falsafa ya mwanadamu. Ila nilikuja kwenu, katika nguvu za ufufuo, pamoja na Roho Mtakatifu, kusudi imani yenu iwe katika Mungu.” Haya basi. Maana, hiyo ni sauti isiyotambulikana, ndivyo ilivyo hiyo nyingine. Lakini *Hili* ni la hakika, kweli. Vema, ndipo Nuhu alikuwa . . . Samahani.

271 Musa alikuwa amejaribu, kwa sauti isiyotambulikana, maadili yake. Elimu yake, haikuwa na hakika. Bali siku moja akasikia Sauti ya uhakika. Loo! Sasa ninajisikia kubarikiwa. Naam. Yeye alisikia sauti yenye uhakika, kwa kuwa aliona Nuru imening’inia kichakani. “Vua viatu vyako, mahali uliposimama, maana ni mahali patakatifu.” Akasema, “Nimesikia kilio cha watu Wangu, nami nimelikumbuka Neno Langu.” Amina. Hakuna mashaka juu ya hilo. “Ninakumbuka yale niliyomwambia Isaka, na Yakobo, na Ibrahimu, na hao wote. Ninazikumbuka ahadi Zangu. Sizisahau. Ninaviona vilio vya hao watu, nao wakati umekaribia. Nitakutuma, Musa.”

Musa akasema, “Ninawezaje kurudi kamwe?”

272 Sikilizeni. “Bila shaka nitakuwa pamoja nawe.” Hakuna kitu kisicho na hakika kuhusu Hilo.

273 “Kama mimi pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja nawe.” Mnaona? “Nami nitakuwa pamoja nawe.” Hakuna shaka kulihusu. “Nitakuwa pamoja nawe.”

Yeye alimwambia Yoshua, miaka kadhaa baadaye, “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja nawe.”

“Nitaitekaje miji hiyo mikuu iliyozingirwa na kuta?”

274 “Mimi . . . Hilo si lako kuliwazia. Nilikuwa pamoja na Musa. Nitakuwa pamoja nawe. Na kila mahali mguu wako unapokanyaga, ni milki. Endelea tu kutembea. Mnaona? Hakuna kitu kitakachosimama mbele zako, siku zote za maisha yako.” Hakuna mashaka kuhusu hilo. “Nitakuwa pamoja nawe.”

“Hakika nitakuwa pamoja nawe,” Mungu akamwambia Musa.

275 Sasa ninawatakeni muone wakati mtu anapoisikia Sauti ya Mungu, kibinafsi anapolisikia Neno la Mungu. Sasa, unaweza kulisikia. Useme, “Vema, Mungu hana budi kuja kukutana nami.” Naam, bwana. Ningeweza kuketi hapa na kuhubiri mpaka—mpaka nianguke nife mimbarani, miaka kumi, ishirini, thelathini, hamsini tangu sasa, usingeweza kulisikia mpaka Mungu akufunulie Neno. Unaweza kuketi moja kwa moja kwenye kiti chako. Haikubidi kuwa karibu na kichaka kinachowaka moto. Labda uko karibu zaidi kuliko unavyofikiria. Keti tu hapo na umwache Mungu aseme nawe, katika Neno.

276 “Sina budi kuachana na maisha ya namna hii ninayoishi. Sina budi kuwa sawa.” Huyo ni Mungu, Mungu katika Neno Lake, akijitambulisha Mwenyewe kwako. “Ninapaswa kuyaweka maisha yangu sawa na Mungu.” Huyo ni Mungu. Huyo ni Mungu, hakika. “Sina budi kufa siku moja.” Hakika utakufa. “Sina budi kuwajibika katika ile Hukumu.” Hakika utawajibika kwenye ile Hukumu.

277 Basi hukumu yako iko wapi, huko kwenye Kiti cha Enzi ambako huna rehema, ama hapa kwenye Kiti cha Enzi ambapo unaweza kupata rehema? Sasa, ni chaguo lako. Huo hapo mti, kama vile katika bustani ya Edeni, mmoja wa Uzima na mwingine wa mauti. Ukiupuuza, Humo, unakufa. Ule sasa, upate kuishi. Sasa wewe ndiwe hakimu, unaona, wewe ndiye huna budi kufanya hivyo. Wewe ndiwe hakimu sasa, lakini Yeye ndiye Hakimu wakati huo. Wewe ndiwe hakimu sasa, kama unataka ama huutaki. Yeye ndiye Hakimu wakati huo, kama uliupokea ama la. Kwa hiyo huna budi tu kujiamulia, yale unayotaka kufanya, lakini ni juu yako. Kila mtu, kama vile Adamu na Hawa, mema na mabaya yamewekwa mbele ya kila mtu, nawe huna budi kujiamulia.

“Hakika nitakuwa pamoja nawe.”

278 “Ningewezaje kurudi na kumwambia bosi wangu ya kwamba niliokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu?”

“Hakika nitakuwa pamoja nawe.”

279 “Nitamwambiaje mume wangu kwamba nitaachana na uchoyo wangu? Nitawezaje kufanya hivyo?”

“Hakika nitakuwa pamoja nawe.”

280 “Ninawezaje kumwambia mke wangu, ya kwamba ni—niliishi vibaya, nimefanya mambo mabaya? Ningewezaje kufanya jambo hili? Ninawezaje kusimama mbele ya familia yangu tena? Watawezaje kuniamini, wakati—wakati wanajua nimelaani na kufanya yasiyofaa, na kufanya mambo yale niliyofanya, kisha nirudi niwaambie ‘mimi ni Mkristo?’”

“Hakika nitakuwa pamoja nawe,” alisema Mungu.

281 Itakufanya ufanye mambo usingeyawazia. Mwangalie Musa, jinsi ilivyomfanya atende kimapinduzi. Alifanya nini? Mtu huyo; umri wa miaka themanini. . .

282 Mnasema, “Vema, Ndugu Branham, mimi—mimi ninaingia kwenye umri wa makamu, mzee. Ama. . .” Sijali una umri mkubwa jinsi gani. Hilo halina uhusiano wowote. Ile siku ambayo Mungu angeweza kukutuliza vya kutosha kusema nawe, nawe unaweza kulisikia Neno Lake, hiyo ndiyo siku Yeye anasema nawe, haijalishi una umri gani. “Ninawezaje kufanya hilo, Ndugu Branham?”

283 Mwangalie Musa, umri wa miaka themanini. Misri ilikuwa imeushinda ulimwengu wote. Walishikilia kila, siri zao zote za kijeshi na kila kitu mkononi mwao. Ndipo Musa akamweka mke wake kutagaa maskini nyumbu, akamweka Gerishomu pajani mwake. Naye huyu hapa anaenda, kesho yake asubuhi, akiwa na fimbo iliyopinda mkononi mwake, masharubu meupe yakining’inia chini namna *hii*, na labda kichwa chake chenye upara kiking’aa, namna hiyo. Naye maskini nyumbu huyu akishuka kupitia pale, akimvuta maskini nyumbu huyu. Yeye alikuwa akipiga makelele, “Utukufu kwa Mungu! Bwana asifiwe!”

Mtu fulani aseme, “Musa, unaenda wapi?”

284 “Ninashuka kwenda Misri, kukiteka kitu hicho.”

“Ni mzaha jinsi gani!”

285 Lakini wakati mtu anapozugumza na Mungu, naye anayo Sauti ya Mungu ndani yake, na Neno la Mungu ndani yake! “Mkikaa ndani Yangu,” Yohana 15. “Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu; mnaweza kuomba mtakalo, nanyi mtatendewa.” Mnaona? Hakuna chenye mashaka. Litatendwa. Hiyu ni kweli. Hamna mashaka.

286 Musa, “Utawezaje Wewe. . .” Huenda Musa alimwambia Mungu, “Nitafanyaje jambo hilo, utakuwa ni uvamizi wa mtu mmoja? Ninawezaje mimi, mzee hapa, umri wa miaka themanini, basi nitaendaje kule chini kwenye hilo jeshi kuu mno la mamilioni ya watu, na kuliteka?”

287 “Hakika nitakuwa pamoja nawe.” Hayo tu ndiyo yaliyompasa kujua. Huyu hapa anaenda. Huyu hapa anaenda. Anateremka chini. Naye akaiteka, pia. Kwa nini? Alikuwa na hakika ya kwamba ile Sauti aliyoisikia ilikuwa ni ya kweli.

288 Nayo Sauti unayoisikia asubuhi ya leo ni ya kweli, kwa sababu ni Neno la Mungu.

289 Wana wa Kiebrania kwenye ile tanuru iliyowaka moto, walijua je ya kwamba wangekombolewa? Wao walisema, “Mungu wetu anaweza kutukomboha.” Yeye hakuwa amefanya hivyo hapo kabla. “Anaweza kutukomboha na tanuru hii ya moto. Lakini, hata hivyo, tuna hakika ya kwamba Yeye anaweza.” Hakuna

mashaka kuhusu hilo. “Tulijua tu mapenzi Yake, bali, hata hivyo, hatuisujudii sanamu yako.”

290 “Hatutahudhuria karamu hiyo. Hatutavuta hizo sigara. Hatutakunywa pombe hiyo. Hatutasema huo uongo. Hatutafanya uzinzi. Hatutawakimbia wake zetu tena, waume zetu tena. Tuna hakika, Mungu anaweza kutukomboa.”

291 “Vema, ukifanya hivyo, watakufukuza kwenye mchezo wa karata. Watakufukuza kwenye karamu ya kamari, msaada wa kina mama.”

“Sijali watakayonifanyia. Mungu anaweza kunikomboa.”

292 “Unajua watakayofanya? Watakuita wa mtindo wa kale. Acha nywele zako zikue tena, kama ukifanya hivyo. Kisha uvae hizo nguo ndefu na kutenda kama mama wa heshima. Unajua watakayofanya? Watakuita wa mtindo wa kale.”

293 “Sijali yale wafanyayo. Bali Mungu anaweza kunikomboa, na hilo ndilo jambo ninalotafuta leo hii. Mungu anaweza kunikomboa. Hivyo tu.”

294 “Vema, kama hutavaa kaptura msimu huu ujao wa kiangazi, Susie atasema nini?”

295 “Sijali Susie atasema nini. Ninataka kujua yale Mungu asemayo. Kwa sababu, Susie ana sauti isiyotambulikana. Lakini Mungu anasema kweli. Hiyo ni Sauti ya hakika.” Kwa hiyo, kweli Yeye aliwakomboa.

296 Ibrahimu alikuwa na uhakika jinsi gani, baada ya kungojea kwa muda wa miaka ishirini na mitano, kwa ajili ya mtoto mchanga ambaye Mungu alimwambia ya kwamba angempata? Ungeweza kuwazia, Ibrahimu, mzee, mwenye sifa nzuri miongoni mwa watu? Ndipo siku moja, Mungu akanena naye, kasema, “Ibrahimu, nitakufanya ‘baba wa mataifa,’ nitalibadilisha jina lako sasa, na kukuita Ibrahimu, kutoka kwa Abram u likawa Ibrahimu. Nami nitamwita, kutoka Sarai (S-a-r-a-i) kuwa S-a-r-a ‘binti mfalme,’ nami nitalibadilisha jina lake. Na sasa nyote wawili. . . Hebu tuone, Ibrahimu, wewe una umri wa miaka sabini na mitano, naye yuna sitini na mitano. Umekuwa ukiishi naye tangu alipokuwa na yapata umri wa miaka kumi na sita, kumi na saba, maana yeye ni dada yako wa kambo. Nawe umekuwa ukiishi naye muda huu wote. Ulimwoa wakati alipokuwa tu msichana mdogo, na hata hivyo bado hujapata watoto wowote. Lakini ni—nitafanya hivyo. Uh-huh. Nitakupa mtoto mchanga. Basi unaniamini Mimi, Ibrahimu?”

“Naam, Bwana, ninakuamini.”

“Vema, sasa, wao—watasema una ‘kichaa.’”

“Loo, hilo ni sawa, Bwana. Ni sawa.”

“Waambie utampata mtoto.”

297 Vema, anaenda huko na kumshika Sara upesi, kasema, “Kipenzi, wajua nini? Tutapata mtoto mchanga.”

“Ati nini? Ati mtoto mchanga?”

“Naam.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo.”

298 “Amina. Hiyo ni kweli, basi kipenzi, tutampata. Vema, sasa, unajua nitakalofanya? Nipe pesa kidogo. Ninashuka, nikanunue vijibuti. Nitanutua jichondege na vipini. Nasi tutajiandaa kwa ajili ya mtoto huyu mchanga, unaona, maana anakuja sasa hivi. Naam, bwana.” Basi huyo akaenda dukani.

299 Nami ninawasikia wakishuka kwenda kwa daktari, na kusema, “Daktari, wajua nini? Ninataka uweke nafasi hospitalini. Tutampata mtoto mchanga.”

300 “Uhu, uhu, uhu, uhu, uhu! Hum! Uhu, wewe, ati ulisema jina lako ni nani?”

“Ibrahimu.”

301 “Uh-huh. Naam. Naam, bwana. Samahani. Nina haraka leo, unaona.”

302 Anarudi, kasema, “Aisee, afadhali ukawaite wataalamu, wamfanyie mzee huyo uchunguzi wa akili. Mbona, yeye yuna umri wa miaka sabini na mitano, naye yule mwanamke mkongwe anayeketi pale huku akiwa na maskini shuka moja mgongoni mwake, kama maskini nyanya, na kusema atajifungua mtoto. Mbona, huyo si—huyo si ni mwana wa Tera huko chini, aliyeshuka kutoka huko Shinari, huko kwenye ule mnara? Huyo—huyo si yule. . . Huyo si ni mwanawe?”

“Naam.”

303 “Vema, maskini jamaa huyo mzee alitoka nje kwenye jua kali kupita kiasi. Ameathiriwa na jua kali. Kidogo ana kichaa. Mnaona? Naam.” Lakini hiyo ni sauti isiyotambulikana.

Ila Ibrahimu alikuwa na Sauti ya hakika, “Mungu alisema hivyo.”

304 “Vema,” viongozi wanasema, “amekuwa ni mzee mwaminifu. Ninajua mara nyingi, yeye huwapa vitu wajane. Naye anatoa vitu. Wao—wao. . . Naye mke ni mkarimu sana. Sitaki kuwafunga, wala chochote kile. Hebu tusiwaweke kule nje kuuegemea ule mti, katika hizo pingu na vitu kama hivyo, wangeathirika zaidi. Hebu niwaambie, tutawaangalia tu, mwajua.” Nao wakaendelea kuwaangalia. “Uh-huh? Uh-huh?” Ni sauti isiyotambulikana jinsi gani!

305 Lakini Ibrahimu alijua Sauti hiyo ilikuwa ni ya hakika. Kwa hiyo akasema, mwezi wa kwanza ukapita, “Unajisikiaje, kipenzi, tofauti yoyote?” Sasa kumbukeni, ninyi kina mama; zile siku ishirini na nane, alikuwa amezipita muda mrefu uliopita,

yapata umri wa miaka arobaini. Naye huyu hapa, umri wa miaka sitini na mitano. “Unajisikiaje, kipenzi?”

“Vema, kipenzi, hakuna tofauti yoyote.”

³⁰⁶ “Utukufu kwa Mungu, tutampata, haidhuru.” Hakuna mashaka. “Hakika. Nina hakika. Naam, bwana. Nina hakika tutampata.”

“Unajuaje, Ibrahimu, utampata?”

“Mungu alisema hivyo. Nitampata, kwa vyovyote vile.”

³⁰⁷ Vema, mwezi wa pili, mwezi wa tatu, mwaka wa kwanza, “Unajisikia tofauti yoyote, kipenzi?”

“La.”

“Hakuna kitu kilichotukia bado?”

“La. La.”

“Vema, utukufu kwa Mungu! Tutampata, kwa vyovyote vile.”

³⁰⁸ “Ibrahimu, nilisikia ya kwamba ulisema utakuwa na mtoto mchanga. Hee-hee! Hee-hee!” Hiyo ni sauti isiyotambulikana. Mnaona?

³⁰⁹ Lakini Ibrahimu alikuwa tayari amesikia Sauti nyingine iliyoyazamisha hayo yote kabisa. “Utukufu kwa Mungu. Sijali Yeye atangojea muda gani. Nitampata, kwa vyovyote vile.”

“Unajuaje, Ibrahimu?”

“Mungu alisema hivyo.”

“Sasa, Yeye, hivi Mungu alishuka na kusema nawe?”

“Naam.”

“Unajuaje? Hebu nimsikie?”

³¹⁰ “Alisema nami, sio na wewe. Vema, endelea.” Kasema, “Endelea, ewe maskini asiyeamini. Huamini, kwa vyovyote vile. Ninamwamini Yeye, unaona, kwa hiyo endelea tu kusonga mbele.” Jambo ndilo hilo. “Nitampata mtoto, kwa vyovyote vile.” Miaka ishirini na mitano ikapita.

³¹¹ Lakini kabla wakati huo haujawadia, walikuwa wakiwatania na kuwachekeka. Mungu akasema, “Wajua nini? Nitakuondosha tu kwao. Panga nguo zako zote na kadhalika, jiweke tayari. Toka, jitenge na kundi hilo la wasioamini. Nitakupa kanisa dogo huku, watu wengine watakuamini. Toka kwenye maskini madhehebu hayo baridi, ya kawaida. Njoo huku nje. Tembea pamoja na Mimi, peke yako.” Mungu kamwe hakumbariki mpaka alipofanya hivyo kabisa, akajitenga na kutokuamini kwote.

³¹² Wala Yeye kamwe hatakuabariki mpaka utakapofanya vivyo hivyo. Ondoa ushirikina huo wote wa kale kwako, na, “Labda ndivyo ilivyo, na labda sivyo.”

Kama umekuja kuombewa, asubuhi ya leo, njoo na imani halisi, “Mungu alisema hivyo, na hilo latosha.” Jambo ndilo hilo. “Mungu alisema hivyo.” Hakuna lingine. “Mungu alisema hivyo.” Yeye alilisema, na hilo—hilo latosha. Usiwe na mahangaiko tena kulihusu, kuwazia. Vema.

³¹³ Sasa, baada ya miaka ishirini na mitano, naye Ibrahimu alikuwa amezeeka sasa. Alikuwa na umri wa miaka mia moja. Naye Sara alikuwa na umri wa miaka tisini. Sasa waziini hilo, maskini nyanya, shuka dogo mgongoni mwake, kijikofia kidogo cha vumbi. Naye babu, mwajua, namna *hii*. “Basi unajisikiaje, kipenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Nitampata, kwa vyovyote vile. Utukufu kwa Mungu!”

³¹⁴ Siku moja ilitokea kwamba aliangalia, nao hawa hapa Watu watatu wakaja wakitembea. Wakaketi chini. Wawili wao wakashuka kwenda Sodoma, kuhubiri.

³¹⁵ Akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Loo, jamani! Whiu! Sasa kumbuka, Yesu alisema hilo lingetukia tena, mwajua, Malaika yule yule.

Yeye alitambua walikuwa ni Malaika. Mnaona? Alikuwa ameisikia Sauti hiyo. Wakati alipomsikia Mtu huyo akizungumza, kulikuwako na kitu fulani kumhusu huyo, ambacho alikitambua, kwamba hiyo ilikuwa ni Sauti ile ile. Mnaona? Yeye alijua huyo alikuwa ni Mtu yule yule.

³¹⁶ Akasema, “Sara?” Akaingia kisiri, kasema, “Kipenzi, toka huko nje haraka sana, ukapanguse meko upesi sana, na ubingirishe baadhi, ukande baadhi, chukua kabari uiweke kwenye ile chekeche ya kale.” Mnazikumbuka hizo? “Chekecha unga kidogo.”

³¹⁷ Ni wangapi wenu, ninyi Wakentaki, wanaokikumbuka hicho? Vema, jamani, mnapaswa kukumbuka. Nimemwona mama akichukua kitu hicho cha kale na kukipiga, “bum, bum, bum,” na kukisugua, na kukisugua, kisha “bum, bum, bum,” akiutikisa huo unga utoke, apate kutuokea keki jembe. Ha—halafu basi kuchemsha maskini ngozi hizo za nyama, kwenye kikaango, mwajua, ama kiokamikate, na kukitia mafuta. Na njugu jicho nyeusi na majani ya tanipu, chakula kizuri sana. Kwa hiyo basi—kwa hiyo basi wakati sida ilipokuwa ngumu, na kutengeneza siki, mwajua; na kuondoa kuvu yote juu yake, akaitia siki kidogo. Ni nzuri. Kwa hiyo basi—basi. . .

³¹⁸ Ninamwona Sara akioka hizi keki jembe, huko nje juu ya jiwe hili, hivyo. Ibrahimu akatoka, akatafuta kuona ni wapi angempata maskini ndama mnono; akamchinja, akamleta, akamtengeneza.

³¹⁹ Akatoka huko nje, kasema, “Kuna kitu kuhusu Mtu huyo. Nimeisikia Sauti hiyo awali. Ninajua yuna mavumbi nguoni

mwake mwote, na kadhalika. Ameketi pale, akiupangusa uso Wake, na kuangalia huku na huku namna hiyo. Lakini ninawaambia, ninaijua Sauti hiyo, maana si sauti isiyotambulikana. Maana, niliisikia, miaka ishirini na mitano iliyopita. Na, kipenzi, tumetumainiwa muda huu wote, kuamini. Na kuna kitu fulani kuhusu Mtu huyo. Sijui ni kwa nini, bali kuna jambo fulani kumhusu Yeye, ninaamini.” Vema.

³²⁰ Kwa hiyo wakati alipotoka, naye akachukua kifukuza nzi na kuwafukuza nzi wote, mwajua, kisha akaketi pale wakati Wao wanakula. Kwa hiyo basi, baada ya kitambo kidogo, wawili wa Hao wakaanza kuangalia huko chini Sodoma. Na Wao wakateremka kule, mhubiri wa kisasa akashuka kule kuwahubiria Injili basi.

³²¹ Kwa hiyo Ibrahimu alikuwa ameketi pale pamoja na Mtu huyu, naye alikuwa ameuelekeza mgongo Wake kwenye hema. Akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

Kasema, “Yuko hemani, nyuma Yako.”

³²² Kasema, “Kulingana na wakati wa uhai, nitakurudia sawasawa na ile ahadi niliyokuahidi.” Yeye alijua Sauti hiyo ilikuwa ya hakika basi.

³²³ Nini kilichotukia? Mara baada ya huyo Malaika kuondoka, Sara akawa kijana mwanamke, mrembo, akarejeshwa moja kwa moja, ikionyesha yale atakayomfanyia kila Uzao wa Ibrahimu. Maskini nyanya huyo akawa mwanamke kijana. Naye Ibrahimu, kinundu kikatoweka mgongoni mwake, na ndevu nyeupe zikatoweka, naye akawa kijana mwanamume tena.

³²⁴ Ndipo wakafanya safari ndogo, maili mia tatu, kule chini Gerari. Ndipo walipofika kule chini, Abimeleki, mfalme wa Wafilisti kule chini, alikuwa akitafuta mke. Ndipo akaangalia kote, hao wanawake warembo wa Kifilisti. Ambao, wao ni warembo. Na kwa hiyo akaangalia huko, akawaona hao wanawake wote wa Kifilisti, kasema, “Kamwe siwezi kumchagua mmoja, kwa njia moja ama nyingine. Mimi kamwe...” Siku moja alimwona maskini Sara akishuka kuja sasa, mwenye umri wa miaka mia moja, maskini nyanya. Akasema, “Huyo ndiye niliyemngojea. Huyo hapo. Huyo ndiye.” Kwa hiyo, akamchukua naye alikuwa akitaka kumwoa.

³²⁵ Ndipo Mungu akamtokea, katika ndoto, kasema, “Ati unamchukua?” Kasema, “Huyo ni mke wa nabii Wangu.” Kasema, “Wewe ni kama mtu aliyekufa.”

Akasema, “Bwana, Wewe unajua uaminifu.”

³²⁶ Hakuna mashaka kuhusu hilo. Akasema, “Mrudishe. Sitasikia maombi yoyote unayoniomba. Sitasikia chochote kuyahusu. Kwa sababu, yeye ni nabii, basi mrudishe na umrejeshe. Maana, mimi...” Alihitaji pesa kidogo, hiyo ndiyo sababu haya yote yalitukia. Kwa hiyo, walihitaji pesa

kidogo. “Kwa hiyo nenda huko ukamrudishe, mke wake kwake. Usipomrudisha, wewe ni kama mtu aliyekufa.” Hakuna kitu chenye mashaka kuhusu hilo, maana Mungu alikuwa amefunga kila tumbo la uzazi la kila kitu alichokuwa nacho. Hiyo ni kweli kabisa.

³²⁷ Akaenda huko nje, na kusema, “Ibrahimu, kwa nini ukafanya hivi?”

³²⁸ Kasema, “Mbona, yeye ni dada yangu, kama nilivyokwambia alikuwa. Lakini,” kasema, “yeye akawa mke wangu.”

³²⁹ Halafu, akaendelea. Sasa yeye alikuwa ni nani? Ndipo wakati mtoto huyo mchanga alipozaliwa, baada ya miaka hii yote, walipogeuka tena. Mungu alisema, siku moja, kasema, “Mpeleke mlimani, ukakate shingo yake.” Loo, jamani!

³³⁰ Mwanzo 22, yeye alimpeleka maskini mtoto huyu mdogo kule juu. Naye akamchukua mtoto Isaka, loo, hakuwa ni mtoto mchanga, alikuwa na yapata umri wa miaka kumi na minne, akarudisha nyuma nywele zake za matimutimu namna *hiyo*. Ndipo akachomoa kisu, maskini mkono huo unaotetemeka wa baba huyo mzee; hapana shaka, akimeza kwa shida, ikikaba roho, mwajua. “Mwanangu wa pekee. Nimengojea miaka hii yote. Jamani! Kamwe sijapata kuwa na mvulana. Mwangalie. Mwangalie. Huyu, yeye ni mwanangu wa pekee, maskini jamaa huyu mdogo. Lakini, Mungu, uliniambia nifanye hivyo. Ninajua kulitumainia Neno Lako. Sijui jinsi utakavyolifanya. Lakini, Bwana, ulimkabidhi kwangu, kama aliyetoka mautini.”

³³¹ Sasa, kama mkitaka kuandika hilo, Waebrania 11:17 hadi 19. Hebu tulifungue tu, kisha tatalipata tu. Waebrania 11, saba-... hadi 19. Tuko karibu kufunga, katika dakika moja tu. 11:17, vema.

Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu: na yeye . . . aliyepokea hizo ahadi alikuwa akimtoa . . . aliyepokea hiyo ahadi alimtoa mwanawe, mzaliwa pekee.

Naam, yeye aliyeambiwa, Katika Isaka uzao wako utaitwa:

“Akihesabu” . . . Kifungu cha 19.

Akihesabu ya kuwa Mungu aliweza kumfufua hata kutoka kwa wafu; akampata tena toka huko kwa . . . mfano.

³³² Ibrahimu alisema, “Bwana, kama ukipata . . . Huko nyuma wakati nilipokuwa mgumba, sikuwa na kitu. Nilikuwa mwenye dhambi, na Wewe ukanifanya kitu fulani. Ulinipa ahadi. Nayo hii hapa, Wewe ulinipa mvulana huyu. Nami nilimngojea miaka ishirini na mitano kuja. Na sasa, miaka kumi na minne baadaye, mbona, huyu hapa, kijana mwanamume, kipenzi tu cha moyo wa mamaye. Nilimchukua kisiri kutoka nyumbani.

Kuweka . . . Mama asingeelewa. Bali mimi ninakuelewa, Bwana, ninajua ya kwamba Sauti Yako ni ya kweli. Sasa uliniambia nimtoe dhahihu, nimwue. Nawe uliniambia, kwamba, kupitia kwangu, mimi, ningekuwa baba wa mataifa mengi. Kupitia kwa mvulana huyu, kwamba ungemchukua mvulana huyu, na kupitia kwake. . . Wakati uliponifanyia ile ahadi, na kukatakata vile vipande vya nyama, siku hiyo, nayo ile Nuru ndogo nyeupe ikapitia katikati yake, Wewe ulinipa ahadi, ya kwamba, kulingana na mtoto huyu hapa, ya kwamba ungemwinua Mwanao Mwenyewe. Amina. Wewe ungemleta Mwanao Mwenyewe. Kupitia kwa uzao wa mwanangu, Wewe ungemleta Mwanao, Naye ataliokoa taifa lote. Sijui jinsi utakavyofanya hilo, Bwana. Sio kazi yangu. Lakini ninajua uhakika wa hilo. Ninajua uhakika wa ahadi Yako, nami nimeshawishika ya kwamba nilimpokea kama mmoja kutoka kwa wafu. Nami nimeshawishika kabisa ya kwamba Wewe unaweza kumfufua katika wafu. Kama nikimwua, Wewe unaweza kumfufua tena. Nitaliamini Neno Lako, Bwana.”

³³³ Akachomoa kisu. Kasema, “Kwaheri, Isaka.” Akambusu. Akavuta nyuma.

³³⁴ Ndipo Mungu akasema, “Ngoja kidogo, Ibrahimu. Ngoja kidogo. Ninajua unaniamini Mimi. Ninajua unanipenda. Ondoa mkono wako.”

³³⁵ Yapata wakati huo, yeye akasikia kitu fulani nyuma yake. Akaangalia, na huyo hapo kondoo dume ameshikwa kwenye vichaka. Huyu kondoo dume alitoka wapi? Alitoka wapi? Yeye alikuwa maili mia moja kutoka kwenye ustaarabu, huko nyuma nyikani ambako kuna simba, mbwa mwitu, mbweha, na vitu hivyo vyote namna hiyo, ambavyo huwaua kondoo. Halafu alikuwa huko juu sana mlimani, ambako hakuna maji wala chochote kile huko juu kwa ajili ya kondoo kuishia. Wala hakuwako pale, dakika moja kabla ya hapo. Akaangalia nyuma, naye huyo hapo, dakika nyingine moja, pale. Yehova-yire! Mungu alisema. . .

³³⁶ Ibrahimu akaangalia juu, kasema, “Wewe ni Yehova-yire.” *Yehova-yire* linamaanisha nini? “Unaweza kutoa chochote unachosema. Kama ulisema hivyo, hilo latosha. Unaweza kulifanikisha.”

³³⁷ Yeye. . . Yeye alifanya nini? Ilimbidi kusikia sauti ile ile ambayo Nuhu alisikia. Wakati, “Yeye atapataje maji huko juu angani?”

³³⁸ “Sijui. Lakini, Yeye ni Yehova-yire. Anaweza kuweka maji kule juu.”

³³⁹ “Yeye atamwinuaje mtu kutoka ardhini na kumpeleka Utukufuni?” Siwezi kuwaambia. “Sisi ni wazito. Nina uzito wa ratili mia moja na hamsini. Nina uzito wa ratili mia mbili.” Sijali una uzito gani. Yeye ni Yehova-yire. “Usafiri unaendaje?”

Siwezi kukwambia, bali Yeye atawasafirisha kule wakati huo utakapowadia.

Niseme hili kwa niaba ya marafiki zangu weusi wanaoketi hapa, asubuhi ya leo. Huko chini Kusini kulikuwako na mzee mweusi aliyebeba Biblia yake kila mahali. Akasema...Ndipo bosi wake alikuwa akimtania, kwa kuwa alisema alikuwa na dini ya moyoni. Akasema, "Hakuna kitu kama dini ya moyoni."

Akasema, "Bosi, umepungukiwa na jambo moja." Kasema, "Hakuna kitu kama dini ya moyoni, kadiri ujuavyo." Mnaona? Lakini yeye alijua vinginevyo.

Kasema, "Unafanya nini na hiyo Biblia? Huwezi kuisoma."

³⁴⁰ Kasema, "Ninaiamini." Kasema, "Ninaiamini, kutoka chalada hadi chalada, na ninaiamini chalada, pia. Kwa sababu," akasema, "maana imeandikwa 'Biblia Takatifu' juu Yake."

Kasema, "Nadhani unaamini hadithi hizo zote Mle?"

³⁴¹ Kasema, "Naam, bwana." Kasema, "Ninaamini kila kitu ambacho Mungu alisema. Na kila kitu Mungu anachoniambia, ninaiamini."

³⁴² Akasema, "Sasa, sasa sikiliza, Sambo, huwezi kufanya hivyo." Kasema, "Sasa vipi kama Mungu akikwambia uruke kupitia kwenye ukuta ule wa mawe kule, ungefanya nini?"

Akasema, "Naam, bwana. Ningeruka moja kwa moja kupitia kwenye ule ukuta wa mawe."

³⁴³ Akasema, "Utapitiaje kwenye ukuta huo wa mawe, pasipo na shimo ndani yake?"

³⁴⁴ Kasema, "Kama Mungu aliniambia 'ruka,' Yeye angekuwa na shimo nifikika pale." Kwa hiyo hilo ni karibu sawa. Hiyo ni kweli.

³⁴⁵ Mungu atalidumisha Neno Lake. Hakuna kutokuwa na hakika juu ya hilo. Wakati Parapanda ya Mungu inapolia maskioni mwako, ile Parapanda ya Injili, hiyo ni ya hakika. Amina. Dumu papa hapa pamoja Nayo. Loo, loo, ni ya hakika!

³⁴⁶ Mbona watu hawa wote sasa...Nasi tunapitisha wakati; tamko jingine moja tu, ama Maandiko mawili hapa, nimeyaandika, nafikiri. Ni kwa nini watu hawa wote wakafanya hivi? Kwa sababu walikuwa wameisikia Sauti ya Mungu. Sasa, upesi sana sasa, kumalizia, katika yapata dakika tatu ama nne.

³⁴⁷ Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Nina nguvu za kuweka uhai Wangu chini. Nina nguvu za kuutwaa tena." Sasa, hapakuwepo na mashaka yoyote kuhusu hilo. "Ninazo." Sio "Nitakuwa nazo." Lakini, "Ninazo sasa. Ninazo nguvu za kulaza maisha Yangu chini. Ninazo nguvu za kuyatwaa tena." Vema.

348 Martha, akiisha kumpoteza ndugu yake, Lazaro, alimsikia Yeye akisema, “Nitaenda nikamwamshe.” Kasema, “Mmemzika wapi?” Sasa Yeye. . .

349 Aliagizia, kasema, “Yesu, njoo ukamponye ndugu yangu. Yeye ni mgonjwa.” Yesu hakumsikiliza hata kidogo; naye akaenda zake. Akaagizia tena, yeye na Mariamu. Nao wakaendelea, hakujali hilo.

350 Ndipo, baada ya kitambo kidogo, Lazaro akafa, wakamlaza kaburini. Alikuwa ananuka, alikuwa amelala mle siku nne. Pua tayari ilikuwa imebonyea ndani; funza ndani yake, kila kitu, amefungwa katika nguo hizi na kadhalika. Jiwe limewekwa juu ya kaburi, kama vile wanavyowazika wafu katika mashariki. Una shimo tu, kisha unaweka jiwe juu yake. Hilo lilikuwa ndilo kaburi.

351 Kwa hiyo wakasema, na muda si muda wajua, kasema, “Yesu amekuja.” Na kwa hiyo Martha akavaa shuka lake, naye akashuka mtaani, msichana huyu mdogo, mrembo. Akakimbia kule chini. Akasema, “Bwana.” Angalia ule msogeo. Alikuwa ameisikia Sauti, siku moja, nayo ilikuwa ya hakika. Alijua ya kwamba kuna jambo fulani kumhusu Yeye. Akasema. . .

352 Sasa vipi kama angalienda na kusema, “Tulitoka kwenye dhehebu letu kwa sababu Wewe ulihubiri dhidi yake. Nasi tulifanya yote haya kwa sababu ulifanya *hivi-na-hivi*. Nasi tulikuamini. Sasa sisi ndio—sisi ndio gumzo la mji. Kila mtu anasema, ‘Yuko wapi Mchungaji wenu mtakatifu anayejibingirisha sasa? Mnaona? Kuna haja fulani. Yuko wapi? Alitoroka. Mnaona? Yuko wapi? Wako wapi hao waponyaji wa Kiungu?’”

353 Kumbukeni hilo lilisemwa nawe, Ndugu Wright, huko chini, na wahubiri wenu wa Church of Christ na hao wengine. Naam, bwana.

354 “Kwani wako wapi? Ati wapi? Haya yote ni ya nini? Vipii kuhusu hilo sasa, mnaona?”

355 Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, ilionekana kana kwamba alikuwa na haki ya kumkemea, kasema, “Kwa nini hukuja wakati nilipokuita?” Lakini, unaona, hiyo siyo njia ya kumwenda Mungu.

356 Usiulize swali. Jua hiyo Sauti ni ya hakika. Alienda moja kwa moja kule, kasema, “Naam, Bwana.”

357 “Bwana, kama—kama wakiniwekea mikono, ninajuaje nitapona?” Si kazi yako. Unaona?

358 Jambo pekee unalopaswa kufanya, ni kujua tu hiyo Sauti ya hakika kwamba, “Mungu alisema hivyo.” Liamini na uendele. Mungu alisema hivyo. Unaona? Naam, bwana. Ni Neno la Mungu.

359 Sasa, basi, jambo la kwanza mwajua, vema, maskini Martha akaja akikimbia huko nje. Naye akasema, “Bwana.” Loo, napenda hilo! Mnaona, yeye alimpa sifa zilizo Zake. Alikuwa ni nanii wake. . . “Bwana, Kama Wewe ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa.” Mnaona? Kasema, “Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Hakuna mashaka kuhusu hilo. La. Mnaona? Mnaona?

360 Hapa ni wakati wawili wa kweli wanapokutana. Mnaona? Hapo ni wakati wawili wenye nguvu zote wanapokutana. Mnaona? Wakati, mmoja mwenye nguvu zote aliyekuwa naye, yeye alikuwa na imani yenye nguvu katika Kristo; naye Kristo alikuwa mwenye nguvu zote. Mnaona? Alikuwa na imani kamilifu, imani isiyu na kikomo katika Kristo, kwamba Yeye alikuwa ni Bwana; naye alijua, lolote alilomwomba Mungu, Mungu angempa Yeye. Kwa maneno mengine, alisema, “Nena tu Neno, hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya. Lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

Huko ni kuwa na ngu- . . . Hiyo—hiyo ni kuwa na nguvu zote, kuwa na uweza wote, maana Yeye ndiyo kwanza aseme hivyo. Mnaona? Vema, na Yeye alikuwa na uweza wote. Hapo ni wakati nguvu mbili, nguvu mbili zenye nguvu zote, zinapokutana. Ni mkutano basi.

361 Wakati waya hapa *una* volti mia moja na hamsini, nayo *hii* ina volti mia moja na hamsini; zinapounganishwa, una volti mia moja na hamsini, pande zote mbili. Unaona?

362 Basi wakati ukiwa na Nguvu kuu sana, wakati Yesu aliposema, “Wekeni mikono juu ya wagonjwa, watapata afya,” nawe una imani kubwa sana kwamba hiyo ni Kweli, unahitaji Mungu mkuu aliyetoa ahadi kuu, ndipo matokeo makuu sana yatatokea. Amina. Jambo ndilo hilo. Mnaona?

363 Sasa mwangalieni. Yeye alikuja, akasema, “Bwana, kama ungalikuwako hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa Wewe.”

Akasema, “Ndugu yako atafufuka tena.”

364 Akasema, “Hakika, Bwana, yeye atafufuka katika siku za—siku za mwisho.” Kwa nini? Yeye alikuwa amelisikia Neno hilo. Yeye alijua hiyo ilikuwa ni Sauti ya hakika. “Hakika, Bwana, yeye atafufuka katika siku za mwisho. Alikuwa ni mvulana mzuri. Atakuja katika ule ufufuo wa kياما, katika siku za mwisho.”

365 Yesu akasema, “Mimi Ndimi.” Hakuna mashaka kuhusu hilo. “Mimi Ndimi vyote viwili, ufufuo na Uzima.” Huh! Whiu! “Mimi ndimi ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Yeye aliye hai na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe.” Hakuna mashaka kuhusu hilo. “Unasadiki haya?”

366 Akasema, “Naam, Bwana. Ninaamini ya kwamba Wewe ni vile vile hasa ulivyosema ulikuwa. Wewe ni Mwana wa Mungu ajaye ulimwenguni, apate kutuokoa. Nami ninaamini ya kwamba lolote ufanyalo, au kusema, ni kamilifu tu. Hakuna mashaka kukuhusu Wewe, hata kidogo.”

“Mmemlaza wapi? Nitaenda nikamwamshe.”

367 Sasa, sio—sio, “Nitaenda nione kama ninaweza, nitaenda nijaribu, nitaenda nione yale ninayoweza kufanya kulihusu.” La, hakuna mashaka. “Nitaenda nikamwamshe.”

368 Kwa nini? Baba alikuwa amemwambia, Naye alikuwa na ahadi ya Mungu, ambayo ilikuwa ni kweli. Alikuwa na ahadi ya Mungu. Maana, Yeye alisema, katika Yohana 5:19, kwamba, “Mwana hawezi kufanya lolote kwa nafsi Yake, ila lile amwonalo Baba analitenda.” Tayari alikuwa amepata ono la yale Mungu aliyokuwa anaenda kufanya, kwa hiyo alikuwa na uhakika. Hakuna ma- . . .

369 “Sitakwenda kujaribu. Ninaenda kutenda hilo.” Amina, amina, amina. Loo, laiti ningaliweza kuchukua tu Hilo, kama kizibuo, na kukinyonganyonga katika kila mtu. Uhum. Mnaona, sio “Nitaenda nijaribu, nitaenda nione kama ninaweza.” “Nitaenda. Nitaenda nikamwamshe. Sitaenda kujaribu. Nitaenda kufanya hivyo. Nitaenda nikamwamshe,” Naye alimwamsha. Loo, jamani! Hakuna chenye mashaka. La, la. “Sitajaribu. Ninayo ahadi.”

370 Basi—basi—basi alipoondoka sasa, Yeye hakutuacha na kusema, “Vema, nitawaambia nini. Ninyi nyote enendeni ulimwenguni kote mkaunde madhehebu makuu. Na, loo, mtakuwa na mamia kadhaa yao, bali yote yatakuwa ni sawa.” Sasa, hilo lisingekuwa na uhakika. Hivyo ndivyo mwanadamu alivyofanya.

371 Ila hili ndilo Yeye alilosema kabla hajaondoka, apate kuwa na hakika hatutadanganyika. Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Huo ni wasioamini, hao watu wote wamejaa kutokuamini, hawatania Mimi tena. Hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi, Mimi, Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.”

372 Yohana 14:12, Yeye alisema, “Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, na kazi kubwa kuliko hizi mtazifanya, nyingi zake.” Hilo neno pale, kabisa, angalieni katika Kiyunani, inasema, “Nyingi zaidi mtazifanya.” Kwa nini? Yeye ni, Mungu, alikuwa katika Mtu mmoja. Sasa, Mungu yuko katika Kanisa Lake lote. Mnaona? Mungu alikuwa katika Mtu mmoja wakati huo; watu wote watakaomwamini sasa. “Nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu. Nitarudi kwenye ile Nuru niliyokuwa, ambayo iliwaongoza wana wa Israeli kupitia nyikani. Nitageuka kwenye hiyo. Halafu basi bado kitambo kidogo, nami nitakuja tena.” Mnaona? Yohana

14:12, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya,” na sasa Yeye alisema, “na nyingi kuliko hizi.”

³⁷³ Katika Marko 16, wakati alipokuwa akiondoka, Yeye alisema, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumwiwa. Na ishara hizi zita...” Ati labda? La. “Zitafuata!” Ni za hakika.

³⁷⁴ “Vema, mwajua, tunaamini Hilo, lakini, hakika, tunaishi katika siku nyingine,” lasema dhehebu. Hilo halina uhakika.

³⁷⁵ Lakini Yesu alisema, “Zitafuatana, hakika zitafuatana, zitafuatana na hao waaminio.” Watafanya nini? “Wataoa pepo; watasema kwa lugha mpya; wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Loo, ndugu!

³⁷⁶ Sio, “Wao, labda watafanya hivi. Hu—huenda wakalibadilisha na kuliundia dhehebu.” La, la. “Ishara hizi, vema, wangali watakuwa ni waaminio.” Loo, la. La, la.

³⁷⁷ “Ishara hizi zitafuata, hakika, zitawafuata.” Yeye angali ni Mungu yeye yule. Yeye hajafa. Mfumo wa Kikristo unawezaje kusema ya kwamba Yeye amefufuka katika wafu, kisha ukane kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele?

³⁷⁸ Sasa katika Mathayo 17, mkitaka kuliandika nyote, Mathayo 17—Mathayo 17:2, mnapata pale, kwenye kule kugeuka sura, sasa, kama ukipata, kama ukipata kamusi ya Kiyunani, uiangalie pale, kwenye kule kugeuka sura. Ilisema, “Akageuka sura.” Ninaamini hiyo ni... Hebu nione kama nimelipata hilo vizuri kabisa, sasa, Mathayo 17. Ninayo yote hapa.

Na baada ya siku sita Yesu akatwaa Petro, na Yakobo na Yohana nduguye, akawaleta juu ya mlima mrefu, faraghani...

Akageuka sura yake mbele yao:...

³⁷⁹ Sasa, mnajua vile Kiyunani halisi kinavyosema Yeye alifanya? Katika “aligeuzwa” mbele yao, “Aliubadilisha mtindo Wake.”

³⁸⁰ Loo, tuna muda gani? [Ndugu Neville anasema, “Siku nzima.”—Mh.] Vu—vumilieni kidogo—kidogo—kidogo tu. Sina budi tu kuliingiza hili ndani. Kitu fulani ndio kwanza kiniguse kwa nguvu, hata sina budi kukisema. Samahani. Sasa, cha—chakula cha jioni, maharagwe hayataungua. Nanyi a—achilieni tu. Vema.

³⁸¹ Yeye angali ni yule yule. Kamwe hajabadilika. Yeye angali ni yule yule. Waebrania 13:12 na 13, ilisema, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Sasa angalieni. Kama tunaamini ya kwamba Yeye alifufuka, basi kama Yeye hajafa, hayuko kwenye kaburi lolote, Yeye yu hai. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo, sivyo?

382 Vema, Yeye alifanya nini hapa wakati alipogeuka sura? Kiyunani kinasema, “Yeye alibadilisha mtindo Wake.” Loo, angalieni! Angalieni utaratibu wa ufufuo. Hilo ndilo lililonigusa wakati huo huo. Angalieni. Ni kitu gani kilichoonekana kwanza? Yeye. . .

383 Huku nyuma hapa katika mlango unaofuata, mlango wa 16, Yeye aliwaambia, “Wengine wasimamao hapo hawapaswi kufa hata watakapouona Ufalme wa Mungu ukija katika Nguvu.” Kwa maneno mengine, wangepanya nini? Wangeona muonjesho wa Ufalme wa Mungu. Wangejua utaratibu wa ufufuo na Kuja kwa Mungu. Mnaona, katika mlango wa 16.

384 Sasa hapa Yeye anapanda kule, na Yeye, kulifanyika nini, mtindo Wake ulibadilika. Kwa maneno mengine, Yeye alifunuliwa kwa njia nyingine. Mnanifuata?

385 Tuliona ufunuo ulikuwa nini, hivi majuzi usiku, katika ufunuo, ufunuo unamaanisha nini? Mchongaji, ilichimbwa hapa chini, kufanya kitu fulani; halafu basi kile afanyacho, yeye huondoa pazia tu, anasema, “Hiyo hapo.”

386 Yeye alikuwa akifanya nini tena hapa? Alikuwa akijifunua Mwenyewe katika mtindo mwingine. Yeye alikuwa ndani ya nini? Hali iliyotukuka, iliyobadilishwa; Kuja Kwake, jinsi anavyokuja, Kristo aliyetukuka, aliyegeuzwa. Mavazi Yake yaling’aa kama jua. Jamani! Loo! Alisimama katika wingu; Naye yuaja katika mawingu ya utukufu. Akafunikwa na wingu; sio maskini radi ndogo nyeupe huko ng’ambo. Bali wingu ambao anakuja ndani yake ni wingu la utukufu, malaika Wake wote pamoja na Yeye. Haleluya! Jamani! Hivyo ndivyo anavyokuja, anakuja katika wingu la utukufu.

387 Sasa, angalieni, wakati walipomwona amesimama pale. Na kabla ya hapo, walimtokea, Musa na Eliya. Angalieni. . .

388 Hilo, Musa alimaanisha nini? Musa, alikuwa, aliwakilisha wale waliokuwa wamekufa na walikuwa wamelala kaburini, maana Musa alikufa na akazikwa. Hakuna mtu ajuaye mahali alipozikwa. Lakini yeye aliwakilisha wale waliolala mauti, wakati atakapokuja.

389 Naye Eliya aliwakilisha wale waliohamishwa ambao haikuwabidi kufa. Mnaona? Haya basi. Mnaona?

390 Na Petro, Yakobo, na Yohana; waliwakilisha masalia wa Israeli waliosimama pale wakisema, “Lo, huyo ndiye Mungu wetu Yule tuliyemwamini.” Hao hapo elfu mia moja na arobaini na nne wenu. (Uko wapi, Ndugu Wood? Hilo ndilo.) Unaona? Haya basi. Petro, Yakobo, na Yohana; watatu, shahidi, kutoa wakati Yeye atakaporudi.

391 Jambo la kwanza lilikuwa ni nini? Ufufuo, Musa na (kiunganishi) Eliya walimtokea. Mnaona? Ufufuo wa wafu, na wale ambao haiwabidi kufa, walibadilishwa, nao walikuwa

wamesimama pale Mbele Zake. Loo, jamani! Naye huyo hapo amesimama, ametukuka.

³⁹² Nao hao hapo Petro, Yakobo, na Yohana; wale masalia wa Wayahudi, wakiangalia, wakisema, “Huyo Ndiye. Huyo Ndiye.” Huo ndio utaratibu wa Kuja kwa Bwana. Mnaliona? Huo hapo, ule ufufuo. Hao hapo. Loo, si ni la ajabu?

³⁹³ Sasa angalieni, jambo pekee alilofanya, Yeye alitoa kinyago chake cha ubinadamu na akawa katika hali iliyotukuka. Mnaona? Alibadilisha mtindo Wake.

³⁹⁴ Sasa, sio—sio watu watatu, kama wanavyojaribu kusema siku hizi, hayo madhehebu. Loo, ndugu! Sio watu watatu, sio watatu. Kubadilika! Sio watu watatu, bali mabadiliko matatu ya Mtu yule yule. Loo, jamani! Masalaale! Wakati mmoja, Yeye alionekana kama Baba; akaondoa kinyago, akawa Mwana; sasa Yeye anatoa hicho kinyago cha mwili, Naye ni Roho Mtakatifu. Sio miungu watatu; mabadiliko matatu ya Mungu yule yule. Loo, Jina la Bwana libarikiwe! Mabadiliko matatu ya Mtu yule yule. Mnaona?

³⁹⁵ Sasa, wakati alipokuwa duniani, Yeye alikuwa ile Nguzo ya Moto, iliyowaongoza wana wa Israeli. Hiyo ni kweli? Kisha akafanyika mwili, katika Mwana wa Mungu, kusudi apate kuonja mauti kwa ajili ya jamii yote ya wanadamu, kufanya upatanisho. Mnaamini hilo? Sasa Yeye ni nini siku hizi? Yesu yule yule. Yeye yule yule (nini?) jana, katika Ubaba; yule yule katika Uwana; yule yule hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, Nuru ile ile.

³⁹⁶ Paulo, akienda zake Dameski, alipigwa akaangushwa na Nuru. Ndipo akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

Kasema, “Mimi ni Yesu.” Uh-huh. Hiyo ni kweli.

³⁹⁷ Ni kitu gani? Mara tatu Yeye alitoa kinyago Chake.

³⁹⁸ Akatoa kinyago Chake, kutoka katika Nguzo ya Moto, na akawa (nini?) Mwanadamu, apate kuiondoa dhambi.

³⁹⁹ Kisha akatoa kinyago Chake, kama Mwanadamu, akarudi tena kuwa Roho, anayelitwa Roho Mtakatifu; Roho ya Mtu, apate kurudi na kuwa juu yako, na ndani yako, na kazi zile zile. Hum! Mnaliona, kanisa? Hakuna mashaka kuhusu hilo. “Kazi nizifanyazo, ninyi nanyi mtazifanya. Kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. . .? . . .mwisho wa ulimwengu, mwisho wa wakati, mwisho wa mambo yote. Nitakuwa pamoja nanyi, nikifanya kazi zile zile.” Sasa, hakuna mashaka kuhusu hayo.

⁴⁰⁰ Lakini unasikia mwingine akisema, “Vema, huna budi kuwa Mpresbiteri. Huna budi kuwa Mmethodisti. Ninyi. . . Sisi Wabaptisti tunalo. Sisi Wapentekoste tunalo.” Hayo yote ni makosa. Hayo ni uongo. Hayo hayana uhakika. Pentekoste inawezaje kuwa Nalo, dhehebu la Kipentekoste, wakati kuna

yapata madhehebu thelathini mbalimbali yao? Lipi Ndilo? Wamethodisti wanawezaje kuwa Nalo, wakati kukiwa na Methodisti Asili, na Huru, na Methodisti mara Methodisti mara Methodisti? Na mashirika sitini na kitu mbalimbali, nafikiri, ya Wabaptisti, na mashirika mengi mbalimbali ya Wakatoliki, na kadhalika. Wote wako wapi? Ni gani Ndilo? Hayo ni Sauti zisizotambulikana.

⁴⁰¹ Lakini unapomsikia Yeye, “Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” hiyo ni Sauti ya hakika.

⁴⁰² Kwa hiyo ni nani atakayejua jinsi ya kujifanya tayari ikiwa baragumu inatoa sauti isiyotambulikana? Ni kitu gani? Ni wapi wanakoweza, wanawezaje? Yeye anawezaje kulifanya, wakati kunayo madhehebu mia tisa mbalimbali? Vema. Huwezi kufanya hivyo.

⁴⁰³ Wakati Yeye alisema katika Matendo 2:38, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu,” hakuna mashaka kuhusu Hilo, “mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Sio “labda mtapokea; labda mnapaswa kupokea.” Lakini, “Mtapokea.” Lini? Mlipotubu. Sasa, unaweza kuingia mle pasipo kutubu, nawe hutampata. Lakini wakati umetubu kabisa na kumwamini Bwana Yesu Kristo, utampata. Hakuna kilicho na mashaka. “Utapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Hiyo ni kweli?

⁴⁰⁴ Wakati Yeye aliposema, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya. Lolote mwombalo katika Jina Langu, nitalifanya.” Hakuna chochote kilicho na mashaka. Hilo ni la hakika. Ishara hizi, “Nitakuwa pamoja nanyi.”

⁴⁰⁵ Sasa unasema, “Vema, kanisa letu haliamini mambo ya namna hiyo.” Vema, ni sauti tu isiyotambulikana.

⁴⁰⁶ Biblia inasema hivyo. Yeye alisema, Mwenyewe, “Nitakuwa pamoja nanyi. Na kazi nilizofanya wakati mmoja, sikuzote nitazifanya ndani yenu; na kuwa pamoja nanyi, hata ukamilifu wa dahari. Nao wale wanaoniamini Mimi, watakapowekewa mikono, wakiwa ni wagonjwa, watapata afya. Watapata.” Sio “labda watapata afya.”

⁴⁰⁷ “Jones alipata afya, bali Johnson hakupata.” Hilo halina uhusiano wowote nao. Iwapo Johnson aliamini kama Jones, angalipona, pia. Hiyo ni kweli?

⁴⁰⁸ Hakuna mashaka yoyote. Hukuna mashaka. “Yeye anijiaye Mimi, kamwe sitamtupa nje.” Hakuna mashaka.

⁴⁰⁹ “Vema, sasa, huenda Yeye asinipokee.” Loo, ewe maskini mtu uliyedanganyika!

⁴¹⁰ Sikiliza. Hebu nikwambie, kama mtumishi Wake. Hakuna awezaye kuja Kwake pasipo Yeye kumpokea. “Dhambi zako zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji.” Hakuna mashaka, “Nitasamehe sehemu yao, labda umefanya

jambo *hili*; na umefanya *lile*, nami nitakuwajibisha.” “Zitakuwa nyeupe kama theluji.”

411 “Vema, Yeye hatanisamehe yale niliyomfanyia mume wangu, yale niliyomfanyia mke wangu, yale niliyomfanyia dada yangu, yale niliyomfanyia ndugu yangu, yale niliyofanya.”

412 Sijali yale uliyofanya. Hakuna kilicho na mashaka. Yeye atasamehe kila kitu. “Zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu.” Hakuna kilicho na mashaka.

413 “Tubuni, mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Ahadi hii ni kwa ajili yenu, watoto wenu, wote walio mbali,” sasa angalieni sasa, angalieni, ninyi wa utatu msio na kiasi, “na kwa wote watakoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Maagizo yaya haya, yatumika katika kila kiz- . . .

414 Sio, “Huenda ikawa. Ita—itabadilika, baada ya kitambo kidogo, kuwa ‘Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.’” Ewe maskini mwalimu uliyedanganyika.

415 Mungu hawezi kubadilika. Yeye hana kikomo. Maagizo yanatumika kila wakati, unapoyatoa kwa njia ifaayo. Naam, bwana! Sasa, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ni . . .”

Nini? Maagizo haya, ubatizo huu, mfano huu wa ubatizo, huyu Roho Mtakatifu, Nguvu zizi hizi! Sio tu kupeana mikono, kusema, “Nitafungua ukurasa mpya na kufanya vizuri zaidi.” La, bwana! “Mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Nazo Nguvu za Mungu zitakuja juu yenu, zibadilishe njia zenu, mnene kwa lugha, mweke mikono juu ya wagonjwa, muwatoe pepo, mfanye mambo yale yale waliyofanya.”

Kwa ajili ya wangapi? Muda gani?

416 “Hata mwisho wa wale wanafunzi.” Wewe ni nabii wa uongo kama ukisema hivyo. Wewe ni mwalimu wa uongo kama ukisema hivyo.

417 Kwa kuwa, “Yesu Kristo,” Biblia inatufundisha ya kwamba “Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.” Nao mitume walisema hapa, ya kwamba, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, hata . . .” Semeni pamoja nami: “. . .na kwa wote watakoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Ni wangapi? Kila wakati, kila kizazi, kila rangi, kila kanuni ya imani, kila yeyote yule, wote watakoitwa na Mungu. Basi kama Mungu akikuita, Yeye anakuumuru ubatizwe katika Jina la Yesu Kristo, na kumpokea Roho Mtakatifu, ndipo Kristo Mwenyewe anaishi ndani yako. Wala hakuna sauti isiyotambulikana, hapana mashaka Kwake. Unayo Biblia. Loo, unasimama juu Yake. Unaweza kuishi juu Yake. Unaweza kufa

juu Yake. Utafufuka juu Yake. Utukufu! Ni Neno la Mungu. Whiu! Jamani!

418 Kama vile Rebeka aliyempa yule ngamia maji, ngamia yule yule aliyemnywesha maji, alimpanda, apate kukutana na bibi-arusi wake. Mungu yeye yule tunayemhubiri, Neno lenyewe ambalo ni Mungu, Mungu yule yule aliye katika Neno, atatufufua siku moja, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nao wakosoaji wetu watauawa na Nguvu zile zile zinazokuinua hata Utukufuni. Loo, jamani! Tuinuke na kupanda juu Yake.

Ninyi watu mlio wagonjwa, msije mkakosa kumwamini Mungu.

419 Je, Leo na hao wengine...Sijui kama...Je, alisambaza kadi zozote za maombi? Kadi zozote za maombi zimetolewa? Billy hakuja asubuhi ya leo. A—alishikwa na homa, jana. Na yeye—yeye...Vema. Sasa nini? Ha—hatutaihitaji. Hatutaihitaji. Sikilizeni.

420 Mnaamini yale nimehubiri kwamba ni Kweli? Unaamini kwa moyo wako wote? Ni Sauti inayojulikana kwako?

421 Hili linasikikaje? Agizo la kwanza ambalo Yesu alitoa, Mathayo 10, kwa Kanisa Lake, “Enendeni, na hizi...” Wala silisomi. Ninalinukuu tu, Mathayo 10. Ningeweza kulipata hapaa. “Aliwaita mitume Wake kumi na wawili, na akawapa mamlaka juu ya pepo wachafu, kuwatoa pepo wachafu, kuwaponya wagonjwa, na kuwafufua wafu, na kuwatoa pepo, na kuponya ukoma.” Hiyo ni kweli? Kwa kuwafanya watu kuamini, kisha kuwawekea mikono. Kuwafanya watu kuliadini, kisha kuwawekea mikono. Kuwafanya watu kuliadini, kuwawekea mikono. Hilo lilikuwa ndilo agizo Lake la kwanza wakati alipowatuma sabini Wake?

422 Agizo la mwisho alilotoa lilikuwa ni lipi? Marko 16, Maneno ya mwisho yaliyotoka midomoni mwa Bwana wetu, hapo alipoliagiza Kanisa Lake. “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa.”

423 Sasa kumbukeni, “Huenda atahukumiwa? Huenda akawa na nafasi?” Hatakuwa na nafasi yoyote kamwe. Hakuna sauti isiyotambulikana kuhusu Hilo. Iwapo haamini, atahukumiwa.

424 Sasa ni ishara za namna gani zitakazowafuata? Ishara hizi, ati “Vema, juu ya baadhi yao zitafuata; labda zitafuata; huenda ikawa zitafuata”? Ishara hizi zitafuatana nao. Wataamini katika uponyaji. Wataamini katika kuwatoa pepo. Wataamini katika kunena kwa lugha. Loo, wataamini katika kazi zote za kimbinguni za Mungu, Yesu aliyefufuka akitenda kazi pamoja nao. Hiyo ni Kweli? Hilo ndilo Neno la mwisho la Mungu? Basi amelaaniwa yeye anayekaribu kuongeza, ama kuondoa kwake. Hivyo tu ndivyo lilivyo, ndivyo lilivyo.

⁴²⁵ Je, Kanisa la Kipentekoste lilikuwa ni Kanisa la makelele, huko nyuma mwanzoni hapo Roho Mtakatifu aliposhuka kwa mara ya kwanza? Bikira Mariamu, kana kwamba alikuwa amelewa, akiyumbayumba chini ya Nguvu za Mungu, na hao wote namna hiyo. Nao hao watu wakasema, “Wamejaa divai mpya.” Hivyo ndivyo Kanisa lilivyoamriwa. Hivyo ndivyo kila Kanisa limeamriwa. Kila wakati Mungu anapokuwa na Kanisa, litakuwa ni Kanisa la namna iyo hiyo maana halina sauti isiyotambulikana.

“Vema! Vema, askofu wetu alisema . . .”

⁴²⁶ Sijali askofu anasema nini. Yale Neno lililosema! Mnaona? Huyu askofu ana sauti isiyotambulikana. Kama sauti yake inasema jambo lile lile Hili lilivyo, yeye anasema kweli. Halafu basi kama kanisa halitendi kama lilivyotenda, namna hiyo, yeye amekosea. Kama ukisema unaye, wala hutendi jinsi hiyo, basi una kasoro. Maana, hivyo ndivyo lilivyosema hasa, “Kila mmoja.” Angalieni, juu . . . Baada, akashuka kwenda nyumbani . . .

⁴²⁷ Filipo alishuka, akiwahubiria kwa Wasamaria. Akawawekea mikono, Paulo akashuka ama . . . Petro akashuka, akawawekea mikono. Wakampokea Roho mtakatifu, akafanya jambo lile lile walilofanya hapo mwanzoni.

⁴²⁸ Akapanda juu, nyumba ya Kornelio, na hapo walikuwako Wamataifa wote huko juu, Wayunani, na kadhalika. Akawawekea mikono, wakampokea Roho Mtakatifu kama walivyofanya hapo mwanzo.

⁴²⁹ Hebu niwaambie jambo fulani. Mimi ni mmishenari, mwajua, kama . . . Sasa, ninaamini mmishenari ni jamaa anayeenda na kurudi. Huyu ni mmishenari. Ukienda kule kukaa, wanamwita huyo mmishenari; lakini huyo ni mtunza nyumba, ulibadilisha tu makao yako. Mnaona? Huyu si mmishenari. Mmishenari, kwe- . . . Paulo alikuwa ni mmishenari; hakukaa. Aliendelea tu kwenda, kwenda, kwenda, mmishenari. Sio kubadilisha makao yake; kuendelea kwenda, mmishenari.

⁴³⁰ Sasa, katika huduma ya kimishenari, nitawaambia, huko chini katika ma—maeneo ya chini kabisa ya Afrika, huko chini kwenye maskini watu wa msituni, nao hata hawakujua kama walikuwa ni wanadamu ama la, kwa muda mrefu. Serikali ya Uingereza, walipoinyakua Afrika Kusini, unaweza kuingia katika msitu mdogo na hapo kuwe . . . Unaona vichaka, “burrrr” vinatikisika kama kundi la tumbili; nawe ukiangalia kote, hakuna kitu. Na ikitokea uangalie, usukume kupitia kwenye mchanga, unaona kichwa kidogo cheusi kikiangalia kote. Unaona? Alikuwa amejificha katika changarawe, akakimbia na kujifunika kwa mchanga, upesi sana. Hawakufikiria walikuwa . . . Walidhani walikuwa ni wanyama, kwa muda mrefu. Lakini unajua jinsi walivyopata kujua ya kwamba wao

walikuwa ni—walikuwa wanadamu? Walikuwa na mbwa. Naye mbwa hataishi na chochote ila mwanadamu. Mnaona? Basi wakapata kwamba walikuwa ni wanadamu.

⁴³¹ Basi chukua mmoja wa jamaa hao wadogo, na uchukue mmoja wa Wa—Wabasuto, Washangaani, Wahosa, mmoja wa hayo makabila, ambao hata hawajui mkono wa kulia wala wa kushoto, sikuzote kitu fulani, “blaa, blaa, bluu,” mwajua, wakizungumza namna hiyo. Na wanawake uchi, wanaume, na wote. Nakwambia utakalofanya. Acha tu Roho Mtakatifu amshukie, naye atafanya jambo lile lile mnalofanya papa hapa Roho Mtakatifu anapowashukia. Hakuna sauti isiyotambulikana hapo. Hakuwahi kusikia kitu kama kunena kwa lugha, maishani mwake, na, tazama, huyu hapa akinena kwa lugha kwenu.

⁴³² Lakini huyu hapa mfasiri amesimama, jamaa huyu anasimama pale na kusema, “Blaa? (Unataka kuokoka?)”

“Blaa-laa. (Naam.)”

“Yupo mtu fulani huko juu. . . (Aa-blaa, blaa, blaa, blaa?)”

“Inua mikono yako na uupokee. (Aa-blaa.)”

⁴³³ Vema, vema, loo, jamani! Huyu hapa anakwenda, akinena kwa lugha; kamwe hajapata kuisikia, hajui neno juu Yake. Hakuna mashaka kuhusu hilo. Huyu ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Mwangalie. Ataenda moja kwa moja kwenye makabila na aanze kuwaombea wagonjwa. Haikubidi kumwambia.

⁴³⁴ Nasi wanawake wa Kimarekani, ninyi wafuasi wa kanisa. Sizungumzi sana, ninyi hapa. Huu unarekodiwa, mwajua. Ninyi wafuasi wa kanisa, huko nje mkivaa kaptura, na kufanya mnavyofanya. Kila mwaka mnavua kidogo, kisha mna kaptura, kisha kaptura fupi, na halafu kaptura fupi na kaptura fupi, na yote namna hiyo. Vema, ewe maskini mfuasi wa kanisa uliyedanganyika, wewe ni mbaya kuliko walivyo huko Afrika; wakati hao wanawake waliposimama pale siku hiyo, wakati elfu thelathini walipompokea Kristo kama Mwokozi wao binafsi, kwa wakati mmoja. Nanyi mnaimba kwenye kwaya, na kuvaa kaptura uwanjani, kukata nyasi zenu, na katikati ya mji. Ninyi ni wabaya kuliko wao walivyo. Mtaninii. . . Watasimama kwenye Siku ya Hukumu na kuwafanya mjionee aibu.

⁴³⁵ Nimewaona wanawake wakisisimama pale, wakiwa uchi, hawakuwa na kitu ila kipande kidogo tu mbele yao hivyo. Na juu ya sehemu zao hapa, se—sehemu zao za matiti, hakuna kitu hata kidogo. Na ukanda mmoja tu mdogo, yapata inchi nne ama sita, ki—kidogo umezungushiwa viunoni mwao namna *hii*, ukining’inia mbele yao. Nao wanaume, pia, walisimama pale uchi wa mnyama. Hawakujua mkono wa kulia na wa kushoto. Na mara nguvu za Roho Mtakatifu zilipokuja, hao wanawake waliikunja mikono yao; pasipo na kitu cha kufunika kifua chao;

waliikunja mikono yao, katika aibu, wakaondoka. Ndipo kesho yake walikuwa na nguo. Haleluya! Hakuna—hakuna—hakuna mashaka hapo.

⁴³⁶ Roho Mtakatifu hukufanya uvae nguo. Utaninii... Anakufanya uwe na adabu. Hakuna mashaka kuhusu hilo. Hivi hamumtaki? Hivi msingetaka kumtumikia Mtu wa namna hiyo, Bwana Yesu? Ziondokeeni sauti hizi zisizojulikana.

⁴³⁷ Loo, wewe ni maskini mtu maarufu, naam, umejipamba vilivyo, na kila kitu. Unafikiri wewe ni maarufu sana. Lakini, kipenzi, unakufa. Unafikiri unaishi, nawe unakufa. Biblia ilisema, “Mwanamke aishiye kwa anasa, amekufa ingawa anaishi.” Biblia ilisema hivyo. Hiyo si sauti isiyotambulikana. Ilisema, “Amekufa.” Hiyo ni kweli. Hakuna sauti isiyotambulikana kulihusu. Ni hakika, ndugu.

⁴³⁸ Mungu ni Mungu mtakatifu. Na wakati mtu amezaliwa kwa Roho Mtakatifu, yeye ni—yeye ni mhusika. Si hilo tu, bali yeye ni mfalme, ni mtawala. Anatoka katika Taifa lingine. Ufalme wake ni huko Juu. Amejazwa na Nguvu za Mungu, Uwepo wa Mungu. Mwanamke anayefanya hivyo, huvaa nguo. Mwanamume anaishi kwa adabu na mwaminifu kwa mke wake. Mwanamke anaishi mwaminifu na mwenye adabu kwa mume wake. Hawataki chochote cha ulimwengu. Wanayafikiri yaliyo Juu. Wamemalizana na mambo ya duniani. Wao ni viumbe vipya katika Kristo. Nao ni watakatifu, wanaishi; sio wao watakatifu, bali Roho Mtakatifu huwatawala. Hawana nia yao wenyewe. Roho Mtakatifu hutenda kazi ndani yao. Hiyo ndiyo sababu wanatenda kiwazimu, kwa watu wa ulimwengu, kwa maana wanaongozwa na Ro—Roho wa Ufalme mwingine.

⁴³⁹ Loo, ninajua ndivyo ilivyo, rafiki. Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, bali sasa nimepatikana. Nilikuwa kipofu kwa mambo hayo, bali sasa ninaona. Neema ndiyo iliyofundisha moyo wangu kuhofu. Neema ndiyo iliyoiiondoa hofu yangu. Jinsi neema hiyo ilivyoonekana yenye thamani ile saa niliyoamini kwanza, nilipomjia Kristo!

⁴⁴⁰ Sasa katika kufunga. Kwa ajili ya wokovu na uponyaji pia, hebu niseme maneno haya kwa dakika moja tu.

⁴⁴¹ Paul Rader alikuwa ni rafiki yangu. Nilimjua muda mfupi tu. Nilikuwa tu mvulana, nikaketi miguuni pake; mhudumu mashuhuri aliyefia hapa sio muda mrefu uliopita California. Basi wakati alipokuwa akifa... Alishikwa na kansa, naye alikuwa akifa huko California. Kwenye maskani ambayo sasa O. L. Jagers anayo, alikuwa nayo huko juu. Maskini... Ninii tu, nasahau jina lililoitwa wakati huo, bali ni kanisa la Ulimwengu sasa. Maskani ya kale ya Paul Rader, nayo ilikuwa huko juu nyuma ya Mtaa wa Eldorado, unapoelekea huko juu, uvuke kuelekea hekalu la McPherson, upande wa pili tu wa njia kule

kwenye bustani. Sasa, ndipo wakati Paul Rader alipokuwa akilihudumia hilo, walitoka huko nje, na wakati alipokuwa . . .

442 Kabla hajafa, aliweka mikono yake juu ya bega la ndugu fulani, ninayemjua vizuri sana, rafiki wa Ern Baxter, na kusema, “Laiti ningaliupeleka ujumbe wangu wa neema kwa hawa Wapentekoste motomoto sana, na badala ya kujaribu kujipumbaza nanyi kundi la Wabaptisti, ningalikuwa hai leo hii. Lakini,” kasema, “mmenikera, nami nimefadhaika sana, na niko kwenye hali mbaya sana, hata nakufa.”

443 Kwa hiyo wakati alipolala mle chumbani, walivuta chini ma—mapazia na kadhalika, nao walikuwa wamesimama pale, wakiimba, *Karibu Zaidi Na Wewe, Mungu Wangu*. Naye alikuwa na ucheshi. Akasema, “Kwani anayekufa ni nani, mimi ama ninyi? Mnasikika zaidi sana kana kwamba mnakufa kuliko mimi,” akasema. Akasema, “Msifanye hivyo. Niimbieni nyimbo changamfu kweli, za Injili.” Ndipo maskini kundi la waimbaji wanne kutoka Chuo cha Biblia cha Moody likaanza kuimba *Msalabani Alipokufa Mwokozi Wangu*. Akasema, “Huo unasikika ni bora zaidi. Mungu asifiwe!”

444 Kasema, “Yuko wapi Luke?” Naye Luke na Paul walishikana pamoja, kama tu vile mimi na Billy, mwanangu. Walikuwa ni ndugu, nao walishikana pamoja. Kasema, “Yu wapi Luke?” Naye Luke hakutaka kumwona ndugu yake akifa, basi alikuwa kwenye chumba hicho kingine pale hospitalini. Kasema, “Nendeni mkamwite, mumwambie aje hapa.”

445 Basi alipokuja mahali Paul alipokuwa, Paul alinyosha mkono wake na kuushika wake. Ndipo Luke akajaribu kukigeuza kichwa chake. Akasema, “Luke, tumepitia kwenye vita vingi vigumu pamoja. Sivyo, ndugu?”

446 Kasema, “Naam, tumepitia. Kote katika miaka hii, tumesumbuka, ndugu. Hiyo ni kweli, vita vingi vigumu.”

447 Lakini akasema, “Luke, liwazie. Katika dakika tano kuanzia sasa, nitakuwa nimesimama katika Uwepo wa Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake.” Akaufinya mkono wa ndugu yake, kisha akafa. Hakuna chochote chenye mashaka kuhusu hilo. Alijua njia aliyokuwa anaenda. Alijua. Alikuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, Nguvu za Mungu maishani mwake.

448 Yeye alikuwa ni mkata miti, naye alikata miti na kadhalika.

Kisha akasema . . .

449 Alikuwa mmishenari, pia, kama vile mimi ninavyoenda nchi za ng’ambo. Naye pamoja na Luke, na hao wengine, walikuwa huko chini kisiwani, wakashikwa na homa kali ya maji meusi. Kama mtu yeyote anajua hiyo ni nini, ni kifo cha haraka. Nayo ni mbaya mno. Kwa hiyo, akashikwa na homa kali ya maji meusi. Ilikuwa huko nyuma kabisa misituni, ambako hakuna kitu. Yeye na maskini mke wake mpendwa walikuwa kule.

Mnajua jinsi alivyosema. . . Nimewaambia hadithi hiyo, jinsi alivyosema, “Mara ya mwisho, ilikuwa na hisia, wakati alipompa busu la kwaheri.” Na basi walikuwa huko nyuma. Basi ikawa, likaendelea kuingia giza, giza zaidi chumbani, akasema alijua alikuwa anaondoka, ama alifikiri alikuwa anaondoka.

⁴⁵⁰ Akamwambia mkewe, kasema, “Kipenzi, inakuwa giza sana hapa ndani.” Akasema, “Nakufa.”

⁴⁵¹ Naye akasema, “Loo, Paul. Paul.” Ndipo akaanguka kifudifudi akaanza kulia.

⁴⁵² Kasema, “Kipenzi, endelea tu kulia. Hebu mimi. . . Endelea kumlilia Mungu, na hebu niisikie sauti yako. Hebu mtu fulani aombe. Siwezi kuomba tena.” Kasema, “Wakati nikifa, ninataka kuisikia.”

⁴⁵³ Basi akaendelea kumlilia Mungu, “Ee Mungu, usimwache afe. Kazi yake haijamalizika bado. Endelea. . .” Lia, “Ee Mungu, naomba usimwache Paul afe.” Alikuwa amelala kumkingama, namna hiyo.

⁴⁵⁴ Ikawa giza zaidi na zaidi. Kasema, “Kipenzi, giza linaingia zaidi na zaidi, na zaidi na zaidi.”

⁴⁵⁵ Hatimaye, akazimia. Akasema, “Nilipozimia, niliota ya kwamba nilikuwa kijana mwanamume tena.” Kasema, “Nilikuwa huko juu mwituni,” huko Oregon ambako alitoka. Kasema, “Nilikuwa nimeangusha mti. Bosi akasema, akaniambia, ‘Nenda huko juu ya kilima, Paul, nami ninataka uangushe mti fulani, na zaidi sana, kisha inatupasa kutengeneza mbao.’”

⁴⁵⁶ Basi akasema alisema, “Vema, bosu.” Naye akasema angeweza kuinusa, jinsi ilivyokuwa mbichi; na jinsi alivyojisikia vizuri. Kasema alikuwa akikimbia kupitia mwituni namna hiyo. Ndipo akachukua shoka lake, na kusema angeweza kuhisi maskini shoka hilo likiama ndani ya msonobari huo laini, mwajua, msonobari huo wa Oregon. Kisha kasema, uliposhuka humo ndani. . . Mwajua, huko Kusini, wana mti uo huo, ni mgumu sana. Ukipanda juu, huko Kaskazini, basi kadiri unavyozidi kupata baridi, ndivyo miti inavyozidi kuwa miororo. Kasema angeweza kupata. . . Kasema alichukua shoka lake, na kukimbia, pamoja na maskini ile lijamu maradufu, akayapogoa matawi yote kutoka kwake. Kasema alilipigilia shoka mle ndani, kasema, “Vema, nitashuka moja kwa moja kilimani pamoja nao.”

⁴⁵⁷ Akaushika, naye akasema asingeweza kuunyanyua. Kamwe asingeweza kuunyanyua. Basi akasema alijaribu na kujaribu. Akasema alikumbuka ya kwamba misuli mizuri zaidi ya mwanadamu iko mgongoni mwake. Kwa hiyo akasema aliyaweka magoti yake pamoja, asije akajipasua, naye akainama na kuushika. Ndipo akachukua magoti yake, misuli iliyo nyuma ya miguu, hapa juu, misuli mikubwa ya miguu yake, mikononi

mwake, mgongoni mwake, akaweka misuli yake yote kwake. Basi akasema yeye alikokota, na kukokota, wala asingeweza kuunyanyua. Kasema alijitahidi sana, mpaka akajaribu na kujaribu. Kasema, “Sina budi kulipeleka hili gogo kule chini. Sina budi kulipeleka. Bosi aliagiza lipelekwe kule chini. Sina budi kulipeleka kule. Mbona,” kasema, “kwa kawaida. . . sijui nguvu zangu zote zimekwenda wapi. Kwa hiyo, ningaliweza kwa urahisi kukibeba kitu hicho mgongoni mwangu na kutembea nacho,” kasema, “lakini siwezi kuliinua.” Basi akajaribu, na kujaribu, na kujaribu. Alisema kamwe asingeweza kulinyanyua. Alijichosha tu.

⁴⁵⁸ Kasema alianguka tu kwenye huo mti. Akasema. “Huh, huh, huh! Nimejitahidi na kujitahidi. Nimejitahidi na kujitahidi, mpaka kamwe siwezi kwenda mbele. Nami ni. . . Sina budi kulipeleka hilo gogo kule chini, lakini sijui vile ninavyoweza kufanya hivyo. Siwezi kulinyanyua.” Kasema, ameketi pale tu, kwa hiyo akasema, “Sijui la kufanya.”

⁴⁵⁹ Ndipo akasema alisikia Sauti Yake, ya Bosi wake, ikisema, “Paul,” naye akasema ilikuwa ndiyo Sauti iliyo tamu kuliko zote aliyowahi kusikia.

⁴⁶⁰ Basi kasema, “Nilipogeuka kuangalia,” kasema, “haikuwa ni bosu wangu, bali ilikuwa ni Bosu wangu halisi.” Kasema, “Ilikuwa ni Yesu.”

⁴⁶¹ Yeye kasema, “Kwa nini unang’ang’ana nalo, Paul?” Kasema, “Unaona kijito kile kinachotelemkia pale?” Kasema, “Kijito hicho kinapitia moja kwa moja kambini.” Kasema, “Kwa nini usilisukume tu majini na ulipande, utelemke?”

⁴⁶² Kwa hiyo alisema alichukua tu hilo gogo na kulibingirisha majini, kisha akaruka juu yake; akapanda juu ya hayo mawimbi, akipiga tu makelele na kushangilia, akisema, “Nimepanda juu yake. Nimepanda juu yake.”

⁴⁶³ Kisha kasema, alipozinduka, humo chumbani, huku mke wake amelala juu yake, akiomba; aliruka katikati ya sakafu, akipiga makelele, “Nimepanda juu yake. Nimepanda juu yake.”

⁴⁶⁴ Ndugu, hebu nikwambie jambo fulani asubuhi ya leo. Using’ang’ane nalo. Mimi sijaribu kung’ang’ana nalo. Litakuchosha kabisa, huku na huku. “Mimi ni Mmethodisti? Mimi ni Mbaptisti? Mimi ni *hili*.” Ndio kwanza nimpokee Yesu. Nilichukua ahadi Yake, kwa neema. Akaja kwangu, nami nimepanda juu Yake. Sijali kinachofanyika, ama kiendacho, ni mara ngapi tunaitwa “wendawazimu, ama mllokole.”

⁴⁶⁵ Juu ya uponyaji wenu asubuhi ya leo, tunapoombea. . . Hatutakuwa na wakati sasa, inaelekea saa saba, kwa ajili ya mstari wa maombi. Tutawaombea wagonjwa, na kupata. . . na—na kumwombea kila mmoja hapa. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Hiyo ni kweli? “Wakiweka

mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Hiyo ni kweli? Nimepanda juu Yake. Mko tayari kupanda juu Yake?

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

⁴⁶⁶ Mungu mwenye rehema. Loo, siku hizi za mwisho, wakati saa zinapoingia giza, kanisa limebingirika kwenye Neno. Wamejisokota kupitia kwa madhehebu. Nao wanajua hilo si sawa, Bwana. Jalia tu waache kulisokota. Labda kunao watu hapa, asubuhi ya leo, ambao wametoka kanisa moja hadi lingine. Wakati mmoja walikuwa katika Methodisti, kisha katika Baptisti, halafu Pentekoste, kisha Church of God, kisha Nazarayo. Ee Mungu, jalia wakome tu kufanya hivyo.

⁴⁶⁷ Jalia waje tu, wapande juu ya ile ahadi asubuhi ya leo, Bwana; waburudike tu, wamwamini Mungu kwenye ahadi Yake, wakati Yeye aliposema, “Kama ukitubu, na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zako, utapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Mungu, jalia kwamba wangeweza kuipanda ahadi hiyo, asubuhi ya leo, waingie moja kwa moja hata kwenye bahari ya wema Wake, minyunyizo ya Uzima usio na mwisho, Maji ya Roho. Tujalie, Bwana.

⁴⁶⁸ Jalia Roho Mtakatifu, ambaye anakimbia, haraka-haraka, upya, moja kwa moja mlangoni mwao sasa, jalia waingie tu kwenye kile Kijito, kwenye ahadi ya Mungu, na kusema, “Bwana, nimepanda juu Yake. Mimi huyu hapa naja. Nimepanda juu Yake.”

⁴⁶⁹ Wajalie wagonjwa na wanaoteseka, walio wagonjwa na hawajui la kufanya, madaktari wamewakatia tamaa, wamepambana sana, kutoka hospitali hadi hospitali, kutoka mlango hadi mlango, kutoka mahali hadi mahali, hawajui la kufanya, Bwana, lakini Kijito cha Uzima kinabingirika papo hapo karibu nao, asubuhi ya leo, jalia walichukue Andiko hilo, Marko 16, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Waaminio watapata afya wakati mikono imewekwa juu yao.

⁴⁷⁰ Bwana, jalia tu waizingatie hiyo asubuhi ya leo, wapande juu Yake, na kusema, “Bwana, mimi hapa. Sijui jinsi nitakavyoenda, bali nimepanda juu Yake. Ninatolemka moja kwa moja kwenye Vijito, nikishangilia, nikiyapigapiga Maji ya Uzima kwa mikono yangu, nikiyatupa kwenye nafsi yangu, na juu ya kichwa changu, na kujiosha mwenyewe katika wema Wako, na nikifurahi ninapoenda, nimepanda juu ya ahadi Yako ambayo ulisema, “Watapata afya.” Tujalie, Baba.

Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

⁴⁷¹ Sijui kama kuna mtu kwenye jengo hili, asubuhi ya leo? Ni wangapi humu jengoni, asubuhi ya leo, ambao hawamjui Kristo kama Mwokozi wako, nawe unaamini ya kwamba kile Kijito cha Uzima kimeletwa kwako? Umesikia kila namna ya sauti zisizotambulikana. Umejenga nyumba yako juu ya vitu

ambavyo ni mchanga unaodidimia. Unatambua ya kwamba siku moja utakufa. Unaondoka huku ulimwenguni. Nawe unataka, kweli unataka kusikia Sauti ya hakika, nawe unaamini umesikia asubuhi ya leo, ya kwamba Kristo angali anakupenda. Sijali jinsi ulivyo mwenye dhambi, Yeye angali anakupenda. Nawe ungenitaka nikukumbuke kwa maombi?

⁴⁷² Na papo hapo unaposimama. Hatuwezi kukuita hapa madhabahuni. Hakuna madhabahu, maana yamejaa watoto, na kadhalika. Lakini ungetaka, unaamini ya kwamba unataka kumkubali Kristo sasa hivi kama Mwokozi wako binafsi, nawe unataka nikukumbuke kwa maombi? Waweza kuinua mkono wako. Wewe sema, “Mimi sasa...” Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, huko nyuma, nyuma kabisa. Mungu akubariki, hapa katikati. Chini upande *huu*, Mungu akubariki. “Ninamkubali Kristo sasa kama Mwokozi wangu binafsi. Ninamtaka awe mwema kwangu.” Mungu akubariki, huko nyuma kabisa. Huko nyuma kabisa katika roshani, nakuona huko nyuma. Mungu akubariki. Kungekuwako na mwingine? Inua mkono wako, haidhuru uko wapi. Vichwa vimeinamishwa. Mungu akubariki, msichana. Mungu akubariki huko nyuma, dada. Mungu akubariki huko nyuma, dada. Mimi sininii...

⁴⁷³ Hukuinua mkono wako. Lakini nilienda kumwona mume wako jana usiku, alikuwa kule hospitalini, hawezi kabisa; kutoka huko juu kwenye kanisa la ndugu. Usijali. Atakuwa mzima. Bwana alingusa papo hapo jana usiku. Niliona shida yake. Madaktari wamejaribu siku nne, kuipata, bali wasingeweza kupata chochote kwa eksirei. Lakini Roho Mtakatifu huingia kwenye kilindi sana kuliko eksirei. Kwa hiyo alipata... Ni sawa. Ata—atakuja nyumbani sasa. Huenda akaja nyumbani leo hii. Vema.

⁴⁷⁴ Mtu mwingine? Una...Huko nyuma kabisa, Mungu akubariki. “Nataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wangu binafsi. Ninataka kuwa tayari, basi. Ninajua mashaka ya nyumbani kwangu. Ninajua mashaka ya kazi yangu. Ninajua mashaka ya maisha yangu. Sijui ni wakati gani nitakapokufa. Huenda bado nikafa leo hii. Sijui. Haina uhakika. Lakini ninataka Sauti ya hakika. Ninaamini niliisikia leo kupitia kwa Injili, ya kwamba Yesu Kristo ananipenda. Nami ninataka kumkubali kama Mwokozi wangu binafsi.” Mtu fulani ambaye hawajainua mikono yao, na anataka kufanya hivyo? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Vema. Mtu mwingine inua mikono yako, ambaye hajawahi kuiinua awali. Inua mkono wako, useme, “Unikumbuke, Ndugu Branham, katika maombi.” Mungu akubariki. Vema.

⁴⁷⁵ Baba wa Mbinguni, kumekuwako na Sauti ya hakika ambayo watu hawa wameisikia. Wengi wao hapa, wengi kweli, ambao asubuhi ya leo wamekukubali Wewe kama Mwokozi

wao. Sasa, Baba, ninajua ya kwamba ni kawaida kuwaleta watu huku madhabahuni, kuomba; bali si la Kimaandiko, kwa kuwa Maandiko yalisema, “Wote waliomwamini Yeye, walibatizwa.” Kwa hiyo ninaomba, Baba, ya kwamba hawa ambao wamekuamini Wewe, ya kwamba umejifunua Mwenyewe kwao, katika Mlio huo wa uhakika wa Sauti, kwamba wanajua ni Wewe. Nao wanakutaka kama Mwokozi. Waliinua mkono wao, nipate kuwakumbuka katika maombi.

⁴⁷⁶ Ee Mungu, nikijua ya kwamba zile saa zinamalizika, nuru zinazima sasa. Nuru ya ustaarabu inazima. Nuru ya Marekani inazima. Nuru ya—ya mataifa inazima, kwa kuwa Nuru ya ulimwengu inaingia. Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utawajalia waipokee Nuru hii kuu. Tunatambua ya kwamba hakuna giza linaloweza kukaa mbele ya Nuru. Nuru ina nguvu zaidi kuliko giza.

⁴⁷⁷ Basi jalia wajue ya kwamba yapata kumi na ta...saa kumi zilizopita, jengo hili lilikuwa na giza lilivyoweza kuwa, usingeweza kuona hata kiti kimoja. Ilikuwa ni giza la usiku wa manane katika jengo hili, saa kumi zilizopita. Lakini, jua likachomoza. Giza hilo lilienda wapi? Nitafutieni. Hawawezi kupipata. Wapi ke—wapi kemia yake? Ilikuwaje kwake? Haliwezi kupatikana. Limetoweka.

⁴⁷⁸ Vivyo hivyo na dhambi zao sasa. Ambapo, dakika ishirini zilizopita, giza lilikuwa nafsini mwao; lakini wamekukubali Wewe kama Mwokozi wao sasa, na giza lote limefukuzwa. “Dhambi zenu, zilizokuwa nyingi, zimetakaswa, na sasa ni nyeupe kama theluji.” Hamwezi kuzipata tena. Zimeondolewa kwenye kile Kitabu. Zimeondolewa kwenye kumbukumbu. Damu ya Yesu Kristo ilizisamehe dhambi zao. Wajalie, kama malipo, wasimame na kubatizwa usiku wa leo katika Jina la Yesu Kristo, wakiliitia Jina la Bwana, na kumpokea Roho Mtakatifu. Lijalie, Baba. Ninawakabidhi Kwako kama kumbukumbu za Ujumbe huu asubuhi ya leo, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao.

Sasa huku mmeviinamisha vichwa vyenu.

⁴⁷⁹ Kila mmoja wenu uliyeinua mkono wako, endapo hujabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kanisa litakuwa... lina ibada usiku wa leo. Basi jitayarishe sasa, hebu mchungaji aliandike jina lako sasa, asubuhi ya leo. Ubatizo wako, huo si wa asubuhi ya leo, sivyo, ndugu? [Ndugu Neville anasema, “Kubatizwa asubuhi ya leo.”—Mh.] Naam. Wanabatiza, asubuhi ya leo; mara baada ya ibada hii, ya ubatizo. Njoo moja kwa moja huku juu. Tunazo nguo tayari kwa ajili yenu kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

⁴⁸⁰ Wewe ni Mkristo sasa. Nuru ya Mungu imeingia moyoni mwako. Kumbuka jinsi hilo lilivyo zuri. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu.” Ni kwa nini ukainua mkono wako? Kwa sababu kitu Fulani kilikwambia

hivyo. Yeye yule aliyekwambia hivyo, aliifanya hiyo ahadi. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele.” Hakuna mashaka kuhusu hilo. Unao Uzima wa milele sasa. Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote, umepita sasa kutoka mautini kuingia Uzimani. Wewe u hai milele.

⁴⁸¹ Sasa mpokee Roho Wake Mtakatifu, Nguvu za Mungu, kutenda kazi maishani mwako na kukufanya umtumikie. Naomba umpokee asubuhi ya leo, unapobatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

⁴⁸² Kwa wale walio wagonjwa na wanataka kuombewa, ninataka kuona hiyo idadi, nipate kuona kama sisi. . . Inua mkono wako. Nione ni wangapi, kama nifanyize mstari wa upambanuzi ama. . . Wapo wengi kupita kiasi. Itatubidi tu kuwaombea. Kuna wengi kupita kiasi. Kunao watu mia moja na hamsini, mia mbili, wa kuombewa. Vema.

⁴⁸³ Ni wangapi wamewahi kuona utambuzi, inua mkono wako. Vema, ninyi nyote. Hiyo ni kweli, kwa hiyo mnajua kwamba ni nini. Sasa mnaamini, asubuhi ya leo, ya kwamba mmeisikia Sauti ya Mungu?

⁴⁸⁴ Sasa nitamwomba Ndugu Wood, Ndugu Fred Sothmann, na baadhi ya wadhamini, waje hapa kwa muda mfupi tu. Baadhi yenu ndugu wadhamini, ama mashemasi, ama wowote wale, mje hapa kwa dakika moja. Sasa kidogo kutakuwa na msongamano hapa, nami ninawatakeni msaidie. Sasa kwenu ninyi, ninyi watu kwenye hili, mkono wangu wa kulia, mtakaombewa, ninawatakeni mje upande *huu* hapa. Nawe ndugu, Ndugu Collins, simama moja kwa moja mle, tafadhali. Kisha uje papa hapa chini, kusudi waweze kupitia hapa na kuombewa.

⁴⁸⁵ Nitawaombeni ninyi watoto wadogo upande *huu* wa madhabahu, kama mtaenda upande *huu* kwa dakika chache tu, kwa ajili ya Ndugu Branham; sio kwa ajili yangu, bali kwa ajili ya Bwana Yesu.

⁴⁸⁶ Sasa ninyi ndugu simameni hapa watu wapate kupita moja kwa moja, na halafu—halafu tutawachukua wote upande huu mwingine. Sasa kutoka safu hii ya kwanza papa hapa. Ndugu Charlie, sijui kama ninyi ndugu, David pamoja nawe, kama ukitaka kuja hapa juu, ama urudi nyuma kidogo upande wa nyuma? Vema. Sasa wa kwanza hapa katika safu *hii*, inuka tu namna hiyo; anzieni tu upande huo, huku kuegemea ukuta, tunapoomba, sasa, tutakapokuwa tayari kuanza. Sasa, bado. Ndipo wakati upande huu hapa, tutawatakeni nyote mrudi nyuma upande *huu*; halafu basi, halafu basi mje upande *ule*, kisha mshuke. Sasa wadhamini na hao wengine watawaweka mahali pazuri.

⁴⁸⁷ Sasa, kama huyo mama ni kiwete na hawezi kuamka, na kama vile huyu msichana mdogo hapa kwenye kiti cha

magurudumu, sasa wewe keti tu pale pale mahali ulipo. Nitakuja kwako moja kwa moja. Mnaona? Nami najua maskini Edith, yuko kule nyuma, nasi tutamleta papa hapa. Wale wasioweza kuamka, nitawajia.

488 Sasa ingetufaa nini kusimama hapa na kuzungumza, ingetufaa nini kulihubiri Neno hili la Mungu, iwapo hamlisikii? Mnaona? “Yeye asikiaye na kuamini. Yeye asikiaye!”

Mko tayari, kila mmoja wenu yuko tayari kujikabidhi kwa Mungu, na kusema, “Hilo ni Neno la Mungu. Wala sijali hali yangu ni nini, nikiisha kuombewa, nimepona kwa vyovyote vile”? Mtaliamini?

489 Sasa watu wengi wanatafuta kitu fulani, mwajua. Kama vile vipi. . . Mwanamke yule, nilipomwomba kwenye vipandio vya kule nyuma, nilimwambia, ndipo hilo likatukia. Vipi kama yeye alikuwa amesema, “Vema, mwezi wa kwanza ulipita, ninaninii tu. . . Ninakuwa mkubwa zaidi wakati wote”? Mnaona? La, la, sio yeye. Alisikia Sauti, nayo Sauti hiyo ikamwambia. Ndipo akaliamini kwa moyo wake wote. Ndipo hicho kivimbe, baada ya muda kidogo, kikashuka moja kwa moja. Na sasa yeye ni wa kawaida na mzima.

490 Leo, uko wapi? Yeye yuko hapa mahali fulani? Ninasahau jina la mama huyo. Labda mtu fulani angekumbuka. Ninayo anwani yake. Nitaita kanisani. Ninyi, nani, mnalikumbuka jina lake? [Ndugu Leo anasema, “Pearl, Pearl.”—Mh.] Ni Red- . . . Redford, ama Redfort? Tunalo jina lake na anwani, iwapo mnetaka kuandika.

491 Aliponywa papa hapa, kivimbe, kilichokuwa na uzito wa pauni thelathini. Hakuna mkwaruzo juu yake, kutokana na kisu. Ile pale picha yake, wakati alipokuwa na hicho kivimbe. Huyu hapa sasa, bila mkwaruzo popote. Mungu alimponya, akakiondoa kwake. Zile pale taarifa za daktari, ambako alimkatia tamaa, “Kufa, kwa kansa inayoyala mafigo yake.” Na sasa yeye ni kawaida na mzima, bila shida yoyote ya figo hata kidogo.

492 Yeye ni mmoja wa makumi elfu. Ni kitu gani? Si sauti isiyotambulikana. Lakini jambo ni kwamba, rafiki, unaweza kuisikia?

493 Sasa parapanda ikitoa sauti isiyotambulikana, iseme, “Vema, baadhi yao huponywa na wengine hawaponywi.” Hiyo ina mashaka. Mnaona? Usiamini hiyo.

494 Yesu alisema, “Yeyote.” Hilo lina uhakika. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiwekewa mikono juu yao, watapata afya.” Unaamini hilo sasa? Kwa moyo wako wote, liamini.

495 Nami nitamwomba mchungaji, sasa tutaninii tu...Sasa tuna ibada ya ubatizo itakayofuata huu. Kwa hiyo, unaona, basi hatutakuwa na wakati mwingi kupita kiasi.

496 Lakini nitaliombea kusanyiko, kila mgonjwa aliye humu ndani. Nao wanapopitia hapa, ninaenda...Mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Mbona, kama unaamini hilo, basi upako wa Roho Mtakatifu utakuja moja kwa moja ndani yako. Unaona? Hana budi kuja, rafiki. Sisemi...Sio kitu, kwangu. Mimi ni ninii tu...Mimi ni ndugu yenu.

497 Mimi ndimi niliye mdogo kuliko wote miongoni mwenu, bali hivyo ndivyo inavyonipasa kuwa. "Aliye mdogo sana miongoni mwenu, na—na—na..." Hebu niwe mtumishi wenu nyote. Mnaona? Hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa. Mimi ni mtumishi wenu. Wewe ni mtoto wa Mungu. Mimi, mimi ni mtumishi Wake tu. Ninajaribu kuwatumikia, mnaona. Mimi ndiye mdogo kuliko wote. Hakuna kitu kunihusu mimi, bali, mnaona, mtu fulani hana budi kuweka mkono juu yako. Na kama akinijalia kulileta Neno, basi, ninyi aminini Neno hunijia mimi. Wengi wenu sana wananiita mwaminio, halafu Neno linanijia, jiamulieni wenyewe kama ni la kweli ama si la kweli. Mnaona? Acheni Mungu aamue, kama Neno Lake. Vema, kama Hilo ni kweli, basi kila ahadi ni kweli. Haina budi kuwa. Mnaona?

498 Nuhu, yeye aliendelea tu kujenga safina. Wao wakasema, "Yeye ni mlakole. Hakuna kitu huko juu. Utayapataje hayo?"

499 "Haileti tofauti yoyote. Mungu anaweza kuiweka huko juu," na akaendelea kugonga-gonga. Ni vipi—ni vipi...?

500 Ilikuwa ni nani, mwingine, niliyenena habari zake? Musa, Musa angeandaje kule chini, kuliteka jeshi hilo? Ataitekaje Misri yote? Anawezaje kufanya hivyo, mzee mmoja, umri wa miaka themanini, mke wake na mtoto? Atalifanyaje?

501 "Hiyo si kazi yangu. Mungu alisema, 'Nenda ukaiteke,' nami ninaenda huko chini." Utawakomboaje kutoka kwenye mikono ya Farao? "Mimi, hakika nitakuwa pamoja nawe." Hakuna mashaka.

502 "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hakuna chenye mashaka. Kama unaamini, mikono iwekwe juu yako, huna budi kupona. Unaamini hilo kwa moyo wako wote?

503 Sasa, ninataka kila mtu humu ndani, anayeweza kuomba, ninakutaka uinamishe kichwa chako. Ninataka uombe kimoyomoyo. Nitaziombea nguo hizi zilizowekwa hapa, maana ninauhisi Uwepo wa Roho Mtakatifu.

504 Baba wa Mbinguni, tunakaribia kufunga ibada moja na kuingia nyingine. Wengi wamekupokea, Bwana, asubuhi ya leo. Mikono mingi iliinuliwa. Wamepita kutoka mautini kuingia Uzimani, wakati huo mpole uliopita, Nuru ndogo ilipita karibu nao. Msongo mdogo ulikuja juu ya dhamiri zao. Ilikuwa ni nini?

Walikuwa wanakufa, nao wakapita basi kutoka mautini kuingia Uzimani.

505 Kama vile punje ya ngano inavyoanguka ardhini. Jambo la kwanza, inazima; inakufa, inaoza. Ndipo chipukizi ndogo ya uhai inatoka kwake, na inazaa hindi lingine.

506 Sasa, Bwana, asubuhi ya leo, msongo mwingine mdogo wa mauti ulipita juu yao. Na ulipopita, waliamka, katika dakika chache walipoinua mikono yao. Wanajisikia kusongwa sana, kwa Neno la Mungu, Kitu fulani kikisema, “Umehukumiwa. Wewe ni mwenye dhambi. Utakufa na kwenda kuzimu. Utaangamia. Kamwe hutafufuka tena,” yale mauti yanakuja juu yao. Hatimaye wakafa mahali hapo, mpaka walipoisikia Sauti ikisema, “Lakini mimi ni Mwokozi wenu. Njoni Kwangu, nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo.”

507 Nao wakainua mikono yao, “Ninataka kumkubali Yeye kama Mwokozi wangu binafsi,” ndipo chipukizi ya Uzima ikaingia nafsini mwao. Wakachipuka tena, wapate kumleta Mkristo mwingine.

508 Mungu, jalia waende majini sasa, mbele ya kusanyiko, wakabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zao; kuwaacha watu waone kwamba wameachana kabisa na—na mambo ya ulimwengu, nao wanaenda kumtumikia Kristo tangu sasa na kuendelea. Kwa kuwa wamekufa na kuzikwa pamoja na Yeye katika ubatizo, wapate kufufuka katika Maisha mapya, kutembea katika maisha mapya.

509 Hizi hapa lesu nyingi ninazoshika kwa mikono yangu, Bwana. Zinawakilisha watu wagonjwa.

510 Sasa, katika Biblia, wakati mmoja, kama ambavyo nimenukuu hili mara nyingi: Wakati Israeli walipokuwa katika jukumu lao, wakienda kwenye nchi ya ahadi, Bahari ya Shamu iliwazuia. Mungu akaangalia chini kupitia kwa hayo mawingu, kwa macho yenye hasira, kupitia kwa ile Nguzo ya Moto. Nayo hiyo Bahari ya Shamu ikaogopa, kwa sababu Mungu alikuwa amefanya ahadi. Hakuna sauti isiyotambulikana. Bahari ilijua ya kwamba Neno la Mungu halikuwa na mashaka. Walijua lilikuwa la hakika. Israeli walielekea kwenye nchi ya ahadi. Hakuna kitu kingaliweza kusimama njiani mwao, kwa sababu Mungu alikuwa amesema hivyo. Kwa hiyo, bahari ikaogopa na kurudi nyuma, ikafanya njia kavu kupitia katikati yake. Nao wakavuka juu ya nchi kavu.

511 Sasa wapo Wakristo wengi walio wagonjwa, Bwana. Hizi hapa lesu zao. Wanasema, katika Biblia, ya kwamba, “Walichukua kutoka kwenye mwili wa Paulo, lesu, ama nguo.” Tunajua sisi si Mtakatifu Paulo. Bali tunajua ya kwamba Wewe ungali ni Mungu yule yule, pamoja na Neno lile lile na ahadi ile ile. Ninapozituma lesu hizi kwa hao walio wagonjwa na wanaoteseka, jalia ibilisi huyo aliyewafunga, aogope na kurudi

nyuma. Jalia hawa watoto wa Mungu watembea kwenda kwenye ahadi ya afya njema. Lijalie, Bwana.

⁵¹² Sasa wengi wao wako katika jengo hili. Huyu hapa mchungaji Wako, asubuhi ya leo, ndugu yangu, Neville. Hawa hapa mashemasi Wako na wadhamini waliosimama hapa, watu waliochaguliwa wa kanisa hili, ambalo Wewe unalibariki sana kwa neema, ingawa sisi hatustahili, Bwana. Lakini tunamwona Roho Wako akitenda kazi miongoni mwetu, nasi tuna furaha sana kwa ajili ya hili; inaonekana kana kwamba uamsho unatokea kwa mara ya mwisho. Ee Mungu, tuliacha yote, huko Misri, sasa tuko njiani kwenda kwenye Nchi ya ahadi. Safari ya siku chache tu nasi tutakuwa tunavuka Yordani.

⁵¹³ Na sasa, Baba Mungu, tunaomba ya kwamba Wewe utaondoa kila kizuizi njiani mwetu. Wengi wa watu hawa hawako katika hali ya kutembea taratibu. Wako hapa kwa sababu wao ni wagonjwa na wanateseka. Maradhi hayo yanawezaje kuwashikilia watu hao? Mateso hayo yanawezaje basi kuwadumisha wakiwa viwete, na katika kiti cha magurudumu, wakati wakiwa safarini kwenda kwenye Nchi ya ahadi? Haleluya! Mungu, tunapoweka mikono yetu juu ya mwili wao, jalia ibilisi aogope na kurudi nyuma. Jalia wawe katika hali ya kutembea taratibu.

⁵¹⁴ Ninakushukuru Wewe kwa ajili ya mwanamke huyo ambaye nimekuwa nikizungumzia asubuhi nzima, siwezi kumsahau. Kumwona mwanamke huyo, hata asingeweza kusimama, akiwa na hicho kivimbe kikubwa; madaktari wakimtania. Lakini, yeye alikuwa ameisikia ile Sauti, haikuwa isiyotambulikana. Ilikuwa ni Sauti ya hakika, naye akaiamini.

⁵¹⁵ Sasa, Bwana, jalia kila mgonjwa humu ndani aone... asikie Sauti ile ile, asubuhi ya leo; na awe katika hali ya kwenda taratibu, kuondoka, Bwana, kwa ajili ya safari. Tujalie, Bwana. Kila kitu kimepakiwa sasa. Loo! Tuko tayari kusonga mbele, Bwana. Tuko tayari kwenda nyikani, na kuvuka Yordani huko. Siku chache tu za safari nasi tutawasili. Mungu, jalia twende katika Nguvu za Roho Mtakatifu. Jalia daima tuwepo tunapoiona ile Nuru ikiangaza huko ng'ambo, Bwana, akiongoza njiani, yule Kristo aliyefufuka akiangaza kwenye ile Siku kamilifu. Tujalie, Baba. Sasa wakati sisi...

⁵¹⁶ Ipake mafuta mikono yetu, tupake mafuta, ili Roho Mtakatifu, aliye ndani yetu sasa, aangaze. Nurulimwengu, ile ipitayo nuruli-... Nuru ya Mungu iangazie ndani ya wagonjwa, miili minyonge, na kila mmoja wao aponywe.

⁵¹⁷ Tunasonga mbele, Bwana, kukabiliana na ibilisi. Tunasonga mbele kukabiliana na Bahari ya Shamu. Hiyo, kama kwamba ilikuwa ni Bahari ya Shamu, hiyo ni kusema, bahari ya magonjwa ambayo inawashikilia watu wasisonge mbele. Tunasonga mbele huko Roho Mtakatifu akiangazia mbele yetu,

kukabiliana na ibilisi, katika Jina la Yesu Kristo. Maradhi hayo hayana budi kurudi nyuma, kwa sababu Wewe uliangalia chini kupitia Nguvu za Neno Lako. Nao hawana budi kupata afya. Tunakuja katika Jina la Yesu, kumkabili adui. Amina. 🙏

60-1218 Sauti Isiyojulikana
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org